Kiswahili

Kitabu cha Mwanafunzi

Darasa la Tano



Taasisi ya Elimu Tanzania

Mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hakiuzwi

Kiswahili

Kitabu cha Mwanafunzi

Darasa la Tano

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI

NA TEKNOLOJIA

Cheti cha Ithibati

Na. 2055

Jina la Chapisho: Kiswahili Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tano

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978-9912-765-06-1

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 31 Mei 2025 kuwa Kitabu cha Kiada kwa ajili ya Mwanafunzi wa Darasa la Tano katika ngazi ya Elimu ya Msingi nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa Mwaka 2023.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa

Kamishna wa Elimu

For Online Use Only

Taasisi ya Elimu Tanzania

© Taasisi ya Elimu Tanzania 2025

Toleo la Kwanza 2018

Toleo la Pili 2025

ISBN: 978-9912-765-06-1

Taasisi ya Elimu Tanzania

Eneo la Mikocheni

132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi

S.L.P. 35094

14112 Dar es Salaam

Simu: +255 735 041 168/+255 735 041 170

Baruapepe: director.general@tie.go.tz

Tovuti: www.tie.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kukitoa kitabu hiki au sehemu yake kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

For online use only

Yaliyomo

Shukurani v

Utangulizi vi

Sura ya Kwanza

Kusimulia matukio 1

Sura ya Pili

Kubainisha nafsi 11

Sura ya Tatu

Kutumia nahau na methali 21

Sura ya Nne

Kutumia alama za uandishi 31

Sura ya Tano

Kuandika insha 39

Sura ya Sita

Kuandika barua za kiofisi 49

Sura ya Saba

Kusikiliza na kusimulia hadithi 58

Sura ya Nane

Kutafsiri ujumbe wa hadithi 65

Sura ya Tisa

Uhusika katika hadithi 73

FOR online use only

Sura ya Kumi

Kuwasilisha mawazo makuu 80

Sura ya Kumi na Moja

Utoaji wa hoja 92

Sura ya Kumi na Mbili

Kujibu barua za kirafiki 99

Sura ya Kumi na Tatu

Kuchambua mawazo katika matini 108

Sura ya Kumi na Nne

Kueleza mawazo katika matini 118

Sura ya Kumi na Tano

Kufupisha habari 127

Sura ya Kumi na Sita

Kutunga maigizo 138

FOR online use only

Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki kutoka taasisi mbalimbali za umma na binafsi walioshiriki katika kufanikisha uandishi wa kitabu hiki cha mwanafunzi. Kipekee, TET inatoa shukurani kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino cha Tanzania (SAUT), Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule (UUS), vyuo vya ualimu, Shule ya Sekondari Itiji na Shule ya Msingi Gilman Rutihinda. Pia, TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wafuatao:

Waandishi: Bi. Rose S. Chipindula (TET), Prof. Kulikoyela K. Kahigi (SAUT), Dkt. Faraja J. Mwendamseke (DUCE), Dkt. Adventina Y. Buberwa (UDSM), Dkt. Mgogo P. Yangson (Shule ya Sekondari Itiji), Bi. Agnes S. Maguga (Mstaafu - TET), Bi. Winifrida J. Mutagwaba (Chuo cha Ualimu Ilonga), Bw. Marco M. Julius (Chuo cha Ualimu Butimba), Bi. Ester K. Koroti (Chuo cha Ualimu Butimba), Bw. Oscar O. Ndalibamale (Shule ya Msingi Gilman Rutihinda), Bi. Merina A. Yohana (TET), Bi. Razia Y. Shemlugu (TET), Bw. Jailan M. Hafidhi (TET) na Bi. Editha D. Ndangilwa (TET)

Wahariri: Dkt. Titus N. Mpemba (UDSM) na Dkt. Luinasia E. Kombe (DUCE)

Msanifu: Bw. Sultan A. Tamba

Wachoraji: Alama Arts and Media Production Limited na Bw. Fikiri A. Msimbe (TET)

Mratibu: Bi. Rose S. Chipindula (TET)

Vilevile, TET inatoa shukurani kwa walimu na wanafunzi wote wa shule za msingi walioshiriki katika ujaribishaji wa kitabu hiki. Mwisho, TET inaishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha zilizofanikisha kazi ya uandishi, uchapaji na uchapishaji wa kitabu hiki.

Dkt. Aneth A. Komba

Mkurugenzi Mkuu

Taasisi ya Elimu Tanzania

For online use only

Utangulizi

Kitabu cha Kiswahili Darasa la Tano kimetayarishwa kwa kuzingatia Muhtasari wa Somo la Kiswahili Elimu ya Msingi Darasa la Tatu mpaka la Sita wa Mwaka 2023 uliotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kitabu hiki ni Toleo la Pili lililoboreshwa kutoka kitabu cha Kiswahili kilichochapishwa mwaka 2018 kwa kuzingatia Muhtasari wa Somo la Kiswahili Elimu ya Msingi Darasa la III - VII wa Mwaka 2016.

Lengo la kitabu hiki ni kukuza uwezo wako wa kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kuandika lugha ya Kiswahili. Pia, kitakuwezesha kutumia msamiati wa lugha ya Kiswahili kwa namna mbalimbali. Vilevile, kitakujengea uwezo wa kupanga mawazo yako kwa mpangilio na mtiririko unaotakiwa.

Kitabu hiki kina picha, hadithi, habari, mashairi, utenzi na igizo. Vyote hivi vitakuwezesha kujifunza kwa ufasaha. Pia, kuna maswali ya kupima ufahamu wako kutokana na ulichokisikiliza, ulichokiona au ulichokisoma. Vilevile, kitabu kina mazoezi mbalimbali yatakayokuwezesha kujenga ujuzi wako wa somo la Kiswahili.

Soma kwa makini kitabu hiki ili kuweza kujenga ujuzi wako wa kumudu somo la Kiswahili.

Jifunze zaidi kupitia maktaba mtandao:

https://ol.tie.go.tz au ol.tie.go.tz

Taasisi ya Elimu Tanzania

FOR online use only

Sura ya Kwanza

Kusimulia matukio

Utangulizi

Katika sura hii, utajifunza kutumia msamiati sahihi katika kusimulia matukio mbalimbali kwa kujiamini ili kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuwa msimuliaji mzuri wa matukio na habari kwa kuteua msamiati kulingana na wakati, wahusika, mahali, mada na mazingira mengine.



Fikiri

Namna unavyoweza kuelezea kilichoandikwa kwenye beti zifuatazo:

La tano tumeshatua, tulipimwa tukashinda,
Na akili zimekua, walimu walijipinda,
Tuwape yao maua, walimu tunawapenda,
Tupo Darasa la Tano, la nne tulishaaga.

Tupo Darasa la Tano, upimaji tumeshinda,
Juhudi letu patano, elimu iwe matunda,
Walimu yao maono, tusome na kujilinda,
Mengi tuta'yojifunza, ujuzi mwingi 'tapata.

Ufahamu

Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.

Mtego wa vitendawili

Nzige, Panya na **Kiwavi** waliishi msituni pamoja na Kipepeo, Nyoka, Ndege, Mjusi na Mzee Ngedere. Nzige, Panya na Kiwavi walikuwa marafiki walioshirikiana kwa mambo mabaya. Mara nyingi, marafiki hawa walivamia mashamba ya Binadamu na kufanya uharibifu wa mazao. Walileta kero kubwa.

For online use only

Binadamu alitumia mbinu nyingi ili kuwaangamiza viumbe hao lakini mbinu zake hazikufua dafu. Siku moja, Mzee Ngedere alikwenda kwa Binadamu kuomba kazi ya kuwaangamiza Nzige, Panya na Kiwavi.

Binadamu alicheka sana kwa kumdharau Mzee Ngedere. Mzee Ngedere akasema, “Usinicheke, ninaweza kuwakamata na hata kuwaangamiza viumbe wale waharibifu iwapo utaniamini.” Binadamu akamjibu, “Mimi nimehangaika miaka nenda miaka rudi sijaweza kuwakamata, wewe utawezaje na uzee wako?”

“Mbona unakata tamaa, hujui kuwa uzee ni dawa? Mimi ninawajua viumbe hao; hupenda sana mafumbo. Nitawakamata kirahisi sana kwa mtego wa vitendawili,” Mzee Ngedere alieleza.

“Utahitaji malipo gani?” Binadamu aliuliza. Mzee Ngedere akamjibu kuwa atajilipa kwa kuchukua mazao anayoyataka shambani kwa binadamu. Binadamu alimruhusu Mzee Ngedere. Mzee Ngedere akaandaa tangazo kuwa kutakuwa na shindano la kutegua vitendawili. Aliahidi zawadi ya shamba na ghala la chakula kizuri kwa atakayetegua kitendawili chake kwa usahihi.

Nzige, Panya na Kiwavi walilipata tangazo hilo wakiwa wame**jibanza** mafichoni. Nzige akawauliza wenzake, “Rafiki zangu, hivi mnaujua utamu wa vitendawili?” Kiwavi akajibu, “Mimi ninaujua. Vitendawili ni vitamu kuliko hata chakula. Twendeni nikawaoneshe uhodari wangu wa kutegua vitendawili.”

Panya naye hakuwa nyuma. Akasema, “Hilo shamba na ghala lazima nivipate mimi. Nitafaidi utamu wa vitendawili na nitajipatia ghala la vyakula vizuri. Lazima nife kishujaa kupata ushindi huu.”

“Hebu tusiandikie mate na wino ungalipo. Twendeni tukashindane.” Kiwavi aliwahimiza wenzake. Wote wakachapa mguu kuelekea kwenye jukwaa la kufanyia shindano. Wanyama na wadudu wengine walipowaona Panya na wenzake wakiingia ukumbini kwa **maringo**, waliwashangilia kwa nguvu. Nzige, Panya na Kiwavi wakajipanga nyuma na kuwa wa mwishomwisho ili vitendawili vigumu zaidi viishe.

FOR online use only



Kipepeo, Nyoka, Nyuki, Ndege na Mjusi ndio waliotangulia. Wote wakashindwa kutegua vitendawili vya Mzee Ngedere. Nzige, Panya na Kiwavi hawakuacha nyuma maringo yao ikiwa ni moja ya silaha ya ushindi wao. Hatimaye, ikawadia zamu ya Kiwavi. Alijinyonganyonga kwa madaha akapanda jukwaani na kusubiri kitendawili.

“Kitendawili!” Mzee Ngedere alisema. Kiwavi akajibu, “Tega.”

“Nikikutana na adui yangu nanyong’onyea. Nipatie jibu na maana yake.” Mzee Ngedere alitega na kuomba jibu. Kiwavi alichemsha bongo akajibu haraka bila kupoteza muda, “Jibu lake ugonjwa. Maana yake ni kuwa ugonjwa umefananishwa na adui; ugonjwa ni adui mkubwa wa viumbe. Binadamu akikutana na ugonjwa, anakuwa mnyonge. Hata sisi viumbe wengine vivyo hivyo.” Mzee Ngedere akamwambia, “Umepata!”

Panya alisogea akarukaruka kwa mikogo jukwaani. Mzee Ngedere akamtegea kitendawili chake, “Adui tumemzingira lakini hatumuwezi.” Panya akajibu, “Jibu lake ni moto. Maana yake ni kuwa hata tukiwa wengi kiasi gani hatuwezi kukabiliana na joto la moto tunaouota. Moto umefananishwa na adui ambaye watu wamemzunguka kana kwamba wanamshambulia.” Mzee Ngedere akamwambia, “Umepata.”

Baada ya Panya kutegua kitendawili, Nzige akawa wa mwisho kutegua kitendawili chake. Mzee Ngedere akatega akisema, “Ukumbuu wa babu mrefu.” Nzige aliyainuainua mabawa yake kwa mbwembwe na kutoa sauti ya nti nti nti! Kisha

For online use only

akajibu, “Njia! Maana yake ni kwamba njia ni ndefu kama ukumbuu. Kitendawili hiki kinafananisha urefu wa njia na mshipi.”

Mzee Ngedere aliwapongeza marafiki hao watatu kwa kutegua vitendawili na kuvipatia maana zake kwa usahihi. Akawaomba waende kwenye chumba cha mapumziko ili wasubiri hatua ya pili. Waliingia kwenye chumba mlimokuwa na chakula kizuri kilichoandaliwa na Mzee Ngedere. Wakaanza kula. Siku za mwizi ni arobaini, na ujanja mwingi mbele kiza. Walipo**gutuka** wakajikuta wamekwishafungiwa humo, huku nje binadamu akiwatazama kwa **dhihaka**. Wakadhani ni **kiinimacho**. Kumbe Mzee Ngedere alikuwa amekula njama kuwakamata kwa **hila** na hilo lilikuwa gereza la waharibifu wa mazao.

Binadamu alimshukuru Mzee Ngedere kwa msaada wake akisema, “Ama kweli umdhaniaye ndiye kumbe siye! Mzee Ngedere naye alimshukuru Binadamu kwa kumpatia nafasi, kisha akarejea mlimani. Kama malipo ya kazi hiyo, Mzee Ngedere wakati mwingine huenda kwenye mashamba ya binadamu na kula mazao.

Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Nzige, Panya na Kiwavi walivamia mashamba ya binadamu ili kufanya nini?
2. Binadamu alijaribu kuwaangamiza Panya na wenzake kwa muda gani bila mafanikio?
3. Kwa nini binadamu alimcheka Mzee Ngedere aliposema anaweza kuwakamata Nzige, Panya na Kiwavi?
4. Taja zawadi mbili ambazo Mzee Ngedere aliahidi kumpa mshindi wa kutegua vitendawili.
5. Katika jamii unayoishi ni vitendo vipi vya udanganyifu vinavyoweza kuhusianishwa na kisa hiki?
6. Nani aliyewaambia wenzake wasiandikie mate na wino ungalipo?
7. Mzee Ngedere alitumia mbinu gani kuwakamata Nzige, Panya na Kiwavi? Pendekeza njia nyingine za kuwanasa maadui hao.
8. Unadhani binadamu alimuahidi Mzee Ngedere malipo ya kuchukua mazao shambani kutoka moyoni? Kwa nini?
9. Eleza kwa ufupi matukio yaliyotokea katika hadithi uliyoisoma.
10. Taja nyakati zilizotumika katika hadithi hii, kisha eleza kwa nini zimetumika.
11. Umejifunza nini kutokana na hadithi hii?

FOR Online Use Only

Zoezi la pili: Msamiati

Eleza maana ya maneno yafuatayo kisha tunga sentensi mbili kwa kila neno.

1. kiwavi
2. jibanza
3. maringo
4. gutuka
5. dhihaka
6. kiinimacho
7. hila

Zoezi la 3: Nahau na misemo

Eleza maana za nahau na misemo ifuatayo kama ilivyotumika kwenye hadithi uliyoisoma.

Mfano: Kufa kishujaa - *ni kupambana kwa nguvu zote mpaka mwisho hata kama utashindwa*

Acha nyuma - *kuwa huwazii tena/sahau/puuza*

1. chapa mguu
2. kata tamaa
3. chemsha bongo
4. kula njama
5. miaka nenda miaka rudi
6. uzee ni dawa
7. leta kero

Zoezi la 4: Vitendawili

A. Tegua na eleza matukio katika vitendawili vifuatavyo:

Mfano:

Kitendawili - *Akitokea, watu wote humwona – jua*

Tukio - *Jua huchomoza asubuhi. Sote tunalitegemea jua. Tukiota jua la asubuhi, tunapata vitamini D. Wakati mwingine, tunafua nguo na kuzianika juani ili zikauke.*

Kitendawili - *Hasemi na akisema hatasahaulika – kalamu*

Tukio - *Nilitumia kalamu kumwandikia rafiki yangu wimbo ambao kila mara huurudia kuusoma na kuuimba.*

For Online use only

(i) Mtungini mwangu hamuingii kata.

(ii) Wakikua mama yao huwatupa mbali kwa kishindo.

(iii) Kondoo wetu ana nyama nje na ngozi ndani.

(iv) Teketeke huzaa gumugumu na gumugumu huzaa teketeke.

(v) Akitembea huringa hata akiwa hatarini.

(vi) Nina wanangu watatu, akitoka mmoja wawili hawafanyi kazi.

(vii) Kipara cha babu kinafuka moshi.

(viii) Wali wa mama mtamu.

(ix) Wana wa mfalme ni wepesi kujificha.

(x) Fuu fuu funua, fuu fuu funika.

B. Tega vitendawili kutokana na picha zifuatazo:

(i)



(ii)



(iii)



(iv)



(v)



(vi)



For online use only

Zoezi la 5: Methali

Kamilisha methali zifuatazo:

Mfano: Polepole ……

Polepole <u>ndio mwendo.</u>

…… heri ya mtu.

<u>Maasi hufilisi</u> heri ya mtu.

1. Mtaka yote kwa pupa ……
2. ……, sharti ainame.
3. …… yasiyo na ncha.
4. Akufaaye kwa dhiki ……
5. Hakuna masika ……
6. Siku za mwizi ……
7. …… mbele kiza.
8. Masukuzi ya leo ……
9. …… kuna wakati atawika.
10. Ukimfukuza sana mjusi ……

Zoezi la 6: Mazoezi ya lugha

A. Kanusha sentensi zifuatazo:

Mfano: Mzee Ngedere ana busara.

Mzee Ngedere hana busara.

Abiria anapaswa kuchunga mzigo wake.

Abiria hapaswi kuchunga mzigo wake.

(i) Panya, Nzige na Kiwavi walishirikiana kwa mambo mema.

(ii) Binadamu ataweza kumkamata Panya na wenzake.

(iii) Viumbe hawa hupenda mafumbo.

(iv) Mzee Ngedere alikula njama kuwakamata wezi.

(v) Mjusi atashinda shindano la vitendawili.

For online use only

(vi) Binadamu amemshukuru Mzee Ngedere.

(vii) Wanyama wote ni hodari wa kutegua vitendawili.

(viii) Nzige na binadamu ni marafiki.

(ix) Nzige aliyainua mabawa yake kwa mbwembwe.

(x) Panya alisogea jukwaani kwa mikogo.

B. Andika KWELI au SI KWELI

(i) Nzige, Panya, Kiwavi na Mzee Ngedere walikuwa marafiki wakubwa.

(ii) Binadamu alimlipa Mzee Ngedere ghala la chakula kinono.

(iii) Nyoka hakuweza kutegua kitendawili alichotegewa.

(iv) Panya alisema atafaidi vitendawili na kuchukua ghala la chakula.

(v) Binadamu aliwakamata Panya, Kiwavi na Nzige kwa mtego wa vitendawili.

(vi) Kiwavi aliingia ukumbini kwa mbwembwe.

(vii) Mzee Ngedere hula mazao kwenye shamba la binadamu ili kujilipa ujira.

(viii) Binadamu alikuwa amekata tamaa ya kuwakamata Kiwavi, Nzige na Panya.

C. Kamilisha habari hii kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia maneno yaliyomo kwenye kisanduku.

akawaona, wanaoga, ilijaa, akawaambia, wadudu, waliondoka, wakavaa, aliondoka, machafu, kutambua, kichocho

Watoto walikuwa (i)_____ na kuogelea kwenye dimbwi karibu na nyumbani kwao. Walizama na kuibuka kwenye yale maji (ii) _____.

Miili yao (iii)_____ matope. Haikuwa rahisi (iv)_____ sura zao. Bibi Loshi alipokuwa anapita pale, (v)___ wale watoto. “Loo! Nyie watoto mtaleta balaa! Maji hayo yana (vi)_____wengi. Tokeni haraka.” Wale watoto walitoka

(vii)_____ nguo zao. Bibi Loshi (viii)____,“Humondanimnawaduduwanaosababisha (ix) ____, homa ya matumbo na magonjwa mengine. Ondokeni wajukuu zangu.” Wale watoto (x)_____. Pia, Bibi Loshi (xi) _____ akaendelea na safari yake.

For online use only

D. Panga sentensi katika mtiririko sahihi.

(i) Siku ile ilikuwa ya furaha mno, kwani ilikuwa ni mara yetu ya kwanza kupanda mlima.

(ii) Likizo ilikuwa nzuri sana kwani tulikula mahindi ya kuchoma na kuchemsha.

(iii) Sote tulipanda mlima bila shida, lakini ilipofika wakati wa kushuka ilikuwa taabu sana.

(iv) Tulishindwa kushuka kwa miguu; tukatambaa mithili ya nyoka.

(v) Mpwa alitutembeza sehemu mbalimbali za vivutio kama vile milima yenye miamba mikubwa.

(vi) Tulifika chini tukiwa hoi lakini sote tulikuwa tumefurahi kupanda mlima.

(vii) Likizo ya mwezi wa sita nilienda kwa mpwa wangu wilayani Mbulu.

E. Badili sentensi zifuatazo kuwa katika wakati uliopo na ujao.

Mfano:

Wanafunzi walienda kwenye mashindano ya kucheza ngoma.

Wanafunzi wanaenda kwenye mashindano ya kucheza ngoma.

Wanafunzi wataenda kwenye mashindano ya kucheza ngoma.

Sote tulisambaza mbolea bustanini.

Sote tunasambaza mbolea bustanini.

Sote tutasambaza mbolea bustanini.

(i) Meli iliondoka asubuhi kwenda Mafia.

(ii) Bustani za mboga zilitunzwa vizuri.

(iii) Mtoto mwenye adabu alifanya kazi kwa bidii.

(iv) Mama alienda shambani kwake.

(v) Vijana walijitahidi kulima korosho.

(vi) Kipindupindu kiliua watu wengi.

(vii) Sisi tulifanya kazi kwa kushirikiana.

(viii) Mtu mwenye busara alikuja kwenye mkutano.

For online use only

(ix) Zaina aliuza maandazi.

(x) Basi liliingia alfajiri.

(xi) Walimu wa Darasa la Tano walirudi shuleni.

(xii) Watoto hao walisoma kwa bidii.

F. Soma maneno au vifungu vya maneno kwenye kisanduku, kisha bainisha yale yanayoonesha wakati na yale yanayoonesha matukio.

mashindano, jana, mwaka jana, safari, kesho, leo, juzi, wiki ijayo, harusi, mwaka uliopita, sasa hivi, muhula huu, maonesho, kipindi hiki, mahafali, saa, dakika



Kazi ya kufanya

Simulia namna ulivyoyapokea matokeo yako ya Mtihani wa Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne.



Zoezi la 7: Utungaji

Andika hadithi yenye maneno kati ya 60 - 70 inayosimulia tukio la furaha katika sherehe ya familia yenu.

For online use only

Sura ya Pili

Kubainisha nafsi

Utangulizi

Katika sura hii, utabainisha nafsi tatu kwa kuzingatia umoja na wingi. Pia, utajifunza namna ya kutumia viwakilishi vya nafsi hizo katika sentensi au kifungu cha habari. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kutumia viwakilishi vya nafsi kwa usahihi katika miktadha mbalimbali.



Fikiri

Maneno mimi, sisi, wewe, ninyi, yeye na wao yanavyotumika katika kifungu cha habari

Ufahamu

Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.

Sisi na wao

Mimi ni Fikira. Nina marafiki wanne, Choki, Zuna, Ndina na Nito. Sisi ni wanafunzi wa Darasa la Tano katika Shule ya Msingi Idona. Tuna marafiki wengine katika Shule ya Msingi Chokoni. Wao ni Chona, Dano, Dino, Ndila na Ngau. Tulizoea kujiita “sisi” na kuwaita marafiki zetu “wao.” Nao walizoea kujiita “sisi” na kutuita sisi “wao.” Sisi na wao tunaishi vijiji jirani. Sisi tunaishi katika Kijiji cha Mkulicho. Wao wanaishi katika Kijiji cha Mkocho. Sisi na wao ni washindani wa michezo wa siku nyingi.

Wakati wa likizo ya mwezi wa kumi na mbili, tuliamua kufanya mashindano ya michezo mbalimbali. Mashindano hayo yalifanyika katika kijiji chetu. Sisi na wao tulishiriki katika mashindano hayo.

Kulikuwa na michezo mitano. Michezo hiyo ni mpira wa miguu, kukimbia, kukimbiza kuku, kuvuta kamba na kuruka kamba. Mimi nilipenda sana kukimbiza kuku na kuvuta kamba. Zuna alipenda kukimbiza kuku na kucheza mpira wa miguu. Yeye alikuwa na shauku sana ya kukimbiza kuku siku hiyo. Watu wali**furika** kuja kuangalia mashindano kati yetu. Miongoni mwa watu hao, alikuwepo pia babu **kikongwe**. Kila kikundi kiliingia uwanjani kwa mikogo. Mara, tukasikia sauti

For online use only

ya babu kikongwe ikisema, “Ninyi wajukuu zangu, kumbukeni umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu.” Sisi na wao tulianza kushindana kukimbiza kuku.



Kila kundi lilikimbiza kuku kwa ustadi mkubwa. Babu kikongwe alituangalia sana huku aki**tabasamu**. Katika mashindano hayo, Dano ndiye aliyekuwa anakaribia kumkamata kuku. Sisi tulianza kukata tamaa. Hata hivyo, mimi nilikuwa nyuma yake. Nikasikia wenzangu wakinihimiza, “Wewe kazana! Kazana! Kazana.” Nikapata nguvu za ajabu. Nikaongeza mbio hadi nikaweza kumkamata kuku. Sisi tukaanza kushangilia kwa furaha, huku wenzangu wakinipigia makofi. Mimi nikawaambia wenzangu, “Ninyi ndinyi mmenitia moyo kwa kuniambia nikazane.” Choki, Zuna, Ndina na Nito walifurahi sana huku wakirukaruka. Wakanibeba juujuu wakisema, “Wewe umekuwa mfano wa kuigwa na unastahili **pongezi**.”

Baada ya hapo, mimi, Choki, Zuna, Ndina na Nito tulipumzika pembeni ya uwanja pamoja na babu kikongwe tukiongea na kufurahi. Chona, Dano, Dino, Ndila na Ngau walikuwa wamekaa pembeni wakituangalia huku wakionesha huzuni. Walikuwa hawana furaha kwa sababu hawakushinda mchezo wa kukimbiza kuku. Babu kikongwe akawaita wakaja pale tulipokaa. Babu kikongwe akawaambia, “Asiyekubali kushindwa si mshindani. Furahini tu wajukuu zangu.”

Sisi na wao tukaanza kuongea pamoja. Sisi tulibeba vyakula kama maziwa na mihogo. Wao walibeba vyakula kama mayai, viazi na nyama. Sisi tulitamani vyakula vyao na wao walitamani vyakula vyetu. Tuliamua tule chakula kwa pamoja. Mimi nilikula sana hadi nikaanza kutapika. Rafiki zangu wakanicheka

sana. Babu kikongwe akawakemea kwa kunicheka. Akaniambia, “Unapokula, ukijisikia umeshiba, usiendelee kula kwa tamaa.”

Baada ya kumaliza kula, mimi nilitamani kuondoka pamoja na Chona, Dano, Dino, Ndila na Ngau. Hii ilitokana na utamu wa vyakula vyao. Choki, Zuna, Ndina na Nito walinikataza. Babu kikongwe akaniambia, “Wewe **mjukuu** wangu! Si vizuri kuondoka nao. Ni vema urudi nyumbani mapema.” Mimi niliamua kuondoka nao. Tulifika Kijiji cha Mkocho giza likiwa limeanza kuingia. Wazazi wao waliniambia nirudi nyumbani kwetu. Nikaanza kurudi nyumbani kukiwa na giza **totoro**. Njiani nilikuwa ninaogopa; nikawa ninakimbia. Ghafla, nikakanyaga kitu kilichoteleza. Nikaanguka chini, huku nikipiga kelele, “Mama wee! Mama wee! Ninakufa.” Nilihisi alikuwa nyoka. Kumbe lilikuwa ganda la ndizi.

Nilipofika nyumbani, niliwakuta wazazi wangu wamekasirika sana. Nikawaomba **msamaha**. Baba akasema, “Usirudie tena, na hutashiriki mashindano ya michezo mwaka mzima.” Mama akasema, “Ama kweli mkaidi hafaidi mpaka siku ya Idi.” Niliwaahidi sitarudia tena. Halafu, nikawasimulia kila kitu kilichotokea siku hiyo.

Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Watu gani walikuwa washindani wa michezo wa siku nyingi?
2. Watu hao walikutana wakati wa likizo kufanya nini?
3. Taja aina za michezo iliyokuwepo siku ya mashindano.
4. Marafiki zake Fikira walimwambia nini wakati wanakimbiza kuku?
5. Kwa nini Fikira aliwafuata Chona, Dano, Dino, Ndila na Ngau kijijini kwao?
6. Kuna uhusiano gani katika utamaduni wa kuomba msamaha kama alivyofanya Fikira na maadili katika jamii unayoishi?
7. Adhabu gani unayoona ingekuwa ni ya manufaa zaidi kwa Fikira? Kwa nini?
8. Andika nafsi zilizotumika katika habari uliyoisoma.
9. Ungekuwa wewe ni mshindi wa kukimbiza kuku, ungefanyia nini zawadi uliyopewa?
10. Umejifunza nini kutokana na habari uliyoisoma?

Zoezi la pili: Msamiati

Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:

1. furika
2. kikongwe
3. tabasamu
4. pongezi
5. mjukuu
6. totoro
7. msamaha

For online use only

Zoezi la 3: Miundo

Tunga sentensi mbili kwa kila muundo.

1. ..... _ngali_ ..... _ngali_ .....

Mfano: *Wewe ungalisoma kwa bidii ungalifaulu vizuri sana.*

2. ..... mara, ...

Mfano: *Mimi nilikuwa ninatembea mara, nikakimbizwa na mbwa.*

3. ..... ila .....

Mfano: *Yeye anapenda kula sana ila hapendi kula ugali.*

4. .... tuli_ .....

Mfano: *Sisi tuliibuka na ushindi.*

5. ..... _ngeli_ ..... _ngeli_ .....

Mfano: *Wao wangelicheza kwa bidii, wangelishinda mashindano.*

Zoezi la 4: Methali

Kamilisha methali zifuatazo:

Mfano: *Ajidhaniaye amesimama aangalie asianguke.*

Asiyekubali kushindwa si mshindani.

1. Mimi ni nyumba ya udongo.....
2. Mimi ni nguva .....
3. Mkono mmoja .....
4. Ukicheka na ngedere, ...
5. Usifunue kinywa, ...
6. Usiache mbachao .....

Zoezi la 5: Nahau na misemo

Eleza maana za nahau na misemo ifuatayo:

1. marafiki wa pete na kidole
2. sina budi
3. msamaria mwema
4. mpenda makuu
5. ana ulimi wa upanga

For online use only

Zoezi la 6: Mazoezi ya lugha

A. Pigia mstari neno linalowakilisha nafsi katika sentensi zifuatazo:

Mfano: *Mimi ninacheza mpira.*

Sisi tutaimba wimbo wa taifa leo asubuhi.

(i) Wewe unaimba vizuri.

(ii) Yeye anasoma kwa bidii.

(iii) Ninyi mnakula chakula.

(iv) Wao wanaruka kamba.

(v) Sisi tunarina asali.

(vi) Mimi na wewe ni marafiki sana.

(vii) Mimi na wewe ni kitu kimoja.

(viii) Wao walishindwa mpira wa kikapu.

(ix) Mimi ninalala mapema sana.

(x) Yeye anapenda kula samaki na nyama.

(xi) Sisi tunapika na wao wanalima.

(xii) Ninyi na wao mtakuja kesho.

(xiii) Mwalimu anatupenda sisi.

(xiv) Siamini kama mimi ndiye mshindi.

B. Jaza kiwakilishi sahihi cha nafsi katika nafasi zilizoachwa wazi kwenye sentensi zifuatazo:

Mfano: _____ tunalima bustani kubwa ya nyanya.

Sisi tunalima bustani kubwa ya nyanya.

(i) _____ ninakula chakula.

(ii) _____ anaimba wimbo mzuri.

(iii) _____ wanacheza vizuri sana.

(iv) _____ mnaruka juu.

For online use only

(v) _____ unalia kwa sauti.

(vi) _____ tutarudi keshokutwa.

(vii) _____ alishinda somo la Kiswahili.

(viii) _____ tulimwagilia kwa mashine za kisasa.

(ix) _____ walipiga mbizi baharini.

(x) _____ alilala na njaa.

C. Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi.

Mfano: Bwina __lienda nyumbani mapema.

Bwina alienda nyumbani mapema.

(i) Juma __naenda nyumbani.

(ii) Wao __nacheza vibaya.

(iii) Mimi __licheza vizuri sana.

(iv) Sisi __lishinda mashindano.

(v) Wewe __lichelewa kurudi nyumbani.

(vi) Ninyi __liwahi kufika.

(vii) Yeye __limpokea baba yake.

(viii) Sisi na wao __lifurahi pamoja.

(ix) Watoto __nacheza mpira vizuri.

(x) Mwalimu __litusisitiza tusome kwa bidii.

D. Kanusha sentensi zifuatazo:

Mfano: Sisi tunacheza mpira.

Sisi hatuchezi mpira.

Yeye anakula ugali na nyama.

Yeye hali ugali na nyama.

(i) Mimi ninapiga kelele.

(ii) Wewe unapiga makofi.

(iii) Ninyi mnapiga piano.

For online use only

(iv) Wao wanaimba wimbo.

(v) Yeye anaingia darasani.

(vi) Mwalimu anawaangalia wanafunzi.

(vii) Mimi ninalima shamba la bibi.

(viii) Wao wanapika makande.

(ix) Sisi tutaandika barua.

(x) Yeye anatengeneza kompyuta.

E. Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake katika kisanduku.

(i) _____ ninakwenda shuleni kila siku.

(a) Wewe

(b) Sisi

(c) Mimi

(d) Yeye

(ii) Baba amelima shamba kubwa sana. Katika neno “amelima” silabi inayoonesha nafsi ni ipi?

(a) li

(b) me

(c) ma

(d) a

(iii) Tunaimba kabla ya kuondoka shuleni. Katika neno “tunaimba”, silabi ipi inaonesha nafsi?

(a) tu

(b) a

(c) na

(d) "tu" pamoja na "na"

(iv) Wingi wa neno “unakula” ni lipi?

(a) anakula

(b) mnakula

(c) watakula

(d) wanakula

For online use only

(v) Ukanushi wa sentensi “Yeye anaingia darasani kila siku” ni upi?

(a) Yeye hataingia darasani kila siku.

(b) Yeye haingii darasani kila siku.

(c) Yeye hutaingia darasani kila siku.

(d) Yeye hawataingia darasani kila siku.

(vi) Wao walikuwa hawana furaha. Sentensi hii ipo kwenye nafsi ipi?

(a) Nafsi ya pili wingi

(b) Nafsi ya kwanza wingi

(c) Nafsi ya tatu wingi

(d) Nafsi ya tatu umoja

(vii) Uyakinishi wa sentensi “Ninyi hamkuwa washindi” ni upi?

(a) Ninyi mtakuwa washindi.

(b) Ninyi mnakuwa washindi.

(c) Ninyi mmekuwa washindi.

(d) Ninyi mlikuwa washindi.

(viii) Ipi kati ya sentensi zifuatazo ni sahihi?

(a) Sisi unatunza fedha zetu.

(b) Sisi tunatunza fedha zetu.

(c) Sisi mnatunza fedha zetu.

(d) Sisi walitunza fedha zetu.

F. Soma sentensi zifuatazo, kisha zibadilishe ziwe katika nafsi ya pili wingi.

Mfano: Wao wanacheza mpira wa miguu.

Ninyi mnacheza mpira wa miguu

Wewe unalia nini?

Ninyi mnalia nini?

(i) Wao ni wanafunzi wa Darasa la Sita.

(ii) Wanasoma Shule ya Msingi Mbugano.

For online use only

(iii) Siku moja, wakiwa darasani, mvua kubwa yenye upepo mkali ilianza kunyesha.

(iv) Ghafla, paa la darasa lao liliezuliwa.

(v) Wakati wanakimbia nje, paa liliwaangukia baadhi yao na kuwaumiza.

(vi) Walioumia walipelekwa hospitalini haraka.

(vii) Walitibiwa na kurudi nyumbani.

(viii) Wao wanatengeneza siagi ya kutosha.

(ix) Wao walikwenda kuchota maji kisimani.

(x) Sisi tunaota moto wakati wa baridi.

G. Oanisha sentensi kutoka Safu A na nafsi kutoka Safu B.

Safu A	Safu B
(i) Yeye anapenda kusoma.	(a) Nafsi ya tatu wingi
(ii) Mimi ninakunywa maji ya moto kila siku asubuhi.	(b) Nafsi ya pili umoja na wingi
(iii) Wao wanacheza mpira vizuri.	(c) Nafsi ya kwanza umoja
(iv) Sisi tunalima na kumwagilia matikiti kila siku jioni.	(d) Nafsi ya tatu umoja na wingi
(v) Wewe unafanya vizuri katika somo la Kiswahili.	(e) Nafsi ya pili wingi
(vi) Ninyi mnajenga nyumba nzuri.	(f) Nafsi ya tatu umoja
	(g) Nafsi ya pili umoja
	(h) Nafsi ya kwanza wingi

FOR Online use only

Kazi ya kufanya

Soma hadithi kutoka vyanzo mbalimbali vya TEHAMA, kisha pigia mstari viwakilishi vya nafsi.

Zoezi la 7: Utungaji

Malizia kuandika habari ifuatayo kwa maneno sabini hadi themanini (70 – 80), kisha eleza nafsi ulizozitumia.

Jina langu ni Bwina. Mimi ninasoma Darasa la Tano. Ninacheza ngoma vizuri. Nilichaguliwa kucheza ngoma siku ya mahafali ya Darasa la Sita. Nilijiandaa kucheza vizuri siku hiyo. Siku ilipofika …

For online use only

Sura ya Tatu

Kutumia nahau na methali

Utangulizi

Katika sura hii, utajifunza kutumia nahau na methali katika mazungumzo na kufafanua maana zake. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kutumia nahau na methali kwa usahihi katika mawasiliano.

Fikiri

Maana ya tukio linalofanyika katika picha ifuatayo:



Ufahamu

Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.

Jongoo na Nyoka

Hapo zamani za kale, Jongoo na Nyoka walikuwa marafiki. Jongoo, katika maumbile yake alijaliwa kuwa na macho lakini hakuwa na miguu. Tofauti na

For Online use only

Jongoo, Nyoka alijaliwa kuwa na miguu lakini hakuwa na macho. Marafiki hawa walifanya kazi bega kwa bega. Urafiki wao wa dhati ulidhihirisha kuwa *akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki wa kweli.* Jongoo na Nyoka walikuwa na rafiki yao aliyeitwa Mwewe. Siku moja, Jongoo na Nyoka walienda kumtembelea Mwewe. Nyoka alitembea polepole japokuwa alikuwa na miguu mingi. Alifanya hivyo kwa kuogopa kuji**kwaa.** Jongoo alikuwa anatambaa harakaharaka kwa sababu alikuwa anaona kila kitu. Nyoka alimtahadharisha akisema, *"Haraka haraka haina baraka."* Jongoo hakusikiliza. Aliendelea kwenda kwa mwendo wa kasi. Kwa bahati mbaya, aligonga jiwe akaanguka chini kwa kishindo. Nyoka alimsogelea na kumsaidia kuinuka. Baada ya tukio hilo, waliendelea na safari yao kwa umoja na tahadhari zaidi.



Hatimaye, walifika nyumbani kwa Mwewe. Walikuta ndege wengi wamekusanyika wakiwa wanalia. Nyoka alisikia sauti lakini hakuona kitu chochote. Alitamani sana kuwa na macho ili aone kinachoendelea. Aliamua kuuliza nini kimetokea. Mazungumzo yao yalikuwa kama ifuatavyo:

Nyoka: Kuna nini hapa jamani?

Kunguru: Oooh, bwana Nyoka! Mtoto wa Mwewe ameaga dunia.

Nyoka: Mbona sikuelewi?

Kunguru: Mtoto wa Mwewe amefariki.

Nyoka na Jongoo walishitushwa na taarifa hiyo. Waliingia ndani; wakamkuta Mwewe ameshika tama kwa huzuni kuu. Uso wake ulionesha uchungu wa kumpoteza mwanawe mpendwa. Walim**fariji** kwa kumkumbatia huku machozi yakiwalengalenga. Baada ya kimya cha huzuni, Nyoka alimfariji rafiki yao, "Pole

For online use only

sana, Mwewe!" alisema kwa sauti ya huruma. Aliendelea kusema. ''Ninatambua una uchungu mkubwa, lakini vumilia. Kufa ni faradhi ya kila mtu," Nyoka na Jongoo walikaa hapo wakiendelea kumfariji hadi siku ya kuanua matanga. Wakarudi nyumbani kuendelea na maisha yao.

Baada ya miaka kadhaa kupita, Jongoo aliugua. Alitumia kila aina ya dawa kwa siri lakini hakupata **ahueni**. Maumivu yalipozidi, alikumbuka kuwa mficha ugonjwa hufichuliwa na kilio. Akaona ni vyema kumweleza rafiki yake.

Jongoo: Rafiki yangu Nyoka, hali yangu si nzuri. Ninaumwa sana. Nimejaribu dawa nyingi lakini sijapata nafuu.

Nyoka: *(Alisema kwa masikitiko.)* Pole sana, rafiki yangu! Babu yangu amekula chumvi nyingi. Yeye ana uwezo wa kuku**tibu** haraka.

Jongoo: (*Alishangaa kusikia hivyo na kuuliza)* Mbona humu ndani tuna chumvi nyingi na kila siku tunaitumia?

Nyoka: Sina maana hiyo rafiki yangu. Nina maana kuwa babu ameishi miaka mingi, na ya kale ni dhahabu. Hivyo, ninaamini atakuponya.

Baada ya Jongoo kusikia hivyo, alikata shauri na kumwambia Nyoka aende kumleta babu yake. Nyoka alikubali ila alimwambia atachelewa kufika kwa sababu hana macho. Hivyo, alimwambia, "Kama hutajali, tubadilishane. Wewe unipe macho, na mimi nikupe miguu. Nikipata macho, nitamleta babu haraka." Jongoo alimwambia, "Basi chukua macho yangu na wewe unipe miguu yako." Nyoka aliondoka haraka kwa furaha maana aliona kila kitu kinachoendelea duniani. Alifika kwa babu yake akamwambia kuwa rafiki yake anaumwa sana hadi amekufa moyo. Hivyo, alimwomba aende haraka nyumbani kwake akamtibu. Wakiwa njiani, nyoka alimwambia babu yake am**shawishi** Jongoo amwachie macho na yeye abaki na miguu. Babu alikubali.

Walipofika, walimkuta Jongoo amelala fofofo. Walimwamsha, kisha babu alimpima. Akasema, "Unaumwa ugonjwa hatari. Nitakuchanja kisha nitakupa dawa. Halafu, nitakupaka mafuta ya ku**meremeta.** Utapona na utakuwa unang'aa wakati wote." Jongoo, baada ya kuelezwa kuhusu tiba, aliuliza gharama za **matibabu**. Babu alimweleza kwamba gharama ni kubwa sana; hivyo, asingeweza kulipa. Babu alimwambia kwamba, ili amsaidie, amwachie mjukuu wake macho na yeye abaki na miguu. Jongoo aliwaza sana. Kwa kuwa aliona anachungulia kaburi, akakubali sharti hilo ili atibiwe. Aliamini kuwa heri nusu ya shari kuliko shari kamili. Babu yake Nyoka akaanza kumtibu.

Baada ya mwezi mmoja, Jongoo alipona kabisa. Alipopona, akatamani awe na macho yake kama mwanzo. Jongoo akamwambia Nyoka amrudishie macho

For online use only

yake na yeye achukue miguu yake. Nyoka, kwa hila zake, alimkatalia Jongoo na kusema, “Nikikurudishia macho yako, ugonjwa utakurudia tena, na sitaki uingie tena kwenye mateso hayo.” Hata hivyo, ndani ya moyo wake, Nyoka alijisemea kwa kejeli, “Shukurani ya punda ni mateke.” Alijiona mwenye haki kwa uamuzi wake wa kubaki na macho. Jongoo akahisi huzuni kuona jinsi rafiki yake alivyomsaliti. Akasema, “Rafiki yangu, ninapata shida hata kuwaona maadui zangu na kujilinda dhidi yao.” Nyoka akamwambia, “Ngoja nikupe mbinu ya kujikinga na maadui. Ukihisi kitu usichokijua, jiviringe mwili wote. Jongoo alitambua ukweli kuwa kikulacho ki nguoni mwako. Tangu wakati huo, Nyoka ana macho na Jongoo ana miguu.

Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Hapo mwanzoni, nani alikuwa anatambaa harakaharaka na kuona kila kitu?
2. Jongoo na Nyoka walienda kumtembelea nani?
3. Nyoka na Jongoo walimfariji Mwewe hadi lini?
4. Kama ungepata nafasi ya kumfariji Mwewe, ungemwambia maneno gani ya faraja?
5. Jongoo alipozidiwa alikumbuka kuwa mficha ugonjwa hufichuliwa na kilio. Unaweza kuthibitishaje usemi huu?
6. Jongoo na Nyoka walibadilishana macho na miguu. Katika jamii yako ni vitu gani mnaweza kubadilishana kwa manufaa ya wengi?
7. Jongoo alitibiwa na nani na kwa makubaliano gani?
8. Baada ya kupona, Jongoo alidai nini?
9. Ungekuwa rafiki wa Jongoo, ungemsaidiaje baada ya kudanganywa na Nyoka?
10. Umejifunza nini kutokana na hadithi hii?

Zoezi la pili: Msamiati

Tunga sentensi moja kwa kila neno.

1. kwaa
2. fariji
3. ahueni
4. tibu
5. shawishi
6. meremeta
7. matibabu

For online use only

Zoezi la 3: Miundo

Tunga sentensi mbili kwa kila muundo kwa kutumia miundo ifuatayo:

1. _____po ……

   Mfano: *Walipofika, walimkuta mama yao amelala fofofo.*

2. …… japokuwa ……..

   Mfano: *Juma alienda shuleni japokuwa alikuwa anaumwa.*

3. Mbona .....

   Mfano: *Mbona hupendi kusoma?*

4. Kama hutajali, ……

   Mfano: *Kama hutajali, nipikie wali usiku.*

5. Hatimaye, ……

   Mfano: *Hatimaye, mgeni rasmi alifika ukumbini.*

6. …… kisha ……

   Mfano: *Tuliwatazama wao, kisha tukaondoka.*

Zoezi la 4: Nahau, misemo na methali

A. Toa maana ya nahau, misemo na methali zifuatazo:

(i) chapa kazi

(ii) kula chumvi nyingi

(iii) kata shauri

(iv) anua matanga

(v) kufa moyo

(vi) chungulia kaburi

(vii) shika tama

(viii) aga dunia

(ix) Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki wa kweli.

(x) Kuishi pamoja ndio kujuana.

(xi) Kufa ni faradhi ya kila mtu.

(xii) Mficha ugonjwa hufichuliwa na kilio.

(xiii) Heri nusu ya shari kuliko shari kamili.

(xiv) Shukurani ya punda ni mateke.

(xv) Kikulacho ki nguoni mwako.

For online use only

B. Chagua jibu sahihi kwa kuandika herufi yake katika kisanduku.

(i) Maana ya methali **udongo uwahi ungali maji** ni nini?

(a) Udongo ukilowa maji unakuwa mgumu.

(b) Fanya jambo udongo ukilowa.

(c) Fanya jambo mapema kabla halijawa gumu.

(d) Maji yakimwagika udongo unalowa.

(e) Maji kwenye udongo ni muhimu.

(ii) Msemo **amepigwa na butwaa** una maana gani?

(a) Amebaki akiwa na mshangao mkubwa.

(b) Amepigwa na mtu aliyeshangaa.

(c) Amepigwa na kuondoka kwa haraka.

(d) Amebaki na butwaa kubwa.

(e) Amepigwa na butwaa kubwa.

(iii) Methali **mgema akisifiwa, tembo hulitia maji** maana yake ni nini?

(a) Mtu akinywa maji mengi husifiwa na mgema.

(b) Mgema anapotengeneza pombe, huongeza maji.

(c) Mtu akizoea sifa, hujisahau na kufanya makosa.

(d) Mgema anapokwea mnazi tembo humshangilia.

(e) Mtu akizoea kusifiwa mwishowe hufanya vizuri.

(iv) Methali **bandubandu humaliza gogo** ina maana gani?

(a) Gogo linapokatwa kidogokidogo magome hutoka na kukauka.

(b) Kidogokidogo hufanikisha jambo bila mafanikio.

(c) Bandubandu ni njia ya kuondoa magogo kidogokidogo.

(d) Jambo gumu au kubwa linaweza kukamilika kwa kufanya kidogokidogo kwa juhudi na uvumilivu.

(e) Vitu vidogovidogo vikitumika mara kwa mara huisha vyote.

(v) Nahau **ana roho ya paka** maana yake ni nini?

(a) Ana hofu na woga.

(b) Ana moyo unaovimba.

(c) Anapenda kula nyama na maziwa.

(d) Ana ustahimilivu wa hali ya juu.

(e) Ana moyo unaofanana na paka.

For online use only

(vi) Maana ya methali **chanda chema huvikwa pete** ni ipi?

(a) Chanda kizuri kuvishwa pete nzuri.

(b) Mtu mwema hupata sifa nzuri.

(c) Kidole kinapendeza kikivaliwa pete.

(d) Mtu akipewa sifa huvikwa pete.

(e) Mtu mwema huvikwa pete.

(vii) Msemo **fanya juu chini** maana yake nini**?**

(a) Jaribu kila njia au mbinu kufanikisha jambo.

(b) Fanya kila kitu kwa uwazi kufanikisha jambo.

(c) Fanya kila kitu kwa kukusudia kupongezwa.

(d) Jaribu kufanya kazi kwa juhudi ili usifiwe.

(e) Fanya baadhi ya kazi usichoke.

(viii) Nahau **amekula yamini** maana yake ni nini?

(a) Amekula chakula kilichopikwa na Yamini.

(b) Ameapa kufanya jambo fulani.

(c) Anapenda kula chakula cha asubuhi.

(d) Anapenda kula chakula cha mchana.

(e) Anapenda kula chakula cha jioni.

(ix) Msemo **amemwaga unga wake** maana yake ni nini?

(a) Amepoteza kazi aliyokuwa nayo.

(b) Amemwaga unga wake chini.

(c) Amefanikiwa kupata unga mwingi.

(d) Amepata kazi yenye kipato kikubwa.

(e) Amepoteza uaminifu katika kazi.

(x) Maana ya methali **hasira hasara** ni nini?

(a) Ukifanya jambo ukiwa na hasira utapata matokeo mabaya.

(b) Hasira ni hali ambayo haikwepeki kwa mtu yeyote.

(c) Hasira ni jambo la kawaida kwa mtu anayejiamini.

(d) Ukifanya jambo kwa hasira utalifanya kwa haraka sana.

(e) Ukiwa na jambo lako lifanye ukiwa na hasira.

For online use only

C. Kamilisha methali zifuatazo kwa kuandika jibu sahihi.

(i) Asiyefikwa na jeraha .....

(ii) ..... hakina usukani.

(iii) Fahari ya macho .....

(iv) ..... kuliko kufa moyo.

(v) Ukitaja nyoka .....

(vi) ..... haviamuliwi kwa fimbo.

(vii) Upele humwota .....

(viii) Tamu ya sukari .....

(ix) Mlinda kisima .....

(x) ..... huruka na bawa lake.

D. Oanisha maana zilizopo katika Safu A na nahau zilizopo Safu B ili kupata maana iliyo sahihi.

Na.	Safu A	Safu B
(i)	Kumfuatilia au kumdhibiti mtu	A. kukata tamaa
(ii)	Kutazama kwa mshangao au tamaa	B. piga kisogo
(iii)	Fichua siri au ukweli uliojificha	C. kucheza karata chini ya meza
(iv)	Kumpuuza au kutomzingatia mtu	D. kutoa macho
(v)	Kuwa katika hali ya hatari au wasiwasi mkubwa	E. kula sahani moja
(vi)	Faidika kwa kazi au juhudi za mtu mwingine bila kushiriki	F. weka mambo hadharani
(vii)	Kufanya jambo kwa siri au hila	G. jikaze
(viii)	Ondoka au anza safari	H. kukalia kuti kavu
(ix)	Kupoteza matumaini juu ya jambo	I. kula njama
(x)	Piga moyo konde	J. kula yamini
		K. ondoka bila kuaga
		L. kula kwa jasho la mtu
		M. shika njia

For online use only

E. Bainisha nahau, misemo na methali zilizochanganywa kwenye jedwali lifuatalo:

Maji ni uhai, Mbiu ya mgambo, Majani hayalingani kwa urefu, Bahati haiji mara mbili, Beba wazazi, Mtu ni afya, Bahati ina miujiza lakini haina ahadi, Mkono kwa mkono, Mtu kwao, Watu wa damu moja, Mchovya asali hachoki kujiramba, Kaza macho, Kikubwa ni uhai, Asiyeuliza hana ajifunzalo, Heshima ya mtu ni mtu

Methali

Mfano: Asiyeuliza hana ajifunzalo.

(i) .....

(ii) .....

(iii) .....

(iv) .....

Nahau

Mfano: Watu wa damu moja.

(i) .....

(ii) .....

(iii) .....

(iv) .....

Misemo

Mfano: Heshima ya mtu ni mtu.

(i) .....

(ii) .....

(iii) .....

(iv) .....

F. Andika nahau, misemo au methali sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi.

(i) Kushirikiana na kuwa na mshikamano huleta mafanikio na nguvu zaidi.

_____

(ii) Wazazi wangu ni wasomi hivyo hupata fursa nyingi katika kuleta maendeleo ya familia na taifa. _____

For online use only

(iii) Walimu huangaza njia ya maisha kwa kutoa maarifa mbalimbali kwa jamii. _____

(iv) Mtu asipopata malezi ya wazazi au walezi atajifunza kupitia maisha ambayo yanaweza kuwa magumu. _____

(v) Furaha na tabasamu la mtoto huleta mwanga na furaha katika nyumba.

_____

Kazi ya kufanya

Kusanya nahau thelathini (30) na methali thelathini (30), kisha ziandike na maana zake katika daftari lako.

Zoezi la 5: Utungaji

Malizia hadithi hii kwa maneno yasiyopungua mia moja (100). Tumia nahau na methali zifuatazo:

1. kata tamaa
2. ponea chupuchupu
3. Subira yavuta heri
4. Baada ya dhiki faraja

Palikuwa na mzee mmoja aliyeitwa Mzee Mkungu. Aliishi katika Kijiji cha Itunja. Kijiji hiki kilikuwa karibu na pori. Mzee huyo alisifika kwa kilimo cha ndizi. Hata hivyo, alisumbuliwa sana na ngedere waliokuwa wanakula ndizi shambani mwake. Siku moja, ngedere aliamka kuelekea shambani kwa Mzee Mkungu. Alipofika, alianza kula raha bila kujua walinzi walikuwa wamejificha...

FOR online use only

Sura ya Nne

Kutumia alama za uandishi

Utangulizi

Katika sura hii, utajifunza kutumia alama za uandishi zifuatazo: nuktapacha (:), nuktamkato (;), ritifaa (') na nuktakatishi (…). Nuktapacha (:) hutumika kutambulisha orodha, kutenganisha saa, dakika na sekunde. Nuktamkato (;) hutumika kuunganisha sentensi mbili zinazohusiana bila kutumia kiunganishi na kutenganisha orodha yenye orodha ndani yake. Ritifaa (') hutumika kuonesha kuwa neno au maneno yameachwa, kwa mfano, katika ushairi. Nuktakatishi (…) hutumika kuashiria kukatishwa kwa maneno au sentensi. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kutumia alama za uandishi kwa usahihi.



Fikiri

Mahali nuktapacha (:), nuktamkato (;), ritifaa (') na nuktakatishi (...) zinapotumika

Ufahamu

Soma habari hii, kisha jibu maswali yanayofuata.

Fabu apata zawadi

Fabu, Bera na Raja ni wanafunzi wanaosoma katika Shule ya Msingi Ngindo. Wote wanasoma Darasa la Tano. Wanafunzi hawa wanaishi katika kijiji kimoja kilichopo karibu na shule yao. Fabu ni **bingwa** wa kuamka mapema kuliko Bera na Raja. Huamka saa 11:00 alfajiri kila siku. Hivyo, mara nyingi huwahi shuleni kuliko wenzake. Kila anapofika shuleni, huwahi namba, kisha kuanza kufanya usafi wa eneo lake. Eneo lake huonekana safi wakati wote. Pia, huwahi kurudi nyumbani mara tu baada ya kuruhusiwa shuleni. Vilevile, Fabu anawa**heshimu** na kuwatii wazazi, walimu na watu wote.

Tofauti na Fabu, Bera na Raja huchelewa kuamka. Hivyo, huchelewa kufika shuleni na mara nyingi hukosa namba. Maeneo yao ya shuleni huonekana machafu kila siku. Wakati mwingine, hukuta vipindi vimeanza. Baada ya kumaliza vipindi, huchelewa kurudi nyumbani. Kutokana na tabia yao, mara nyingi hupewa adhabu. Fabu anasikitishwa sana na kitendo hicho. Kwa sababu hiyo, ana**azimia**

For online use only

moyoni kwamba siku moja atawauliza wenzake kwa nini huchelewa shuleni.

Siku moja Fabu, Bera na Raja wakiwa njiani kuelekea nyumbani, Fabu aliamua kuuliza swali lake lililokuwa likim**sumbua** kwa muda mrefu, “Marafiki zangu, kwa nini huwa mnachelewa kufika shuleni?” Bera na Raja, wakiwa wametazamana, walimjibu kwa dharau, “Heee! Wewe vipi? Kwa nini unauliza?” Fabu alijibu kwa upole, “Samahani, kama nimewaudhi. Nilitaka kujua kwa sababu mara nyingi ninaona mnapewa **adhabu**. Kwani ninyi mnapenda adhabu?” Kusikia hivyo, Bera na Raja walitazama chini kisha wakajibu kwa pamoja, “Hapana! Ila huwa tunachelewa kuamka.” Fabu aliwaonea huruma akawaambia kuwa kesho yake atawapitia asubuhi na mapema. Bera na Raja walikubali.

Siku iliyofuata, Fabu aliamka mapema na kwenda kuwapitia wenzake kama alivyoahidi. Waliongozana kuelekea shuleni. Wakiwa njiani, walikutana na mzee mmoja akiwa na ng’ombe. Jina lake ni Mzee Shibuni. Fabu alimsalimia; Bera na Raja hawakumsalimia. Mzee Shibuni aliwatazama akasema, “Nyie wanangu, mbona hamnisalimii? Muwe na **adabu** kama Fabu.” Bera na Raja walinyamaza kimya. Mzee Shibuni aliamua kuondoka na ngo’mbe wake. Wakati anaondoka wote wawili walisema kwa kugugumia, “Tu…tu…tusamehe mzee”. Baada ya muda mfupi, waliwasili shuleni. Walipata namba, kisha wakaenda kufanya usafi kwenye maeneo yao. Siku hiyo, Bera na Raja hawakupewa adhabu. Walimshukuru Fabu kwa kuwapitia mapema.

Kadiri siku zilivyosonga, Fabu aliendelea kuwa mtiifu, mwenye adabu na bidii katika masomo yake. Kutokana na bidii na tabia yake njema, Fabu alikuwa akifanya vizuri katika masomo yake. Walimu walimpenda sana kutokana na bidii katika masomo na tabia yake njema. Hivyo, Fabu alisifika sana shuleni hapo kwa usafi, nidhamu bora, na kufanya vizuri katika masomo yake. Kwa kuwa shule yao ilikuwa inasisitiza masuala hayo, ilikuwa inatoa zawadi kwa wanafunzi wanaofanya vizuri katika maeneo mbalimbali wakati wa kufunga shule.

Siku ya kufunga shule ilipowadia, wanafunzi na walimu walikusanyika pamoja. Ulipofika wakati wa kutoa zawadi, Mwalimu Mkuu alianza kusoma majina ya wanafunzi waliofanya vizuri. Wanafunzi mbalimbali walipewa zawadi. Fabu, tofauti na wanafunzi wengine, alijipatia zawadi tatu tofauti. Mwalimu Mkuu alimtaja Fabu kuwa ndiye aliyeongoza katika: nidhamu, usafi, na ufaulu kwenye masomo yote.

For online use only



Wanafunzi wenzake na walimu walimshangilia kwa **nderemo** na **vifijo** kwa kupata zawadi hizo. Mwalimu Mkuu alimu**usia** Fabu aendelee kufanya hivyo na wengine waige mfano wake. Fabu alifurahi sana na aliendelea kuwa na bidii siku zote.

Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Fabu, Bera na Raja ni wanafunzi wa shule gani?
2. Nani alikuwa anawahi shuleni kuliko wenzake?
3. Fabu alikuwa na tabia gani?
4. Bera na Raja walikuwa na tabia gani?
5. Katika habari uliyoisoma, ungependa kuwa kama nani? Kwa nini?
6. Swali gani lilikuwa likimsumbua Fabu?
7. Mzee Shibuni aliwaambia nini Bera na Raja?
8. Orodhesha alama za uandishi na jina la alama husika zilizotumika katika habari hii.
9. Unafikiri kwa nini mwandishi wa habari hii ametumia alama hizo za uandishi?

Use Only
For Online

10. Habari uliyoisoma inakufundisha nini?

Zoezi la pili: Msamiati

Tunga sentensi moja kwa kila neno.

1. bingwa
2. heshimu
3. azimia
4. sumbua
5. adhabu
6. adabu
7. nderemo
8. vifijo
9. usia

Zoezi la 3: Miundo

Tunga sentensi mbili kwa kila muundo.

1. ..... **kwamba** .....

Mfano: *Fabu alisema **kwamba** atafaulu masomo yote.*

2. ..... **kuwa** .....

Mfano: *Mzee Shibuni aliwashauri **kuwa** wawe na adabu kama Fabu.*

3. ..... **kwa ajili ya** .....

Mfano: *Mwalimu Mkuu alinunua zawadi **kwa ajili ya** wanafunzi waliofanya vizuri.*

Zoezi la 4: Nahau na misemo

Eleza maana ya nahau na misemo ifuatayo, kisha tunga sentensi mbili kwa kila nahau.

Mfano: kata tamaa - *poteza matarajio ya kupata kitu*

*Buchoti aliondoka mahali pale haraka akiwa ame**kata tamaa**.*

*Nili**kata tamaa** ya kufika mapema baada ya treni kuchelewa.*

1. kaza kamba
2. piga mguu
3. vaa koti la mtu
4. vua macho
5. vunjika moyo

For online use only

Zoezi la 5: Mazoezi ya lugha

A. Badili kauli halisi zifuatazo kuwa kauli taarifa.

Mfano: Bera aliwaambia, “Nitajitahidi kuwahi kesho.”

Bera aliwaambia kwamba atajitahidi kuwahi kesho.

(i) Raja alituambia, “Siwezi kufanya usafi.”

(ii) Mwalimu Mkuu alisema, “Fabu ni mfano wa kuigwa.”

(iii) Wote walijibu, “Tunapenda kula matunda.”

(iv) Dada aliniambia, “Ninaomba maji ya kunywa.”

(v) Baba alisema, “Tutaenda kumsalimia mjomba.”

(vi) Dereva alisema, “Gari limeishiwa mafuta.”

(vii) Mwalimu alituasa, “Chezeni kwa uangalifu msiumizane.”

(viii) Fabu aliuliza, “Kwa nini mnachelewa?”

(ix) Mama alituambia, “Tutaenda sokoni kesho.”

(x) Kiranja aliuliza, “Kwa nini hamjasafisha uwanja?”

B. Badili kauli taarifa zifuatazo kuwa kauli halisi.

Mfano: Kabude alisema kuwa hawezi kuja kwetu.

Kabude alisema, “Siwezi kuja kwenu.”

(i) Mwalimu alisema kwamba atafundisha masomo yote.

(ii) Mzee alisema kwamba Tanzania ni nchi nzuri.

(iii) Kaka alisema kuwa ataanzisha bustani.

(iv) Chambi alisema kwamba atachimba mfereji wake mwenyewe.

(v) Baba alisema kuwa nitanunua gari.

(vi) Mwalimu alihoji kwamba nani alifungua mlango.

(vii) Baba alisema kuwa sisi ni watoto wazuri.

(viii) Dada alituambia kwamba tusisogee karibu na moto.

FOR Online use only

(ix) Babu alituambia kuwa anaumwa kichwa.

(x) Dereva alisema kuwa gari lake limejaa abiria.

C. Tunga sentensi kumi kutokana na jedwali lifuatalo:

Mwalimu alituusia	kwamba	alikuwa darasani
		alienda sokoni
Fabu alijibu		tuwahi shuleni siku ya Jumatatu
Bera alimwambia mwalimu	kuwa	alienda shambani
Raja alisema		ni muhimu kusoma kwa bidii
Nyakabi alitusihi		alifanya usafi wa mazingira ya shule
		Jumatano ni siku ya usafi

D. Oanisha kazi ya alama ya uandishi kutoka Sehemu A na alama za uandishi kutoka Sehemu B.

Sehemu A	Sehemu B
(i) Hutumika kuunganisha sentensi mbili zinazohusiana bila kiunganishi	A. Alama ya nuktakatishi (...)
(ii) Hutumika kukatisha maneno au sentensi	B. Alama ya nuktapacha (:)
(iii) Hutumika kuonesha kuwa maneno fulani yameachwa	C. Alama ya mshangao (!)
(iv) Hutumika kutenganisha saa na dakika	D. Alama ya mtajo (“”)
(v) Hutumika kuonesha maelezo ya ziada	E. Alama ya ritifaa (')
(vi) Hutumika kuweka pumziko fupi	F. Alama ya kuuliza (?)
(vii) Hutumika kufunga sentensi maelezo	G. Alama ya nuktamkato (;)

For Online Use Only

Sehemu A	Sehemu B
(viii) Hutumika badala ya neno “au”	H. Alama ya nukta (.)
(ix) Hutumika kufunga sentensi swali	I. Alama ya mkato (,)
(x) Hutumika kuendeleza neno ambalo halijatosha kwenye mstari	J. Alama ya kistari (-)
	K Alama ya mabano ()
	L. Alama ya mkwaju (/)

E. Jibu maswali yafuatayo:

(i) Nikikutana na maneno mengi, mimi huyadondosha na kujipachika kwenye nafasi yao. Bila mimi maneno kwenye mashairi yasingeweza kukatika na kuimbika. Mimi ni nani?

(ii) Mimi huja pale panapohitaji ufafanuzi zaidi, nikitenganisha sehemu ya kwanza na maelezo yanayofuata. Ukiandika orodha, mimi nipo mstari wa mbele. Mimi ni nani?

(iii) Sionekani mara nyingi, lakini ninapotokea huunganisha maneno yaliyokatika. Mimi ni nani?

(iv) Mimi hutumika kuashiria kukatishwa kwa maneno au sentensi. Mimi ni nani?

(v) Mimi hukaa mwishoni mwa sentensi ya maelezo kuashiria kuwa huo ndio mwisho wake. Bila mimi, maneno yote yangekimbizana. Mimi ni nani?

F. Soma habari ifuatayo, kisha iandike kwa kuzingatia alama sahihi za uandishi.

Siku hiyo nilikuwa nikifanya masahihisho ghafla simu ya nyumbani iliita nilijua ni muhimu kwani nilidhani ni ya mwalimu wangu anataka kuongea na baba yangu niliishiwa nguvu niliipokea na kuishia kusema haloo nilikimbilia chumbani kwangu nilifunga mlango nikaingia uvunguni huku nikitweta

For online use only

Kazi ya kufanya

Tembelea maktabani. Soma matini iliyotumia alama za uandishi zifuatazo: nuktapacha (:), nuktamkato (;), ritifaa (') na nuktakatishi (...), kisha nakili matini hiyo.

Zoezi la 6: Utungaji

Andika habari yoyote kwa kuzingatia matumizi ya nuktapacha (:), nuktamkato (;), ritifaa (') na nuktakatishi (…).

For online use only

Sura ya Tano

Kuandika insha

Utangulizi

Katika sura hii, utajifunza maana ya insha, hatua za uandishi wa insha na muundo wake na utaandika insha mbalimbali. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuwa mwandishi bora wa insha.



Fikiri

Uandishi wa insha unavyoweza kukusaidia katika uandishi wa matini mbalimbali

Ufahamu

Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.

Maisha ya Kanenge

Kanenge ni mwanafunzi wa Darasa la Tano katika Shule ya Msingi Ndondome. Alikuwa akiishi na shangazi yake tangu akiwa mdogo. Kila siku, alikuwa anajiuliza moyoni mwake lini atapelekwa kwa wazazi wake. Siku moja, alikaza moyo; akamuuliza shangazi yake, “Kwa nini ninaishi kwako badala ya kuishi kwa wazazi wangu?” Shangazi alimjibu, “Kanenge tulia, ipo siku utajua.” Kanenge hakuridhishwa na jibu hilo lakini alinyamaza.

Shangazi aliendelea kupika jikoni. Aliwaza sana kuhusu swali alililoulizwa na Kanenge. Moyoni mwake, alikuwa akijua ukweli kuwa Kanenge ni mtoto yatima. Wazazi wake walifariki kwa ugonjwa wa UKIMWI. Kanenge pia ni mw**athirika** wa ugonjwa huo. Shangazi aliendelea ku**tafakari** njia nzuri ya kufikisha taarifa hiyo kwa Kanenge.

Siku hiyo jioni, Kanenge alionekana hana furaha. Shangazi yake alimuuliza, “Kwa nini leo unaonekana mnyonge?” Kanenge alijibu, “Ninaumwa mwili mzima, pia nahisi baridi kali sana.”

For online use only



Shangazi aliona umuhimu wa kumuwahisha hospitali ya jirani. Alimgongea jirani yake mama wawili, na kumwomba amsindikize. Walimpakia katika gari na kumkimbiza hospitalini.

Walipofika hospitalini, waliingia katika chumba cha daktari. Kanenge alipewa nafasi ya kueleza matatizo ya afya yake. Kutokana na maelezo yake, daktari alipendekeza Kanenge afanyiwe vipimo vya maambukizi ya **virusi** vya UKIMWI. Hivyo, aliomba **ridhaa** kwa shangazi na kwa Kanenge mwenyewe. Wote walikubali. Kabla ya kuchukuliwa kipimo, daktari aliweka wazi kuhusu utaratibu wa kipimo hicho. Baada ya hapo, Kanenge alielekezwa chumba cha maabara. Akachukuliwa damu na haja ndogo.

Baadaye, waliitwa kwenda kuchukua majibu. Kabla ya kutoa majibu, daktari aliwakumbusha tena maelezo aliyowapatia kabla ya kuchukuliwa vipimo. Baada ya hapo, alisema, vipimo vimeonesha kuwa Kanenge ana maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Kanenge alishituka aliposikia majibu hayo. Alilia kwa uchungu sana. Shangazi na daktari walimbembeleza kwa maneno yenye faraja. Baadaye, Kanenge aliacha kulia. Daktari alisema, “Kesho ni siku ya kliniki kwa ajili ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Umlete akutane na watalaamu kwa ajili ya kupewa ushauri **nasaha**.”

Shangazi na Kanenge waliondoka kuelekea nyumbani. Walipofika nyumbani Kanenge alianza kulia tena. Alikuwa mtu mwenye mawazo mengi. Sura yake ili**dhoofu** na alikuwa na dalili zote za mtu aliyekata tamaa ya maisha. Shangazi

For online

alijaribu kumbembeleza, lakini Kanenge hakuonesha badiliko lolote. Muda wa kuandaa chakula ulipofika, shangazi alienda jikoni kupika. Kanenge akiwa sebuleni peke yake, aliwasha redio akaanza kusikiliza.

Ilipofika saa saba, alisikia mtangazaji akisema, “Karibuni ndugu wasikilizaji katika kipindi cha afya zetu! Mtaalamu wa afya atatufundisha kuhusu jinsi ya kuishi na virusi vya UKIMWI.” Taarifa hiyo ilipenya katika masikio ya Kanenge. Alikimbia kuelekea chumbani kwake, akachukua kalamu na karatasi, akasogea na kukaa karibu na redio. Mtaalamu alieleza mambo mengi yanayohusiana na namna ya kuishi na virusi vya UKIMWI. Kipindi hiki cha redioni kilileta matumaini mapya kwa Kanenge. Kipindi kilipokwisha, Kanenge aliandika insha hii:

Namna ya Kuishi na Virusi vya UKIMWI

UKIMWI ni ugonjwa unaosababishwa na virusi vya UKIMWI (VVU). Ugonjwa huu hudhoofisha kinga ya mwili, na kumfanya mtu kuugua magonjwa mbalimbali kwa urahisi. Hata hivyo, mtu mwenye VVU anaweza kuishi maisha marefu ikiwa atafuata ushauri wa madaktari na kujitunza vizuri.

Mtu anayeishi na VVU anapaswa kunywa dawa maalumu zinazoitwa ARV kila siku. Dawa hizi husaidia mwili kupambana na virusi vya UKIMWI na kuzuia magonjwa mengine. Pia, ni muhimu kula chakula bora kama mboga za majani, matunda na vyakula vyenye protini ili mwili uwe na nguvu.

Vilevile, anapaswa kufanya mazoezi mara kwa mara ili kuwa na afya njema na kupunguza mfadhaiko. Pia, anatakiwa kukaa na familia na marafiki wenye upendo. Hii itamsaidia kuwa na furaha na kuondoa mawazo ya upweke.

Aidha, jamii haipaswi kuwanyanyapaa watu wenye VVU, bali ina jukumu la kuwaonesha upendo na kuwasaidia. Hivyo, kila mtu anaweza kusaidia kwa kuelimisha wengine kuhusu ugonjwa wa UKIMWI na kuwa karibu na wale walioathirika.

Kila mtu mwenye VVU anaweza kuishi vizuri ikiwa atajitunza vizuri, atakunywa dawa kwa wakati na kupata msaada wa watu wanaomjali.

Baada ya kukamilisha uandishi wa insha, Kanenge alikimbilia jikoni huku akiita kwa sauti ya furaha, “Shangazi! Shangazi! Shangaziiiiiii! Ninakuita mbona husikii?” Shangazi alishituka, akauliza kwa mshangao, “Kanenge, umepatwa na nini

For online use only

tena?" Kanenge alijibu, "Nimepata taarifa njema sana redioni kuhusu maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Pia nimeandika insha kuhusu namna ya kuishi na VVU." Ninaomba nikuambie nilichosikia redioni nikusomee insha yangu." Shangazi alikubali. Walienda sebuleni na kuketi kwa ajili ya mazungumzo.



Shangazi alifurahi baada ya kuona Kanenge yupo katika hali ya uchangamfu na mwenye sura ya tabasamu. Alimpatia Kanenge nafasi ya kuongea. Kanenge alisema, "Mtaalamu wa afya ameeleza kwamba neno UKIMWI ni kifupi cha Upungufu wa Kinga Mwilini. Dalili zake ni homa kali za mara kwa mara, kupungua uzito, kuharisha, ngozi kusinyaa, mwili kukosa nguvu, kukosa hamu ya kula na kupata vidonda mwilini. Njia zinazosababisha kuenea kwa ugonjwa huo ni kama vile kuchangia vitu vyenye ncha kali, yaani wembe, pini, sindano; kuchangia mswaki; kufanya ngono na mtu mwenye VVU. Vilevile, mtaalamu amesema kwamba mtoto anaweza kupata maambukizi kutoka kwa mama mwenye VVU wakati wa kuzaliwa au kunyonya." Baada ya maelezo hayo, Kanenge alimsomea shangazi insha yake, kisha alishusha pumzi akamtazama shangazi kwa jicho la upole kama ishara ya kumpa nafasi ya kuzungumza.

Shangazi alisema, "Pole sana Kanenge! Wewe ni mtoto yatima, wazazi wako walifariki kwa ugonjwa wa UKIMWI. Ulipata maambukizi kwa bahati mbaya wakati wa kuzaliwa. Hata hivyo, usijali; nitaendelea kukuhudumia kwa kukupatia mahitaji yako yote na kukupeleka hospitalini siku za kliniki." Aidha, nitaipeleka insha yako kwenye gazeti. Ikishachapishwa watu wengi wataelimika kuhusiana na

For online use only

UKIMWI. Maelezo hayo yalimfurahisha sana Kanenge. Alimkumbatia shangazi yake, kisha akasema, “Asante sana kwa kunijali.” Shangazi akajibu, “Usijali, wahenga walisema damu ni nzito kuliko maji.”

Siku iliyofuata, shangazi alimpeleka Kanenge hospitalini. Walipewa ratiba ya siku za kuhudhuria kliniki. Baada ya afya ya Kanenge kuimarika, aliendelea na masomo yake. Aliongeza bidii zaidi katika masomo, akafaulu mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi. Aliendelea na masomo ya sekondari hadi kidato cha sita. Baadaye alisoma na kuhitimu shahada yake ya kwanza. Kisha, akaajiriwa katika kiwanda cha maziwa kilichopo katika Jiji la Shamnda. Baada ya muda, alipandishwa cheo na kuwa mkurugenzi mkuu wa kiwanda hicho. Hivi sasa Kanenge ana familia yenye watoto watatu.

Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Kanenge alikuwa anaishi na nani?
2. Habari uliyoisoma inahusu ugonjwa gani?
3. Kwa nini Kanenge alilia akiwa hospitalini?
4. Kwa nini Kanenge aliambiwa arudi hospitalini?
5. Kanenge alifanya kazi gani baada ya kuhitimu masomo ya juu?
6. Taja dalili mbili za mtu mwenye ugonjwa wa UKIMWI.
7. Taja njia mbili zinazosababisha maambukizi ya virusi vya UKIMWI.
8. Wewe ungekuwa ni Kanenge, ungefanya nini?
9. Fikiria wewe ni rafiki wa Kanenge. Ungemsaidiaje?
10. Taja vipengele ambavyo Kanenge amevizingatia katika uandishi wa insha yake.
11. Kanenge alipata maarifa muhimu kupitia redio. Wewe unaweza kupata maarifa kutoka kwenye vyanzo gani?
12. Umejifunza nini kutokana na habari uliyoisoma?

Zoezi la pili: Msamiati

Tunga sentensi mbili kwa kila neno.

1. athirika
2. tafakari
3. virusi
4. ridhaa
5. nasaha
6. dhoofu

For online use only

Zoezi la 3: Nahau na misemo

Tunga sentensi mbili kwa kila nahau na msemo.

1. kaza moyo
2. fanya papara
3. kula kisogo
4. kaa kitako
5. achia ngazi

Zoezi la 4: Methali

Kamilisha methali zifuatazo:

1. ..... ni nzito kuliko maji.
2. Yaliyopita si ndwele, …….
3. Aliye juu, ……
4. …… si mtoro.
5. Mkono mtupu ……..

Zoezi la 5: Mazoezi ya lugha

A. Bainisha sentensi zenye kauli halisi au kauli taarifa.

Mfano: Rafiki yangu aliniambia, “Ninasoma somo nilipendalo.” *Kauli halisi*

Alisema kwamba hakukuelewa. *Kauli taarifa*

(i) Amesema kwamba hawezi kuja shuleni. _____

(ii) “Tunakwenda sokoni,” tulimwambia mama. _____

(iii) Mwalimu alisema kwamba tuwe makini. _____

(iv) Wanafunzi wote walijibu, “Tumemaliza kuandika zoezi.” _____

(v) Dereva alisema kuwa abiria wote tufunge mikanda kwa usalama wetu.

_____

(vi) Ni muhimu kufahamu kuwa elimu haina mwisho. _____

(vii) “Msicheze barabarani,” kaka alituambia. _____

(viii) Shangazi aliniuliza, “Unaumwa nini?”_____

(ix) Wote waliazimia kujenga nyumba bora mwaka uliofuata. _____

(x) “Unatakiwa uanze kliniki,” daktari alimwambia Kanenge. _____

For online use only

B. Weka herufi kubwa mahali panapostahili katika sentensi zifuatazo:

(i) baba alimsisitiza ashura arudi mapema nyumbani.

(ii) hazole hajawahi kufika katika jiji la dodoma.

(iii) njalambaya hajamsalimia mama leo.

(iv) ameelekea upande wa kaskazini.

(v) mwalimu wetu ni mwenyeji wa wilaya ya butiama.

(vi) mimi nitasoma chuo cha ualimu butimba.

(vii) mto rufiji umefurika.

(viii) seni atanitembelea siku ya jumamosi.

(ix) mbuga ya serengeti ina wanyama wengi sana.

(x) shule zitafungwa mwezi novemba.

C. Kuandika kinyume cha maneno yafuatayo:

(i)	tulia	(vi)	kimbia
(ii)	injika	(vii)	funua
(iii)	gumu	(viii)	kosa
(iv)	ukaidi	(ix)	ezeka
(v)	andika	(x)	bandua

D. Andika KWELI au SI KWELI katika sentensi zifuatazo:

(i) Muundo wa insha hufanana na muundo wa barua rasmi. _____

(ii) Insha huandikwa kwa kuzingatia alama za uandishi. _____

(iii) Uandishi wa insha humfikirisha mwandishi. _____

(iv) Katika utangulizi, mwandishi wa insha huandika kwa kirefu kile anachotaka kukielezea. _____

(v) Insha zilizoandikwa vizuri huchukiza wasomaji. _____

(vi) Insha huandikwa bila kufuata mpangilio wa mawazo. _____

(vii) Mawazo katika insha huandikwa katika aya. _____

(viii) Kichwa cha insha huandikwa kwa maneno mengi. _____

For online use only

(ix) Katika kiini, mwandishi wa insha huelezea kwa undani jambo analoliandikia. _____

(x) Uandishi wa insha haumpi mwandishi uhuru wa kujieleza kwa maandishi. _____

E. Bainisha sehemu za insha kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye kisanduku.

A. kichwa cha insha B. kiini cha insha C. hitimisho D. utangulizi

(i) Michezo ni mambo yanayofanyika kwa ajili ya kujifurahisha na kujichangamsha. Kuna michezo ya aina mbalimbali kama vile mpira wa miguu, netiboli, rede, mdako, drafti, karata na dama.

(ii) Umuhimu wa michezo

(iii) Kwa hiyo, jamii kwa ujumla tunasisitizwa kushiriki katika michezo mbalimbali katika maisha yetu ya kila siku.

(iv) Michezo huimarisha afya ya mwili na akili. Pia, michezo hujenga ushirikiano, nidhamu, na kujitolea. Hivyo, hukuza ustawi wa kijamii. Vilevile, michezo inatusaidia kuwa na tabia nzuri ambayo ni muhimu kwa ustawi wa jamii yetu.

F. Panga aya (i) – (v) kwa kufuata mtiririko mzuri wa matukio ili kupata insha. Kichwa cha insha kiwe "Umuhimu wa elimu".

(i) Tunapojifunza darasani, tunapata fursa ya kupata maarifa muhimu kutoka kwa walimu wetu. Maarifa haya yanatufanya tuwe na uwezo wa kuifahamu dunia inayotuzunguka na namna ya kukabiliana na changamoto zinazojitokeza. Bila elimu, ni vigumu kufikia malengo yetu na kuishi maisha bora.

(ii) Kwa kumalizia, ni wazi kuwa elimu ni silaha kubwa inayotuwezesha kukabiliana na changamoto za maisha na kufikia malengo yetu. Hivyo, tunapaswa kufanya bidii ili tuweze kutumia elimu kwa manufaa yetu na ya jamii.

(iii) Elimu pia inatufundisha maadili mema kama vile kufanya kazi kwa bidii, kuwa na huruma na kuwaheshimu wengine. Kupitia elimu, tunajua

FOR online use only

umuhimu wa kufanya kazi kwa ushirikiano na kusaidiana na wengine, ili kufikia malengo yetu.

(iv) Elimu ni mfumo wa mafunzo yanayopatikana shuleni au maishani. Kwa hiyo, elimu ni msingi muhimu wa mafanikio katika maisha ya kila mtu. Kupitia elimu, tunaweza kujifunza mambo mengi ambayo yanatufanya kuwa watu bora na wenye ufanisi katika jamii.

(v) Kutokana na elimu, tunapata maadili ambayo hutujenga kuwa waadilifu na wazalendo kwa nchi yetu na hatimaye kutufanya tuwe na maisha bora na yenye mafanikio makubwa.

G. Tunga sentensi sahihi kumi kwa kutumia maneno yaliyomo kwenye jedwali lifuatalo:

Ndoo	kikubwa	kimeanguka	
Mti	kubwa	limeanguka	
Embe	kidogo	umeanguka	chini
Mimea	mkubwa	imeanguka	
Kitabu	mdogo	zimeanguka	
	mikubwa		
	ndogo		
	dogo		
	midogo		

H. Andika umoja au wingi wa sentensi zifuatazo:

(i) Insha imeandikwa vizuri.

(ii) Mti mkubwa umevunjika usiku wa kuamkia leo.

(iii) Upepo mkali umevuma mchana huu.

(iv) Kiti chote kimevunjika.

(v) Watoto wanapenda kunywa maziwa.

(vi) Mimea imestawi vizuri.

(vii) Daraja limevunjika baada ya mvua kubwa kunyesha.

For Online use only

(viii) Ukuta umebomoka kutokana na ufa.

(ix) Ungo umetengenezwa kwa rangi nzuri.

(x) Magurudumu ya baiskeli yamepinda baada ya kugongwa na bajaji.

Kazi ya kufanya

Kusanya insha mbili, kisha bainisha vipengele vyake.

Zoezi la 6: Utungaji

Andika insha yenye maneno yasiyopungua mia moja (100) na yasiyozidi mia moja na ishirini (120). Chagua kichwa cha insha utakachokipenda.

use only
For online

Sura ya Sita

Kuandika barua za kiofisi

Utangulizi

Katika sura hii, utajifunza jinsi ya kuandika barua za kiofisi kwa kufuata muundo sahihi. Pia, utaandika barua hizo kwa kuzingatia mtiririko wa vipengele vyake. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuwa mwandishi mzuri wa barua za kiofisi.



Fikiri

Mambo ya kuzingatia wakati wa kuandika wa barua ya kiofisi

Ufahamu

Soma habari hii, kisha jibu maswali yanayofuata.

Kabonza amuuguza mama yake

Kabonza anaishi na mama yake katika Kijiji cha Kashule. Anasoma Shule ya Msingi Tumaini iliyopo Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara.

Wakati wa likizo, Kabonza alimsaidia mama yake kufanya shughuli mbalimbali. Alimsaidia kazi za shambani pamoja na za nyumbani. Muda wa likizo ulipokaribia kuisha, mama yake ali**ugua** na kulazwa hospitalini. Kwa kuwa hali yake ilikuwa mbaya, aliwekwa chini ya uangalizi maalumu wa daktari.

Daktari alishauri awepo mtu wa kukaa na mgonjwa. Kabonza na mama yake waliishi peke yao. Hivyo, hakukuwa na mtu mwingine wa kukaa na mgonjwa. Kabonza alimwambia daktari kuwa yuko tayari kumwangalia mgonjwa. Kabonza alianza kumuuguza mama yake. Aliendelea kumuuguza mpaka mwisho wa likizo. Licha ya huduma nzuri aliyoipata, Mama Kabonza hakupata nafuu. Hivyo, Kabonza alitakiwa kuendelea kumuuguza. Kutokana na hali hiyo, aliamua kuomba ruhusa kwa mwalimu mkuu. Aliandika barua ifuatayo:

For online use only

Kijiji cha Kashule,
S.L.P. 60,
Masasi,
Mtwara.

08/07/2025.

Mwalimu Mkuu,
Shule ya Msingi Tumaini,
S.L.P. 60,
Masasi,
Mtwara.

Ndugu,

YAH: OMBI LA RUHUSA YA KUMUUGUZA MAMA

Tafadhali husika na kichwa cha habari hapo juu.

Mimi ni mwanafunzi wa Darasa la Tano. Mama yangu anaumwa na amelazwa hospitalini. Hivyo, ninaomba ruhusa ya kumuuguza kwa muda wa wiki mbili kuanzia tarehe 9 mpaka 22 Julai 2025.

Nitashukuru iwapo ombi langu litakubaliwa.

Wako mtiifu,

K. Digo

Kabonza Digo

Alipomaliza kuandika barua, aliituma kwa mwalimu mkuu, ambaye aliipokea na kuisoma. Baada ya kuisoma barua hiyo, mwalimu mkuu aliwaeleza walimu wenzake yaliyom**sibu** mwanafunzi wao.

Kesho yake, walimu walienda kumwona mama yake Kabonza hospitalini. Mama alifurahi alipowaona walimu wa mwanawe wamekuja kumwona. Aliwashukuru sana.

Baada ya wiki mbili kupita, mama yake Kabonza alipata **nafuu**. Aliruhusiwa na kurudi nyumbani. Kabonza naye alipata **mwanya** wa kwenda shule. Alipofika shuleni, alipokelewa vizuri na walimu. Walimu walimsaidia sana katika masomo yaliyompita. Pia, walimpongeza sana Kabonza kwa kuandika vizuri barua ya kuomba ruhusa kwa mwalimu mkuu.

For online use only

Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Kabonza ni mwanafunzi wa darasa la ngapi?
2. Shule ya Msingi Tumaini iko mkoa gani?
3. Kabonza anaishi na nani?
4. Kwa nini Kabonza alimwandikia mwalimu mkuu barua?
5. Barua aliyoandika Kabonza ilikuwa inahusu nini?
6. Kabonza aliomba ruhusa kuanzia tarehe ngapi hadi tarehe ngapi?
7. Kwa nini walimu walienda hospitalini kumwona mama yake Kabonza?
8. Ungekuwa wewe ni Kabonza ungefanya nini ili uweze kupata ruhusa?
9. Kwa nini walimu walimpongeza Kabonza?
10. Umejifunza nini kutokana na habari uliyoisoma?

Zoezi la pili: Msamiati

Tunga sentensi mbili kwa kila neno.

1. ugua
2. sibu
3. nafuu
4. mwanya

Zoezi la 3: Miundo

Tunga sentensi mbili kwa kila muundo.

1. ..... karibu na .....

Mfano: Mimi ninaishi karibu na shule.

2. ..... kuliko .....

Mfano: Sungura ni mjanja kuliko fisi.

3. ..... kama .....

Mfano: Wewe unacheka kama mama yangu.

4. ..... zaidi ya .....

Mfano: Twiga ni mnyama mrefu zaidi ya wanyama wote.

For online use only

Zoezi la 4: Mazoezi ya lugha

A. Andika KWELI au SI KWELI

(i) Barua ya kiofisi inatakiwa iwe na anwani nne. _____

(ii) Barua ya kiofisi sharti iwe na salamu. _____

(iii) Sio muhimu kuweka kichwa cha barua kwenye barua ya kiofisi. _____

(iv) Mwisho wa barua ya kiofisi ni jina la mwandishi. _____

(v) Kumbukumbu namba ni sehemu mojawapo katika barua ya kiofisi. _____

(vi) Haitakiwi kuweka saini kwenye barua rasmi. _____

B. Andika kinyume cha maneno yafuatayo:

(i) anika _____

(ii) tuma _____

(iii) ruhusu _____

(iv) nuka _____

(v) chukua _____

(vi) fupi _____

C. Panga vipengele vifuatavyo kwa kufuata muundo sahihi wa barua ya kiofisi.

(i) Doto Jumanne

(ii) Yah: Ombi la kushiriki katika mchezo wa kirafiki

(iii) Wako mtiifu,

(iv) 30/4/2025.

(v) Mwalimu Mkuu,
Shule ya Msingi Malugala,
S. L. P. 257,
Meatu.

(vi) Mimi ni mwanafunzi wa Darasa la Tano. Ninaomba kwenda kushiriki katika mchezo wa kirafiki katika Shule ya Msingi Malugala. Mchezo huo utafanyika tarehe 28/05/2025 kuanzia saa 3:00 asubuhi hadi saa 8:00 mchana, katika viwanja vya shule hiyo.

(vii) Shule ya Msingi Malugala, S.L.P. 257, Meatu.

For online use only

(viii) Ndugu,

(ix) Tafadhali husika na kichwa cha habari hapo juu.

(x) D. Jumanne

(xi) Nitashukuru kama ombi langu litakubaliwa.

D. Tumia vipengele vilivyomo kwenye kisanduku kujaza muundo wa barua ya kiofisi uliyopewa.

anwani ya mwandikiwa, jina kamili la mwandishi, anwani ya mwandishi, saini ya mwandishi, tarehe ya kuandika barua, mwanzo wa barua, salamu ya awali, mwisho wa barua, kiini cha barua, kichwa cha barua, salamu ya mwisho

(i)

(ii)

(iii)

(iv)

(v)

(vi)

(vii)

(viii)

(ix)

(x)

(xi)

For online use only

E. Kamilisha barua ya kiofisi ifuatayo kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi.

Shule ya Msingi Tumaini,
S.L.P. 60,
(i) ……..
Mtwara.
8/7/2025.

Kumb. Na. KJK/2025/04

Kabonza Digo,
Kijiji cha Kashule,
(ii)……..
Masasi,
Mtwara.

(iii)……..

YAH: RUHUSA YA KUMUUGUZA MAMA YAKO

Kichwa cha habari chahusika

Rejea barua yako ya tarehe 08 Julai 2025 inayohusu ruhusa ya kumuuguza mama yako kwa muda wa siku 14 kuanzia tarehe 9 hadi 22 Julai 2025. Hivyo, kama ulivyoomba, ninakuruhusu ukamuuguze mama yako na baada ya siku hizo ulizoomba, urudi shuleni kuendelea na masomo.

Uongozi wa shule unakupa pole sana na unakutakia kila la heri.

(iv)……..

O. Kunega

Ongano Kunega

(v) ……..

For online use only

F. Andika maneno yenye maana sawa na maneno uliyopewa.

Mfano: motokaa - *gari*

majani – *nyasi*

(i) barua _____

(ii) hiari _____

(iii) ahueni _____

(iv) andika _____

(v) mja _____

(vi) tabibu _____

(vii) kikao _____

(viii) madhumuni _____

(ix) saini _____

(x) ugonjwa _____

G. Maneno yafuatayo yana maana zaidi ya moja. Andika maana mbili kwa kila neno.

Mfano: funga – sogeza mlango kuziba uwazi

– pata bao katika mchezo au mashindano

poa – hali ya kuwa baridi, neno la kusema mambo

– yako sawa au vizuri (lugha ya mazungumzo)

(i) shinda

(ii) vua

(iii) mlango

(iv) fua

(v) tanga

(vi) kiboko

(vii) nahodha

(viii) pita

(ix) mguu

(x) mtihani

For Online use only

H. Jaza fumbo lifuatalo kwa kufuata maelekezo ya kwenda chini na kwenda kulia.



Kwenda chini

2 Kifaa kinachotumika kuandikia (4)

3 Kitendo cha kugusanisha viganja vya mikono kushangilia jambo (6)

6 Kusimama au kunyooka kwenda juu, simama sawasawa bila ya kupinda (4)

8. Lengo, nia, au kusudi la kufanya jambo fulani (7)

Kwenda kulia

1. Anwani ya mtu inavyoandikwa kwenye barua kwa kifupi (3)
3. Jambo au kitu kinapoanzia (6)
4. Hitimisho (6)
5. Maelekezo ya mahali ambapo mtu huishi au kufanyakazi, sanduku analotumia mtu kutuma na kupokea barua kwa njia ya posta. Pia, akaunti ya mtandao wa kutuma na kupokea barua kupitia mfumo wa intaneti (6)
7. Toa kitu kilichokuwa kimefukiwa na udongo ardhini (5)
9. Mtunzi wa kitabu, au waraka (9)

For online use only

Kazi ya kufanya

Kusanya barua tano za kiofisi, kisha onesha tofauti iliyopo kati ya barua hizo.

Zoezi la 5: Utungaji

Andika barua ya kiofisi kwa mwalimu wa darasa ukiomba msamaha kwa kosa la kufanya fujo darasani. Anwani yako iwe Shule ya Msingi Bombambili, S.L.P. 335, Songea.

For online use only

Sura ya Saba

Kusikiliza na kusimulia hadithi

Utangulizi

Katika sura hii, utasikiliza na kusimulia hadithi. Pia, utajifunza mitindo mbalimbali ya usimuliaji wa hadithi. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kusimulia hadithi mbalimbali kwa mitindo tofautitofauti.



Fikiri

Mitindo ya kusimulia hadithi

Ufahamu

Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.

Kisa cha wanyama kuishi na binadamu

Msimuliaji: Paukwa…

Wasikilizaji: Pakawa…

Msimuliaji: Ngoja nikueleze kilichotokea mahali ambapo hata upepo ulikuwa ukizungumza. Hapo zamani za kale, wanyama wooote waliishi porini. Walikuwa wakishirikiana kutafuta chakula. Simba alikuwa anashirikiana na ng'ombe, mbuzi, kondoo, mbwa, paka na punda. Walikuwa marafiki wa karibu sana. Waliishi kama ndugu wa kuzaliwa.

Walikubaliana kutafuta chakula kwa zamu, huku wengine wakibaki nyumbani kuwahudumia watoto wao. Chakula kilikuwa kinapatikana kwa shida sana. Ilifika zamu ya simba kwenda kutafuta chakula. Aliwaaga wenzake na kuondoka kwenda porini. Huku nyuma, ng'ombe aliwashawishi wenzake kwa kusema, "Jamani, ninaona maisha ya huku porini yanazidi kuwa magumu siku hadi siku. Tuondokeni twende tukaishi kwa binadamu." Mbwa akauliza, "Hawa watoto wa simba tutawafanyaje?" Ng'ombe akajibu, "Tuwatoroke."

Wote walikubali. Ng'ombe akawaambia, "Mkisikia sauti yangu moo... moo... moo..., kila mmoja akimbie na watoto wake." Watoto wa simba watakuwa wamelala. Baada ya muda mfupi, ng'ombe alifanya hivyo, na wanyama wote wakakimbia. Simba aliporudi kutoka mawindoni, hakuwakuta wenzake. Akashituka alipowaona wanawe wamebaki peke yao. Akapiga ukelele wa majonzi "Mamaaa! Uuuwi! Watoto wangu watacheza na nani?" Alitazama huku na kule lakini hakuona rafiki yake hata mmoja. Alilia sana kwa uchungu. Aliendelea kuwatafuta lakini

For online use only

hakufanikiwa kuwaona.

Ng'ombe na wenzake, wakiwa njiani kuelekea kwa binadamu, walianza kuzungumza. Paka alisema, "Tutafanya nini ili binadamu aweze kutukaribisha nyumbani kwake?" Punda akasema, "Kila mmoja aeleze atamsaidia nini binadamu." Ng'ombe akasema, "Mimi nitamwambia binadamu kwamba nitampatia maziwa na **siagi**. Pia, nitamsaidia kulima mashamba na kumpatia **samadi**."

Punda akasema, "Mimi nitamsaidia kubeba mizigo na kulima mashamba kwa jembe la ku**kokota**."

Mbwa akasema, "Mimi nitamlindia nyumba mchana na usiku." Pia, nitalinda mashamba yake dhidi ya wanyama waharibifu. Nitakula chakula kidogo anachokula yeye."

Paka akasema, "Mimi nitamwambia binadamu kwamba nitalinda mazao yake dhidi ya panya wanaoharibu mazao. Nitalala kwenye ghala la kuhifadhia mazao. Nitakula baadhi ya vyakula anavyokula yeye."

Kondoo na mbuzi wao walisema, "Sisi tutamwambia binadamu kwamba tutampatia maziwa. Chakula chetu ni majani. Atatujengea **zizi** moja."

Baada ya mazungumzo hayo, usiku uliingia. Walikuwa wamechoka; wakalala **pango**ni. Alfajiri waliendelea na safari yao ya kwenda kwa binadamu. Binadamu alipowaona, alishituka na kuogopa. Akasema, "Ondokeni! Ondokeni ninyi wanyama." Wanyama wakambembeleza wakiomba awasikilize kwanza.



For Online Use Only

Aliendelea kwa kuwauliza “Mnataka niwasaidie nini?” Ng’ombe akajibu, “Sisi tunaomba tuishi na wewe. Tumechoka maisha ya porini. Unavyotuona hapa, tunahitaji msaada wako.” Aliuliza tena, “Mtanisaidia nini endapo mtaishi na mimi?” Walijieleza kama walivyojadiliana wakiwa njiani.

Baada ya kusikia maelezo ya kila mnyama, akawauliza tena, “Je, hamtanidhuru?” Wakajibu, “Hapana! Hatutakudhuru. Tutakuwa watiifu siku zote.” Binadamu akawakubalia. Akasema, “Nimesikia maelezo ya kila mmoja wenu. Hivyo, kuanzia sasa, tutaishi pamoja. Kila mnyama atekeleze kile alichoahidi kukifanya bila manung’uniko.” Wote walifurahi kuanza kuishi na binadamu. Mpaka sasa, wanyama hao wanaishi na binadamu. Walikubaliana wasiwe wanaongea kabisa ila wawe wanatoa mlio wanapokuwa na tatizo.

Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Simba aliishi na wanyama gani?
2. Nani aliyewashawishi wenzake kwenda kuishi kwa binadamu?
3. Kwa nini wanyama waliamua kwenda kuishi na binadamu?
4. Wakati wanyama wanatoroka, watoto wa simba walikuwa wanafanya nini?
5. Kipengele gani kimekuvutia zaidi katika hadithi hii?
6. Punda aliahidi kumsaidia binadamu kubeba mizigo. Katika mazingira unayoishi ni vifaa gani hutumika kubeba mizigo?
7. Unadhani kondoo anaweza kumpa binadamu nini zaidi ya maziwa?
8. Kama wewe ungepata nafasi ya kuongea na wanyama hawa walioenda kwa binadamu, ungewapa masharti gani?
9. Kati ya wanyama na binadamu, unadhani nani alifanya maamuzi sahihi? Kwa nini?
10. Umejifunza nini kutokana na hadithi hii?

Zoezi la pili: Msamiati

Tunga sentensi mbili kwa kila neno.

1. siagi
2. samadi
3. kokota
4. zizi
5. pango

For online use only

Zoezi la 3: Nahau na misemo

Oanisha nahau na misemo ya Sehemu A na maana zake kutoka Sehemu B.

Sehemu A	Sehemu B
1. shika maneno	(a) jitahidi kwa kila njia
2. shika ulimi	(b) kwa pamoja
3. uma sikio	(c) kata uhusiano
4. fanya juu chini	(d) angalia kwa makini
5. vunja urafiki	(e) fundishwa nidhamu
6. zaa matunda	(f) pata faida
7. shika adabu	(g) nyamaza
8. kaza macho	(h) nong'oneza
9. bega kwa bega	(i) tia maanani; zingatia
10. pigwa butwaa	(j) maliza kazi
	(k) ruhusu watu waende
	(l) shangaa

Zoezi la 4: Methali

Kamilisha methali zifuatazo:

1. Mshika mbili …….
2. ..... harabu ya nzima.
3. Mwenza mbili …….
4. ..... halisikii dawa.
5. Sikio halilali …….
6. ....., ungali maji.
7. Kichwa ni .....
8. Bora lawama, …….
9. Fimbo ya mbali …….
10. ..... huvutia kwake.

For online use only

Zoezi la 5: Mazoezi ya lugha

A. Badili sentensi zifuatazo kuwa katika wakati uliopita.

(i) Ngoma zinafikisha ujumbe kwa jamii.

(ii) Doto atashiriki maonesho ya sikukuu ya wakulima.

(iii) Mwalimu anampongeza mwanafunzi kwa kufaulu masomo yake.

(iv) Wanafunzi wanatembelea mbuga za wanyama.

(v) Mama anaenda kazini.

(vi) Safari imeanza; tumefurahi sana.

(vii) Mkuu wa shule atatoa shukurani kwa mgeni rasmi.

(viii) Wanaimba nyimbo za shangwe.

(ix) Shule yetu imeshika nafasi ya kwanza katika masomo yote.

(x) Shangazi atanileta zawadi.

B. Tunga sentensi kumi kutokana na jedwali lifuatalo:

Pale	kijijini nyumbani shuleni mtaani sokoni	palikuwa na	duka kubwa mti mkubwa visima vya maji wanyama wa kufugwa watoto wengi

C. Andika umoja na wingi wa maneno yafuatayo:

Mfano: chuma – *vyuma*

mnyama – *wanyama*

	Umoja	**Wingi**
(i)	_____	mizimu
(ii)	_____	masega
(iii)	kidari	_____

For online use only

(iv) maji _____

(v) _____ michezo

(vi) mtemi _____

(vii) mwanafunzi _____

(viii) paka _____

(ix) mto _____

(x) _____ vituo

D. Herufi katika maneno yafuatayo zimechanganywa. Zipange ili zilete maneno sahihi.

Mfano: ngede – *ndege*

wamb – *mbwa*

(i) kaap

(ii) mbeto

(iii) mbagu

(iv) wigat

(v) neon

(vi) rigin

(vii) ukis

(viii) moot

(ix) tabuki

(x) mubiz

(xi) panud

E. Chagua neno lisilohusiana na mengine.

(i) cheza, kimbia, kula, simama, upesi _____

(ii) bata, kipepeo, njiwa, kuku, kanga _____

(iii) mtoto, kifaranga, kinda, ndama, mimba _____

(iv) kisu, mwiko, msumari, sindano, wembe _____

(v) shuka, shati, kanzu, gauni, fulana _____

(vi) chai, sukari, chumvi, siagi, mkate _____

(vii) karanga, korosho, maharage, alizeti, ufuta _____

(viii) mbao, misumari, bati, sementi, nyundo _____

(ix) televisheni, redio, simu, daftari, kompyuta _____

(x) polisi, mbwa, askari, mgambo, mwanajeshi _____

For online use only

Kazi ya kufanya

Sikiliza hadithi tatu kutoka vyanzo mbalimbali, kisha chora picha za wahusika wakuu wa hadithi hizo. Tumia picha hizo kusimulia hadithi hizo.

Zoezi la 6: Utungaji

Tunga hadithi yenye maneno miamoja (100) hadi miamoja na hamsini (150) kwa kuzingatia mianzo ya kusisimua kama vile:

(i) Hii si hadithi ya kawaida, ni ya kustaajabisha.

(ii) Na sasa hadithi inakuwa taaamu zaidi, sikiliza.

Kisha, simulia hadithi uliyoitunga.

For online use only

Sura ya Nane

Kutafsiri ujumbe wa hadithi

Utangulizi

Katika sura hii, utajifunza kutafsiri ujumbe mkuu uliomo katika hadithi. Utasoma hadithi kwa makini na kueleza ujumbe mkuu uliomo. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kutafsiri kwa usahihi ujumbe uliomo kwenye matini mbalimbali.



Fikiri

Hadithi uliyoisoma ambayo hutaisahau

Ufahamu

Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.

Umuhimu wa familia

Hapo zamani za kale, palikuwepo na familia moja yenye upendo. Watu wa familia hiyo waliishi kwa furaha na kushirikiana kwa kila jambo. Katika familia hiyo, alikuwepo babu mwenye umri wa miaka mia moja. Babu huyo aliitwa Mzee Mwendapole. Mzee Mwendapole aliwasisitiza wanafamilia kudumisha upendo na kufanya kazi kwa bidii ili kuwa na kipato cha kutosha. Wanafamilia walipokea ushauri na kuufanyia kazi.

Kuanzia asubuhi hadi mchana, walifanya kazi pamoja; jioni waliketi **upenuni** na kula pamoja. Baada ya chakula, kila mmoja alitoa burudani na kituko chake. Mzee Mwendapole ndiye aliyewavutia zaidi kwa **michapo** yake ya kusisimua na kufurahisha.

Katika familia hiyo, walikuwepo watoto wawili pacha, Kulwa na Doto. Kulwa alipenda kufanya kazi na kushirikiana na wenzake. Doto alipenda kujitenga na kufanya mambo mengi peke yake. Alipiga chenga masuala yote yaliyohusu umoja. Babu yake alimshauri kushirikiana na familia kwani, ushirikiano katika familia ni muhimu sana. Alisema, “Hakuna binadamu anayeweza kufanikiwa kwa kuishi peke yake.” Hata hivyo, Doto alimpuuza.

For online use only

Alipofika umri wa ujana, nduguze walizidi kumshauri ashirikiane na wenzake, lakini Doto alikasirika. Akaamua kwenda kuishi porini. Aliondoka nyumbani kwa **makeke**. Huko porini, alitembea kwa mwendo wa kibabe na kwa hatua **madhubuti**.

Alichagua eneo zuri, akaandaa makazi na kulima shamba kubwa. Alilima kwa nguvu huku akijisifu, “Mimi ni nyati, shujaa, sishindwi kitu na sihitaji msaada. Siku zote shujaa husimama peke yake.”

Miezi mitatu baadaye, mazao aliyolima yakastawi vizuri sana. Alipanda juu ya mti mrefu na kutazama mazao kwenye shamba lake. Yalikuwa mengi na yalistawi vizuri sana. Alitabasamu huku akikuna kidevu kwa jeuri. Akanyoosha mkono na kusema, “Nilisema mimi sishindwi kitu, tazama mali ya shujaa. Nitakula nishibe miaka mingi kwa kadiri nitakavyo. Mungu anipe nini?”

Majuma mawili kabla hajaanza kuvuna, Doto alipatwa na homa kali. Akajitahidi kukaza roho na kutafuna mizizi ili kujitibu, lakini homa haikumwacha. Ali**dhoofika**, akakosa nguvu. Mara, akayaona makundi ya ndege, ngedere na nyani wakila na kuharibu mazao yake. Walikula kwa furaha kama wanafanya sherehe. Wali**kwanyua** mahindi na kung’oa mimea aina kwa aina. Wakairusha huku na kule. Doto alitamani ku**amia** lakini mwili wake ulikuwa **taabani**. Hakuweza hata kuinua mkono. Akabaki akiwatazama tu huku machozi yakim**churuzika**. Vitendo vya makundi hayo ya wanyama vilimkata maini.

Aliikumbuka familia yake: akajisemea, “Sasa nimetambua umuhimu wa familia. Ningekuwa na familia yangu, haya yote yasingenitokea. Leo nimeamini maneno ya babu. Ama kweli umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.”

Siku mbili baadaye, alipata nguvu kidogo akafungasha virago na kurejea nyumbani kwa unyonge. **Mwondoko** alioondoka nao nyumbani si ule aliorudi nao. Sasa alikuwa ameweka mikono yake nyuma. Safari hii, hakutembea kwa makeke, bali alitembea kwa unyonge kutokana na afya yake kuwa dhaifu.

Alipokelewa na mdogo wake aliyekuwa akitoka shambani kuamia ndege na kulinda shamba dhidi ya wanyama walao mazao. Walipokaribia nyumbani, alimwona dada yake akiwa na jembe begani na panga mkononi akitoka shambani. Hapo nyumbani, alimkuta baba yake akiwa anamkamua ng’ombe maziwa, na mama yake akiwa anapika chakula jikoni. Binamu yake, ambaye alikuwa bustanini akimwagilia mboga, alipomwona, alipiga mbio akamkumbatia Doto kwa furaha.

For online use only



Watu wote hapo nyumbani walimpokea ndugu yao kwa furaha na moyo mkunjufu. Mara, Kulwa alifika. Alikuwa ametoka hospitalini kumpeleka babu kupata matibabu. Kulwa alifurahi kumwona ndugu yake. Alimkaribisha kwa kusema, “Karibu ndugu yangu!” Babu naye akamkaribisha kwa kusema, “Karibu mjukuu wangu! Hii ndiyo familia yako.” Doto alijibu, “Asante babu.” Aliomba msamaha huku akibubujikwa na machozi na kusema, “Nimeamini hakuna anayeweza kusimama peke yake. Familia ni muhimu sana; iwe kubwa ama ndogo.” Kesho yake, walimpeleka Doto hospitali akatibiwa. Doto akarejea katika afya yake njema na akawa mwenye furaha isiyo na kifani.

Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Pendekeza kichwa cha hadithi hii?
2. Kulwa na Doto walikuwa na tofauti gani za kitabia?
3. Kwa nini Doto aliamua kwenda kuishi porini peke yake?
4. Doto alipougua, alikumbuka jambo gani?
5. Ukilinganisha maisha ya Kulwa na Doto, ni nani alifanya maamuzi bora? Eleza kwa nini.
6. Unadhani Doto alijifunza nini baada ya kuishi peke yake porini?

For online use only

7. Kwa mtazamo wako, unadhani Doto alifanya uamuzi sahihi kurudi nyumbani? Eleza sababu zako.
8. Unadhani familia ina nafasi gani katika maisha ya kila mtu? Eleza kwa mifano.
9. Katika maisha halisi, umewahi kusikia mtu aliyejitenga na familia yake kama Doto? Mwishowe ilikuwaje?
10. Ujumbe gani unaoupata kutokana na hadithi hii?

Zoezi la pili: Msamiati

Eleza maana ya maneno yafuatayo:

1. upenuni
2. michapo
3. makeke
4. madhubuti
5. dhoofika
6. kwanyua
7. amia
8. taabani
9. churuzika
10. mwondoko

Zoezi la 3: Nahau na misemo

Eleza maana ya nahau na misemo ifuatayo:

1. fungasha virago .....
2. kaza roho .....
3. moyo mkunjufu .....
4. kata maini .....
5. piga chenga .....
6. kufumba na kufumbua .....
7. tangu na tangu .....
8. tazama kijuujuu .....

Zoezi la 4: Mazoezi ya lugha

A. Andika kinyume cha maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo:

(i) Doto ali<u>rejea</u> nyumbani akiwa ameweka mikono mbele.

(ii) Nenda nyumbani ukashirikiane na ndugu <u>zako</u>.

FOR online use only

(iii) Doto alirudi nyumbani kwa kuchangamka.

(iv) Binamu alitembea taratibu kumpokea ndugu yake.

(v) Doto alipokuwa porini alipata raha.

(vi) Hii ndiyo familia yako.

(vii) Babu hutusimulia hadithi wakati wa usiku.

(viii) Kulwa alikubali pongezi.

(ix) Shangazi alipata fursa ya kuzungumza na familia.

(x) Alisimama karibu na moto.

B. Badili sentensi zifuatazo kuwa katika wakati uliopita.

(i) Hadithi hiyo itatusaidia kujua umuhimu wa familia.

(ii) Kulwa amepokelewa vizuri na pacha wake.

(iii) Babu anayumbayumba kwa kudhoofu.

(iv) Nimekuwa nikila na kushiba kwa miaka mingi.

(v) Doto ameandaa makazi yake porini.

(vi) Sote tutapanda mlima hadi kileleni.

(vii) Familia itampokea ndugu yao kwa furaha.

(viii) Siku mbili baadaye, atapata nguvu.

(ix) Watu wote tumekumbuka familia zetu.

(x) Binamu yake atakuwa bustanini.

C. Andika sentensi zifuatazo katika wingi.

(i) Ndugu yake alimshauri ashirikiane na mwenzake.

(ii) Mtu huyu ametambua umuhimu wa kufanya kazi.

(iii) Alikuwa ameweka mkono wake nyuma.

(iv) Ngedere alikwanyua hindi.

(v) Shati lake limechanika.

(vi) Panya alijificha uvunguni mwa kitanda.

(vii) Simu ya mkononi ya mama yetu imeibwa.

For online use only

(viii) Ugonjwa huu umeenea katika kata yote.

(ix) Mwalimu anaandika ubaoni.

(x) Huyu kijana ana adabu sana.

D. Kanusha sentensi zifuatazo:

(i) Mjomba alienda kisimani kuchota maji.

(ii) Shangazi anafinyanga vyungu vizuri.

(iii) Binamu alichinja beberu mkubwa.

(iv) Baba mdogo amemnyoa nywele mdogo wangu.

(v) Bibi anasuka kikapu chenye rangi mbalimbali.

(vi) Dereva wa basi hili anaendesha taratibu.

(vii) Msua ni mfinyanzi mzuri wa vyungu.

(viii) Mtoto atalilia chakula.

(ix) Wachuuzi wameongezeka sana.

(x) Shani amefaulu mitihani yake vizuri.

E. Andika sentensi zifuatazo kwa usahihi.

(i) Mimi ninakwendaga shule kila siku.

(ii) Mwalimu Kagete analifundisha Shule ya Msingi Lumwani.

(iii) Chaku analioshapo banda la kuku.

(iv) Baba yake Sima huzilima mpunga na mahindi.

(v) Kazi huwasaidiana wanafamilia kuinua kipato.

(vi) Alitaka amkutage amefika stendi.

(vii) Baba yangu alikuja hasubuhi.

(viii) Pendo ametumbukia ndani mwa shimo.

(ix) Mahali apa ni pazuri.

(x) Nzee Barua alikuwa odari wa kuimba.

For online use only

F. Andika neno lingine lenye maana sawa na maneno yafuatayo:

(i) sala
(ii) hadithi
(iii) wakati
(iv) maana
(v) waza
(vi) mashine
(vii) kaidi
(viii) uso
(ix) salamu
(x) sherehe

G. Chagua neno kwenye kisanduku ili kukamilisha sentensi.

alitozwa	turubai	taji	taabani	kuwapongeza
radi	maktabani	kifani	dhahiri	pancha
ilifana	dharura	aya	tumeazimia	shada

(i) Tuliandaa sherehe ya _____ wanafunzi waliofaulu mitihani.
(ii) Mwaka huu _____ kupanua shamba letu la maharage.
(iii) Malkia alivaa _____ lililotengenezwa kwa dhahabu.
(iv) Nenda _____ ukasome vitabu.
(v) Wakati wa mvua, _____ ilipiga na kuangusha miti.
(vi) Magunia ya mahindi yalifunikwa kwa_____ili yasinyeshewe na mvua.
(vii) Dereva_____ faini kwa kuendesha gari kwa mwendokasi.
(viii) Aliziba _____ zote kwenye tairi la mbele.
(ix) Sherehe yao _____ sana.
(x) Mama alitutafsiria _____ya kwanza.

H. Andika maana mbili kwa kila neno.

(i) toa
(ii) panga
(iii) ujumbe
(iv) kichwa
(v) kibao
(vi) kucha
(vii) ngano
(viii) funga
(ix) ganda
(x) chana

For online use only

Kazi ya kufanya

Soma hadithi mbili kutoka katika maktaba, kisha eleza ujumbe uliomo na unavyohusiana na maisha halisi ya jamii yako.

Zoezi la 5: Utungaji

Andika hadithi fupi unayoipenda yenye maneno kati ya mia moja hamsini na mia mbili (150 - 200), kisha eleza mafunzo ya hadithi hiyo.

For online use only

Sura ya Tisa

Uhusika katika hadithi

Utangulizi

Katika sura hii, utajifunza kuhusianisha mienendo ya wahusika waliomo katika hadithi na maisha halisi. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuelewa mienendo na tabia za watu halisi katika jamii. Pia, utakuwezesha kuwa mtunzi mzuri wa hadithi na kazi nyingine za sanaa ya lugha kwa kuwaumba wahusika kulingana na tabia na mienendo ya watu halisi katika jamii.



Fikiri

Kazi ya wahusika katika hadithi

Ufahamu

Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.

Mkutano wa wanyama

Hapo zamani za kale, wanyama wote waliishi pamoja porini. Walishirikiana katika kazi mbalimbali. Mfalme wao alikuwa Tembo. Walimpenda sana kutokana na busara zake. Kwa muda mrefu, waliishi kwa ku**tangatanga** na kupata chakula kwa taabu. Mfalme wao alifikiria sana kuhusu kutatua tatizo hilo. Alipata wazo kuwa awaite wanyama wote kujadili namna ya kulitatua. Alimwita Simba na kumwagiza, “Nenda ukawaalike wanyama wote kwa ajili ya mkutano wa kesho.”

Simba alijibu, “Nitatekeleza mfalme wetu.” Simba aliondoka na kunguruma gruum! Gruum! Gruum …! Kisha, akasema kwa sauti nene, “Tangazo maalumu! Kesho, sote tunatakiwa kufika kwa mfalme wetu Tembo. Tutajadili namna ya kupata chakula. Asikose mnyama hata mmoja, gruum... gruum... gruuum...!” Wanyama wote walipata taarifa hiyo. Kesho yake, walikutana kwa mfalme. Walikuwepo Simba, Fisi, Nyani, Ngedere, Swala, Nyati, Kifaru, Kiboko, Chui na wanyama wengine.

Mkutano ukaanza. Mfalme akasema, “Ndugu zangu, mnaona tunavyopata shida ya chakula?” Wanyama wote wakaitikia, “Ndiyooo!” Mfalme akaendelea, “Sasa nimewaita ili tujadili tatizo hili.” Mjadala ulianza. Kila mnyama alitoa wazo lake.

use only
Online
FOR

Nguchiro alisema, “Tushikamane kwa umoja wetu; tulime shamba la pamoja. Mvua ikinyesha, tupande mazao. Tutatumia samadi ili mazao yetu yastawi vizuri. Tutavuna na kuyahifadhi katika ghala.” Wanyama wote walikubaliana na wazo hilo.



Mfalme akasema, “Ninawashukuru sana kwa kutambua tatizo letu na kulipatia ufumbuzi. Ardhi yetu ina **rutuba** ya kutosha. Wahenga wetu walinena kwamba umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu. Kwa hiyo, kila mmoja wetu aandae jembe, shoka na panga ili kesho tuanze kulima.” Siku ilipofika, wanyama wote walifika shambani. Mfalme akamwambia Twiga, “Kwa kuwa wewe ni mrefu kuliko wanyama wote, angalia ni mnyama yupi hakufika na utoe taarifa.” Twiga aliangalia huku na huko na kugundua kuwa Kiboko hakufika. Akaamtaarifu mfalme, "Mfalme! kiboko hayupo." Wakati mkutano ukiendelea, mfalme aliendelea kuwaza ni namna gani atahakikisha Kiboko anashiriki shughuli za maendeleo kama wenzake.

Wanyama walifanikiwa kulima shamba kubwa. Mvua iliponyesha, walipanda mazao mbalimbali. Walipomaliza kupanda, mfalme Tembo akasema, “Kwa kuwa Kiboko hakushiriki kabisa, tutamfukuza maana hana ushirikiano na sisi. Tuweke zamu za kulinda shamba letu.” Wakakubaliana na mawazo ya mfalme. Siku ya kwanza, Simba alianza kulinda; akasema, “Akija Kiboko, nitamfinyanga**finyanga**.” Wanyama wakacheka hahaha! Wanyama wengine wakaondoka. Punde si punde Kiboko alifika akamsalimia Simba, “Habari ya leo ndugu?” Simba alikaa kimya. Kiboko akasema, “Nywele zako zimekaa **shaghalabaghala;** ninaomba nikusuke.

FOR online only

Mimi ni **msusi** mzuri. Wanyama wote watakupenda na utachaguliwa kuwa mfalme baada ya Tembo ku**staafu**.'' Simba alifurahi kusikia atapendeza na kurithi ufalme.

Kiboko akamwambia, "Twende pale juu ya mti nianze kukusuka." Walienda juu ya mti. Akaanza kumsuka huku akifunga manyoya yake kwenye mti. Alipomaliza kumfunga, akamwambia, "Sasa naenda kula mazao na kuyaharibu." Kiboko akashuka chini; Simba akabaki ana**ning'inia** juu ya mti. Alipiga yowe wanyama wenzake wakakimbia kuja kumsaidia. Walimkuta Simba ananing'inia juu ya mti. Wakamsaidia kumtoa. Aliwasimulia kisa chote.

Siku iliyofuata, wanyama walitawanyika kuzunguka shamba zima wakimsubiri Kiboko. Walijificha katika majani wakiwa na silaha. Siku hiyo, Kiboko hakutokea. Hawakukata tamaa. Waliendelea kulinda mazao yao siku hadi siku.

Baada ya siku kadhaa kupita, Kiboko alienda tena katika shamba la wanyama. Alifika shambani na kuangalia huku na huko, lakini hakuona kitu. Wakati huo, wanyama walikuwa wamejificha wakimsubiria Kiboko aingie shambani ndipo wamkamate. Aliingia shambani; ghafla, wanyama wakatokea pande zote wakiwa na silaha.

Kiboko aliangalia namna ya kuwatoroka lakini alishindwa kwa sababu wanyama walimzingira. Walimkamata na kumpeleka kwa Mfalme Tembo. Mfalme akasema, "Ndugu yangu, siku za mwizi ni arobaini. Adhabu yako ni kuondoka huku nchi kavu ukaishi majini kuanzia sasa. Ninaamuru jeshi langu likupeleke ziwani au mtoni, ukaishi huko siku zote za maisha yako." Hadi leo Kiboko anaishi majini na hutoka nje wakati wa usiku kutafuta chakula. Mchana anaogopa kutoka nje kwa hofu ya kukamatwa na wanyama.

Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Nani alikuwa mfalme wa wanyama?
2. Mfalme alimwita nani kutoa tangazo la mkutano?
3. Orodhesha wahusika wote kwenye hadithi uliyoisoma, kisha taja sifa za wahusika hao.
4. Unafikiri kwa nini Kiboko hakufika kwenye mkutano?
5. Eleza hatari tatu ambazo Kiboko angeweza kuzipata akiwa juu ya mti.
6. Wanyama walilima mazao ya aina gani?
7. Wewe ungependa kuwa nani katika hadithi hii. Toa sababu.
8. Eleza sababu ya Simba kuning'inizwa juu ya mti.
9. Kama ungekuwa Mfalme Tembo ungefanya maamuzi gani kuhusu Kiboko?
10. Hadithi hii inakufundisha nini?

FOR online use only

Zoezi la pili: Msamiati

Tunga sentensi mbili kwa kila neno.

1. tangatanga
2. rutuba
3. finyanga
4. shaghalabaghala
5. msusi
6. staafu
7. ning'inia

Zoezi la 3: Methali

Kamilisha methali zifuatazo:

1. Ndege mjanja .....
2. Tamaa mbele, ...
3. ..... hajikwai.
4. ..... yavuta heri.
5. Mwana wa kuku .....
6. Si vyote ving'aavyo .....
7. ..... halikuli likakwisha.
8. .... si mkulima.
9. Polepole ya kobe .....
10. ..... halina ubani.

Zoezi la 4: Vitendawili

Tegua vitendawili vifuatavyo:

1. Daima hunifuata nyuma, nikimfuata hunikimbia. .....
2. Anaoga sana lakini hatakati. .....
3. Mwanangu akichanganyika na wenzake simtambui. .....
4. Huna macho lakini unakamata wanyama. .....
5. Kila ukiwakuta wamejiandaa kupigana. .....
6. Kisima cha mfalme hakikauki. .....
7. Maji ya kisima changu hayanyweki. .....

For online use only

8. Watoto wa Mungu hawahesabiki. ……..

9. Kala tumbo limejaa; hakula tumbo limejaa. ……..

Zoezi la 5: Nahau na misemo

Toa maana za nahau na misemo ifuatayo:

Mfano: mtu wa juzi – *mtu mchanga asiyekuwa na uzoefu*

mtu hariri – *mtu mpole*

1. mtu hufa na ulimi wake
2. ana ndimi mbili
3. mwana wa mifupani
4. mguu niponye
5. mjinga wa wajinga
6. mtu wa makamo
7. mtu mkubwa
8. mtu mwanana
9. mtu nyoka
10. mtu wa amali

Zoezi la 6: Mazoezi ya lugha

A. Andika kinyume cha maneno yafuatayo:

(i) kizuri _____

(ii) weza _____

(iii) ng'aa _____

(iv) fukua _____

(v) zomea _____

(vi) tandika _____

(vii) uza _____

(viii) fuma _____

(ix) ongea _____

(x) shika _____

For online use only

B. Pigia mstari neno ambalo ni tofauti na mengine.

Mfano: mbu, <u>mbuzi,</u> mbung'o, nzi, kunguni

choroko, kunde, <u>miwa</u>, maharage, njegere

(i) ng'ombe, nyani, chui, njiwa, kondoo

(ii) ukucha, kidole, mkono, kiwiko, uso

(iii) bata, mbuni, popo, chiriku, kunguru

(iv) rede, dama, ukuti, karata, kete

(v) shati, blanketi, kofia, suruali, kaptura

(vi) wali, ugali, chai, pilau, kande

(vii) parachichi, nanasi, juisi, embe, papai

(viii) kambare, kaa, perege, sangara, kibua

C. Andika maneno kumi yanayokaribiana kimatamshi lakini yana maana tofauti.

Mfano: *ndoa, doa*

baba, papa

D. Andika majina kumi kutoka katika jedwali lifuatalo:

CH	F	T	R	M	V	U	V	I	H	M	D
B	L	W	O	F	N	G	U	CH	I	R	O
D	A	K	T	A	R	I	F	S	Z	U	A
E	Z	I	A	L	F	I	K	A	M	E	A
R	O	O	I	M	W	A	L	I	M	U	A
E	A	N	T	E	O	S	K	W	H	R	A
V	H	G	W	P	O	A	R	T	A	A	Z
A	W	O	I	I	H	L	U	N	S	A	A
A	P	Z	G	T	S	I	O	J	I	K	CH
F	I	I	A	A	F	S	B	A	B	U	I
Y	K	M	U	U	G	U	Z	I	U	K	A
P	U	N	D	A	M	I	L	I	A	U	V

For online use only

Kazi ya kufanya

Chunguza tabia na mienendo ya watu katika jamii yako, kisha zilinganishe na tabia na mienendo ya Nguchiro, Twiga, Kiboko na Simba kama walivyojitokeza kwenye hadithi uliyoisoma.

Zoezi la 7: Utungaji

Simulia ziara kuhusu mbuga yoyote ya wanyama kwa kufuata mtiririko wa picha zifuatazo, kisha uandike hadithi fupi.



For online use only

Sura ya Kumi

Kuwasilisha mawazo makuu

Utangulizi

Katika sura hii, utajifunza kuwasilisha mawazo makuu yaliyomo kwenye hadithi ndefu. Aidha, utasoma hadithi na kueleza ujumbe uliomo katika hadithi hiyo. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuwasilisha mawazo kwa mtiririko mzuri.



Fikiri

Namna ulivyotambua mawazo makuu ya kazi yoyote uliyowahi kuisoma

Ufahamu

Soma hadithi hii, kisha jibu maswali yanayofuata.

Msitu wa Mzee Sunga na mazimwi

Hapo kale, palitokea mazimwi matatu; baba, mama na mtoto wao. Yalihangaika sana kutafuta mahali pa kuishi. Hayakufanikiwa kwa sababu, katika nchi ya Azania, misitu mingi ya asili ilikuwa imekatwa na binadamu kwa matumizi mbalimbali. Misitu michache iliyobaki ililindwa vikali na askari wa maliasili. Mazimwi hayo yalipojaribu kuingia kwenye misitu ya serikali, yalitimuliwa na askari walioilinda.

Yakiwa katika mahangaiko ya kutafuta makazi, ghafla yalijikuta kwenye msitu mzuri na mkubwa sana. Ulikuwa msitu unaopendeza, wenye vichaka, miti mingi, mirefu na mifupi yenye matunda ya aina mbalimbali na isiyo na matunda; na ma**pango** makubwa ya kale. Pia, upande mmoja wa msitu kulikuwa na bonde la maji, asali ya asili, na mizinga ya kisasa.

Mazimwi yalichekelea sana kuuona msitu huo unaopendeza. Yakaishukuru miungu yao kwa bahati hiyo. Yalianza kupanga namna ya kuishi msituni humo. Yakaanzisha makazi kwenye pango moja kubwa.

Hayakujua kuwa mmiliki wa msitu huo alikuwa Mzee Sunga ambaye aliishi kando kidogo ya msitu wake. Siku mbili baadaye, Mzee Sunga alipitapita msituni

use only
online
FOR

kukagua miti yake kama ilivyo **ada** yake. Ghafla, alisikia vicheko vya ajabu vikitoka ndani ya pango mojawapo. Alinyata kuelekea pangoni humo ili ajue vicheko hivyo vilitolewa na viumbe gani.

Yakiwa ndani ya pango, mazimwi yakasikia **mchakacho** wa kiumbe kinachoelekea langoni mwa pango. Muda huohuo, yakanusa harufu ya binadamu. Mazimwi yakakaa ange. Yalipomwona binadamu akiingia ndani ya pango, yalitumia **hirizi** ya urithi ili yatoweke machoni pake.



Baada ya kuingia pangoni, Mzee Sunga hakuona kiumbe yeyote ndani. Hata hivyo, aliona dalili za wazi kwamba kulikuwemo na viumbe muda mfupi uliopita. Ingawa kulikuwa na giza pangoni humo, aliona sehemu kubwa ya sakafu ikionesha kuwa kuna viumbe waliolala hapo usiku. Sehemu hiyo ilikuwa imetandikwa nyasi nyingi kutoka upande mmoja wa pango hadi mwingine. Pia, kulikuwa na mabaki ya kokwa na asali. Akagundua kwamba kuna wavamizi wa ajabu ndani ya msitu wake. Akaanza kuwa na wasiwasi na hofu kubwa. Akatafuta huku na kule ili ajue ni wageni gani waliovamia msitu wake, lakini hakuona kiumbe yeyote.

Mazimwi yale yalipotoweka kwa hirizi ya urithi, yalienda kujibanza kwenye pango jingine jirani. Yalikuwa yameshituka na kujaa **taharuki.** Yalipofika katika

For online

msitu huu, yalidhani yamepata mahali pa amani. Yalidhani ni msitu huru, kumbe sivyo. Yakaanza kujiuliza, “Sasa huyu binadamu anahusianaje na msitu huu? Anaonekana mzee, lakini kwa nini alikuja msituni?” Yakataka kujua zaidi. Hata hivyo, yote yakawa yameupenda msitu. Yakaamua kuwa, kwanza, yapeleleze kuhusu mmiliki wa msitu huo. Pili, kama si serikali, yamshawishi yaununue msitu. Asiposhawishika, yatumie **ulaghai**, mabavu na **miujiza**. Kwa hiyo, yakaandaa mabunda ya fedha. Kisha, yakaamua kujigeuza kuwa binadamu na kwenda kumtafuta yule mzee.

Mazimwi yakamkuta yule mzee ukingoni mwa msitu. Huu ulikuwa upande wa kijiji ambapo wananchi walijenga makazi. Mazimwi yalimsabahi na kujitambulisha kuwa ni watu kutoka kijiji cha mbali kidogo.

“Sisi ni watafiti wa misitu. Tunatafiti utaalamu wa kupanda na kutunza miti. Tuna hamu ya kuwa na msitu mzuri kama huu. Hivi msitu huu ni wa nani?” Zimwi dume liliuliza. “Huu msitu ni wangu,” alijibu Mzee Sunga.

Mazimwi yalishangaa na kufurahi kusikia kuwa msitu huo ni wa binadamu mmoja tu na si wa serikali. Tamaa ikayajaa mioyoni. Yakauliza kwa mshangao, “Kumbe! Hongera! Una bahati na una utajiri mkubwa sana wa **rasilimali.** Uliupataje msitu huu?” “Niliurithi kutoka kwa babu yangu ambaye naye aliurithi kutoka kwa babu yake. Na babu yake huyu aliurithi kutoka kwa babu yake. Kila mrithi amekuwa akipanua eneo la msitu kwa kupanda miti mbalimbali.”

“Ahaa! Tunaona miti ya aina nyingi sana. Mingine hatujawahi kuiona maishani. Waijua yote kwa majina?” Mazimwi yalizidi ku**dadisi**.

Mzee Sunga akajibu, “Naam! Ninaijua kwa majina kama niijuavyo mistari ya kiganja changu. Humu kuna mninga, mkongo, mvule, mpodo, mpingo, mkunguru, mtiki na mingine mingi.”

“Ninatamani kupata msitu kama huu. Miti hii inakufaidisha nini?” Zimwi mtoto aliuliza. Mzee Sunga akajibu, “Miti hii hutoa mbao za kujengea na kutengenezea samani mbalimbali. Mipingo hutumika kutengenezea vinyago, na mitiki hutumika kuundia majahazi na mitumbwi. Mnaona? Humu ndani pia nimening’iniza mizinga na nyuki hutengeneza asali kwa wingi.”

For Online Use Only

“Kuna harufu nzuri humu msituni.” Zimwi la kike lilisema likigeuza pua pembeni kuvuta harufu nzuri ya miti. Mzee Sunga akasema, “Kuna hewa safi na upepo **mwanana** humu kutokana na miti mbalimbali. Licha ya kusaidia kuleta mvua, miti pia huvutia ndege na wadudu wa aina mbalimbali. Wadudu na ndege hawa hupenda kurukaruka kwenye maua ya miti yanayovutia kwa harufu **murua**.”

Baada ya kusikia sifa na manufaa yote hayo, mazimwi yaliwaka tamaa. Yakaanza kumshawishi Mzee Sunga ayauzie msitu huo. Yalitoa mabunda lukuki ya pesa kumshawishi, lakini yeye alikataa akisema, “Siwezi kuuza urithi wangu **adhimu** huu. Ninawashauri mkaanzishe msitu wenu. Baada ya miaka michache, mtafaidika. Mimi nimezaliwa na kukuzwa kwa faida za msitu huu. **Katu** siwezi kuuuza.”

Mazimwi yalipoona Mzee Sunga ana msimamo mkali, yalianza kumtishia yakisema, “Sikiliza wewe mzee. Sisi tuko watatu, na wewe u peke yako tu. Unawezaje kutukatalia? Hujionei huruma mzee?” Sauti zao zilianza kubadilika. Mzee Sunga alianza kujaa hofu. Akaanza kurudi nyuma huku akitetemeka.

Zimwi dume likasema, “Usiogope mzee. Sisi ni watu wema tu. Tuuzie msitu huu tafadhali.”

Zimwi mtoto lilipogeuka kupenga kamasi pembeni, Mzee Sunga akaona kijimkia kimechomoza kidogo ndani ya kaptura. Akazidi kujaa hofu, huku akiendelea kurudi nyuma bila kujua afanye nini zaidi. Akiwa amekata tamaa, Mzee Sunga akajikwaa na kudondoka chini. Mazimwi yakamsogelea, lakini kabla hayajamfikia, sauti za ngurumo za magari zikasikika kwa nguvu. Askari wa maliasili walikuwa wamekuja msituni hapo kwa ajili ya kusaka mazimwi ambayo yalimuua mzee mmoja ambaye alikataa kuyauzia shamba lake kwenye kijiji cha kumi kutoka hapo.

Yalipowaona askari na silaha zao, mazimwi yakataharuki. Nguvu za kizimwi zikayaingia. Yakaanza kubadilika na kuwa mazimwi yanayotisha. Askari waliposogea zaidi, mazimwi yakatoweka mahali hapo. Yaka**tokomea** kusikojulikana na hayakuonekana tena katika msitu huo.

Tangu siku hiyo, Mzee Sunga alipatiwa askari wa kuulinda msitu huo, na akaendelea kufaidika na manufaa yaliyotokana na kupanda miti.

For online use only

Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Hadithi uliyoisoma inahusu nchi gani?
2. Viumbe gani waliingia katika msitu wa Mzee Sunga?
3. Kwa nini mazimwi yalikuwa yakihangaika kupata msitu wa kuishi?
4. Wewe unaweza kutumia vitu gani zaidi ya mbao kutengeneza milango vitanda na meza?
5. Ungetishiwa na mazimwi kama Mzee Sunga, ungechukua hatua gani ili kulinda mali yako?
6. Mzee Sunga alifanya uamuzi sahihi kukataa kuuza msitu wake? Kwa nini?
7. Nani alimwokoa Mzee Sunga?
8. Unafikiri kuna watu wanaofanana tabia na mazimwi katika jamii yetu?
9. Bainisha mawazo makuu katika hadithi uliyoisoma.
10. Umejifunza nini kutokana na hadithi hii?

Zoezi la pili: Msamiati

Tunga sentensi moja kwa kila neno ulilopewa.

1. pango
2. ada
3. mchakacho
4. hirizi
5. taharuki
6. ulaghai
7. miujiza
8. rasilimali
9. dadisi
10. mwanana
11. murua
12. adhimu
13. katu
14. tokomea

For online use only

Zoezi la 3: Nahau na misemo

Tunga sentensi mbili kwa kila nahau na misemo.

1. piga moyo konde
2. kaa ange
3. tua mzigo
4. angua kilio
5. ona fahari

Zoezi la 4: Methali

Chagua methali sahihi kutoka kwenye kisanduku, kisha iandike mbele ya maelezo yanayoonesha matumizi yake.

Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu,
Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu,
Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki wa kweli,
Asiyesikia la mkuu, huvunjika guu,
Ukiona vyaelea, ujue vimeundwa,
Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo

1. Mzee Mdolo alikuwa anatetea tabia ya wizi iliyokuwa inafanywa na mtoto wake hapo kijijini. Siku moja, mtoto wake aliiba mbuzi kwenye zizi la baba yake. Tangu siku hiyo, mzee Mdolo aliamini kuwa .....

2. Kijiji cha Namile kilivamiwa na chui. Mwenyekiti alipiga mbiu ya mgambo. Wanakijiji walikusanyika haraka wakaenda kumsaka. Baada ya muda mfupi chui alikuwa ameuawa. Sasa nimeamini kuwa .....

3. Nilikuwa mchezaji mzuri wa mpira wa miguu kwa miaka mingi. Siku moja, nilivunjika mguu uwanjani. Wachezaji wote waliniacha uwanjani nikigaagaa kwa maumivu. Kamokene alinionea huruma; alinibeba na kunipeleka hospitalini. Nikakumbuka usemi wa wahenga usemao kuwa .....

4. Shazimwa ni mwanafunzi aliyekuwa na mahudhurio hafifu shuleni. Walimu na wazazi wake walimshauri kuacha tabia hiyo lakini hakuwasikia. Katika matokeo ya kuhitimu elimu ya msingi, Shazimwa ndiye mwanafunzi pekee aliyefeli mtihani. Sasa amejifunza kuwa .....

For online use only

5. Mazimwi yalitamani msitu wa Mzee Sunga ambao ulikuwa umetunzwa vizuri. Msitu ulikuwa umesheheni miti ya aina mbalimbali. Walitaka kumpokonya msitu ule uwe wao. Walijisahau kuwa .....

Zoezi la 5: Mazoezi ya lugha

A. Andika maneno yenye maana sawa na haya yafuatayo:

(i) stawi _____

(ii) idhini _____

(iii) penda _____

(iv) tembelea _____

(v) samani _____

(vi) tunza _____

(vii) vuta _____

(viii) kwea _____

(ix) pasua _____

(x) toweka _____

B. Andika neno moja badala ya orodha ya maneno.

(i) mpodo, mpingo, mkunguru, mvule, mninga, mtiki _____

(ii) viti, meza, kabati, dawati, kitanda _____

(iii) nyuki, kipepeo, siafu, panzi, sisimizi, ng'e _____

(iv) tembo, swala, chui, simba, pundamilia, twiga _____

(v) Kiswahili, Kiingereza, Sayansi, Hisabati, _____

(vi) nusu, robo, theluthi _____

(vii) mahindi, mtama, uwele, ulezi _____

(viii) mkuki, rungu, sime, gobore, bunduki _____

(ix) bakuli, sahani, sufuria, kikombe, kijiko _____

(x) mchicha, kisamvu, mnavu, spinachi, matembele _____

For online use only

C. Jibu maswali yafuatayo kwa kuandika KWELI au SI KWELI.

(i) Misitu ni sehemu ya mazingira. _____

(ii) Vichaka, nyasi, miti mifupi na mirefu ni msitu. _____

(iii) Viumbe wote huishi msituni. _____

(iv) Jangwa ni sehemu iliyojaa maji. _____

(v) Binadamu hutegemea misitu katika maisha yake. _____

(vi) Misitu hutupatia vyakula kama vile matunda. _____

(vii) Misitu huleta mvua ambayo hustawisha mazao. _____

(viii) Kazi yakutunza na kulinda misitu ni ya serikali peke yake. _____

(ix) Miti hutupatia kivuli. _____

(x) Ukataji wa miti hufanywa na binadamu. _____

D. Chagua jibu sahihi kujaza nafasi zilizoachwa wazi.

Mfano: Kitabu _____ kimeibwa. (*lake, changu, vyao*)

Kitabu <u>changu</u> kimeibwa.

Matokeo ya mtihani _____ ni mazuri. (changu, yangu, wangu)

Matokeo ya mtihani <u>wangu</u> ni mazuri.

(i) Msitu _____umestawi. (*wangu, yenu, hao)*

(ii) Alipovuna miti _____ alipasua mbao. (*kile, yake, ule*)

(iii) Shamba _____ la miti lilikuwa kubwa. (*lake, changu, chetu*)

(iv) Kipato_____kilitokana na kuuza mbao. (*lao, langu, chake*)

(v) Wachongaji huuza vinyago _____kwa bei kubwa. (*chetu, chake, vyao*)

(vi) Askari_____wa maliasili walilinda misitu. (*wetu, ake, vyake)*

(vii) Mbao_____ni za mkaratusi. (*yenu, yake, zake*)

(viii) Tuitunze misitu_____kwa sababu ina faida nyingi. (*yetu, letu, chao)*

For online use only

(ix) Kikombe_____ni kidogo. (*lile, hiki, yenu*)

(x) Mtu_____ana hasira. (*wale, yenu, yule*)

(xi) Nguo_____zimekauka. (*ile, yao, hizi*)

E. Andika neno moja linalowakilisha maelezo uliyopewa.

(i) Mzee Mwita yeye ni mtaalamu wa kutengeneza samani za aina mbalimbali kwa kutumia mbao. Kwa kazi anayofanya Mzee Mwita, utamwitaje?

(ii) Mjomba wangu anafanya kazi ya kuendesha na kuongoza meli. Kwa kazi anayofanya Mjomba wangu utamwitaje?

(iii) Kaka yangu anaendesha na kuongoza ndege. Kaka yangu utamwitaje?

(iv) Mama alimwambia kaka, "Panda juu ya mnazi ukaangue nazi." Anayeangua nazi utamwitaje?

(v) Dada anafanya kazi ya kupeleka au kuchukua barua posta au katika ofisi nyingine. Kwa kazi anayofanya dada, utamwitaje?

(vi) Asha hutengeneza vitu vizuri kwa kutumia udongo. Asha utamwitaje?

(vii) Mpwa wangu ameajiriwa kwa kazi ya kulinda raia na mali zao. Mpwa wangu utamwitaje?

(viii) Binamu yangu anafanya kazi ya kufua nguo za watu mbalimbali wanaohitaji huduma hiyo. Je, binamu yangu utamwitaje?

(ix) Kidawa ana uzoefu wa siku nyingi wa kutengeneza vidani na kuviuza sehemu mbalimbali. Je, Kidawa utamwitaje?

F. Andika neno lililo tofauti na mengine katika maneno yafuatayo:

(i) figo, moyo, jipu, ini, mapafu

(ii) kisima, chemchemi, bomba, mito, mabwawa

(iii) jua, nyota, mwezi, umeme, taa

(iv) malaria, kipindupindu, mbu, kichocho, UKIMWI,

(v) kompyuta, simu, soketi, redio, televisheni

For online use only

(vi) togwa, titi, chai, uji, maziwa

(vii) kichuguu, kiota, zizi, sega, zeze

(viii) msafara, msururu, msukumo, mnyororo, foleni,

(ix) mtumbwi, nanga, boti, jahazi, meli

(x) zulia, mkeka, godoro, shuka, kirago

Kazi ya kufanya

A. Fupisha habari ya Msitu wa Mzee Sunga na mazimwi kwa maneno kati ya thelathini (30) na hamsini (50).

B. Tafuta hadithi unayoipenda kutoka kwenye kitabu, kisha soma hadithi hiyo kwa makini na andika kwa mpangilio mzuri mawazo makuu.

Zoezi la 6: Utungaji

Andika wazo kuu la kila ubeti wa shairi lifuatalo:

Maua

1. *Enyi jicho la taifa, tunu kuwaandalia,*
   Motomoto zenu sifa, darasa hili sikia,
   Yangu haya maarifa, kinga mikono pokea,
   Maua ni kitu bora, mazingira kuyapamba.

2. *Maua hupatikana, kila kona duniani,*
   Yapo yenye kupatana, yakipandwa masikani,
   Ua hutambulikana, kwa pua au uoni,
   Maua ni kitu bora, mazingira kuyapamba.

For Online Use Only

3. *Miti ina utajiri, wa maua mbalimbali,*
Na matunda hushamiri, karibu hata kwa mbali,
Wanyama ndege wakiri, hufurahia manzili,
Maua ni kitu bora, mazingira kuyapamba.

4. *Twatambua kwa majina, ua sa' sita murua,*
Rangi zake kuziona, machoni zinavutia,
Mawaridi kupangana, rangize kugombania,
Maua ni kitu bora, mazingira kuyapamba.

5. *Asumini nalo ua, jioni linachanua,*
Harufu nzuri kutoa, popote linanukia,
Shada kutengenezea, na nywele kuzifungia,
Maua ni kitu bora, mazingira kuyapamba.

6. *Lingine ua la mwafu, mafuta kutengeneza,*
Huvutia kwa harufu, ni nzuri ya kupendeza,
Mkayakaya nasifu, ua lake huangaza,
Maua ni kitu bora, mazingira kuyapamba.

7. *Matunzo yalo muhimu, palizi hata mbolea,*
Maji yasiwe adimu, kumbuka kupogolea,
Na viwavi wasidumu, kuisitisha ghasia,
Maua ni kitu bora, mazingira kuyapamba.

For Online use Only

8. *Faida kujipatia, ni nyingi kupitiliza,*
Bayana kukutajia, utajiri 'natangaza,
Wapambaji hununua, ili kumbi kupendeza,
Maua ni kitu bora, mazingira kuyapamba.

9. *Ghaibuni twapeleka, na wao huyanunua,*
Dola nyingi twazishika, uchumi kuunyanyua,
Epuka kuhangaika, sasa ajira pokea,
Maua ni kitu bora, mazingira kuyapamba.

10. *Wito wangu sasa kwenu, jembe na mbegu mshike,*
Shuleni kumbuka kwenu, maua mahali pake,
Maua fahari yenu, na kanuni mzishike,
Maua ni kitu bora, mazingira kuyapamba.

For online use

Sura ya Kumi na Moja

Utoaji wa hoja

Utangulizi

Katika sura hii, utajifunza namna ya kutoa hoja na kueleweka kwa kutumia msamiati unaoendana na muktadha mahususi wa mazungumzo. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kufikiri kwa ufanisi na kutoa hoja kwa mpangilio unaoeleweka.



Fikiri

Namna ya kutoa wazo linaloeleweka kwa mwenzio

Ufahamu

Soma na ghani utenzi ufuatao, kisha jibu maswali yanayofuata.

Usafi

1. *Leo nashika kalamu,*
   Kusema jambo muhimu,
   La kukazia nidhamu,
   *Usafi ku**zingatia**.*

2. *Wameshafunza walimu,*
   Usafi mada muhimu,
   Bali hili somo gumu,
   Nami nitaongezea.

3. *Usafi huwa ni **kinga**,*
   *Ya maradhi yano**zonga**,*
   *Ni waganga wame**longa**,*
   Walimu wamekazia.

4. *KWANZA, usafi wa kinywa,*
   Ni muhimu kuambiwa,
   Hukinga mengi magonjwa
   ***Rihi** mbaya kuzuia.*



5. *Ukiamka ‘subuhi,*
   Kupiga mswaki wahi,
   *Kabla ya **staftahi**,*
   Meno kwa dawa sugua.

6. *Unapopiga mswaki,*
   Safisha yote mabaki,
   *Ya chakula yalo**saki**,*
   Menoni yakagandia.

FOR online use only

7. *Yasafishe meno sawa,*
Uchafu wote suguwa,
Kwao mswaki na dawa,
Meno ya nyuma anzia.

8. *Pia ulimi sugua,*
Kisha kinywa ***sukutua****,*
Watu watakukimbia,
Kama harufu watoa.

9. *PILI, usafi mwilini,*
Oga tumia sabuni,
*Dodoki liku****auni***
Mwilio kusugulia



10. *Uchafu haupendezi,*
Oga ondoa ***kutuzi****,*
Sehemu zote za ngozi,
Na za siri zingatia.

11. *Mwili ukiwa* ***nadhifu****,*
Viungo huwa ***kunjufu***
Nawe huwa furahifu,
Usafi kufurahia.

12. *TATU, usafi wa nguo*
Ni muhimu kwa afya
Sabuni ndo kifulio,
Nguozo kuzifulia.



13. *Nguo safi kivutio,*
Nguo chafu kichefuo,
Usafi kila uchao,
Ni ada ya kuwania.

14. *Kijana utapendeza,*
Usafi ukitimiza,
Lakini utachukiza,
Nguo chafu ukivaa.

15. *NNE, usafi shuleni,*
Darasani na vyooni,
Mazingira ya shuleni,
Yawe nadhifu sikia.



16. *Fyeka nyasi viwanjani,*
Fagia taka njiani,
Pawe safi vivulini,
Nawe utafurahia.

17. *Bustani za maua,*
Vema kuzipangilia,
Pia kuzimwagilia,
Mimea itachanua.

18. *TANO, usafi nyumbani,*
Wazazi wape auni,
Bafu, jiko na chooni,
Usafi iwe tabia.

19. *Kiwe safi chumba chako,*
Ufue mashuka yako,
Tandika kitanda chako,
Unadhifu zingatia.



20. *Usafi kuzingatia,*
Ni nidhamu ya murua,
Wazazi kusaidia,
Ni ya kuiga tabia.

FOR online use only

21. *Mengi nimezungumza,*
Bali mengi nimesaza,
Usafi nimehimiza,
Muhimu kuzingatia.

Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Utenzi huu unazungumzia jambo gani muhimu?
2. Ukiamka asubuhi, unafanya nini kwanza?
3. Nini kitatokea usipofanya usafi wa kinywa?
4. Eleza ujumbe unaopatikana katika ubeti wa 12 na 18.
5. Je, usafi unafanyikaje shuleni?
6. Unapaswa kufanya nini kuhusu chumba chako?
7. Bustani za maua zinapaswa kuhudumiwa vipi?
8. Wewe ungekuwa ndiye mwandishi wa utenzi huu, ungezungumzia usafi gani mwingine?
9. Umejifunza nini kutokana na utenzi uliousoma?

Zoezi la pili: Msamiati

Tunga sentensi moja kwa kila neno.

1. zingatia
2. kinga
3. zonga
4. longa
5. rihi
6. staftahi
7. saki
8. sukutua
9. auni
10. kutuzi
11. nadhifu
12. kunjufu

FOR Use Only Online

Zoezi la 3: Methali

Kamilisha methali zifuatazo:

1. Macho .....
2. Meno ya mbwa .....
3. Ulimi unauma .....
4. Mwenye mdomo .....
5. Ulimi .....
6. ..... faraja.
7. ..... si chururu.
8. ....., utajenga ukuta.
9. ....., ndio ulimwengu.
10. ..... hashibi.

Zoezi la 4: Nahau na misemo

Tumia vifungu vya maneno vilivyopo kwenye kisanduku kutoa maana ya nahau na misemo ifuatayo:

kujitia matatani, fuata mawazo ya wengine bila kujali usahihi au la, kaa kimya, kuwa kigeugeu, kuwa na wasiwasi

1. kuwa popo .....
2. fuata upepo .....
3. kuwa tumbo joto .....
4. fyata mkia .....
5. kujipalia mkaa .....

Zoezi la 5: Vitendawili

Tegua vitendawili vifuatavyo:

1. Nina jani moja likipasukapasuka huwa nyasi.
2. Nikipiga kelele kila mtu hunikimbilia.
3. Nina macho mengi lakini siwezi kuona.
4. Ni langu lakini wengine wanalitumia kuliko mimi.

For online use only

5. Sina miguu lakini ninatembea, sina mdomo lakini ninazungumza.
6. Akitokea, watu wote hunung'unika na kuwa na huzuni.
7. Ameingia shimoni akiwa hajavaa nguo, katoka akiwa amevaa nguo.
8. Amejiingiza jela mwenyewe.

Zoezi la 6: Mazoezi la lugha

A. Panga sentensi zifuatazo katika mpangilio sahihi.

(i) Siku ya jaribio ilipowadia, wanafunzi waliwahi kufika shuleni.

(ii) Wanafunzi walifanya usafi wa darasa na kupanga madawati yao.

(iii) Walipomaliza kufanya jaribio, walitawanyika.

(iv) Siku iliyofuata, Mwalimu Koja alihakikisha kila mwanafunzi ana mahali pa kukaa.

(v) Kila mwanafunzi aliingia darasani na kukaa mahali pake.

(vi) Wanafunzi walifanya jaribio.

B. Andika sentensi zifuatazo katika hali ya uyakinishi.

(i) Juhudi hataharibu kitabu cha shule.

(ii) Cheko hakufika mapema shuleni leo.

(iii) Mfugaji hakwenda kuuza ng'ombe mnadani.

(iv) Mvuvi hakuvua samaki wengi.

(v) Kijana hakuogelea vizuri sana.

(vi) Tumaini hakumaliza kazi zote za nyumbani kwa haraka.

(vii) Kiranja hakusimamia kazi vizuri.

(viii) Kaka hakufyeka majani marefu.

(ix) Timu yetu haikufunga magoli mengi.

(x) Dada hakuezeka nyumba yote.

For online use only

C. Oanisha maana za nahau na misemo zilizopo Sehemu A na nahau na misemo katika Sehemu B.

Sehemu A	Sehemu B
(i) Kuweka mambo wazi	A. Kuwasilisha wazo, maoni au mapendekezo mbele ya wahusika au wasikilizaji
(ii) Kutoa hoja mbele ya jopo	B. Kufafanua jambo kwa uwazi na bila kutetereka ili kuepuka mkanganyiko
(iii) Kutetea haki	C. Kuchambua mambo na kuyalinganisha kwa haki ili kutoa uamuzi sahihi
(iv) Kuweka mambo kwenye mizani	D. Kuonesha kielelezo halisi kinachohusiana moja kwa moja na hali halisi ya maisha katika kuthibitisha hoja
(v) Kusimama imara	E. Kutoa maoni au pendekezo jipya linalofaa
(vi) Kutoa hoja kistaarabu	F. Hitimisha hoja katika kikao, mjadala au mazungumzo
(vii) Kutoa mifano hai	G. Kutoa hoja kwa ajili ya kusimamia ukweli
(viii) Kufunga mviringo	H. Kujieleza kwa namna ya wazi yenye mantiki inayowashawishi wasikilizaji/wasomaji
(ix) Kusema wazi wazi	I. Kutoa lawama au shutuma bila ya kuzielekeza kwa mtu mahususi
(x) Kutupa wazo la kipekee	J. Kuunda au kuandika mawazo kwa ufanisi na usahihi
(xi) Kutoa hoja kwa ufanisi	K. Kudumisha au kushikilia msimamo kuhusu jambo fulani bila kuyumba
(xii) Kufunua ukweli	L. Kutoa uthibitisho wa kutosha kuunga mkono hoja yako

For Online Use Only

Sehemu A	Sehemu B
(xiii) Kutoa ushahidi thabiti	M. Kuweka wazi au kumulika jambo lililofichika
(xiv) Kutupa jiwe gizani	N. Kusema bila kificho wala kuzunguka, ili kutoa hoja kwa urahisi
(xv) Kusuka hoja	O. Kuwasilisha maoni au maneno kwa njia ya heshima na kwa staha, bila uchokozi



Kazi ya kufanya

Shiriki katika mdahalo wenye mada inayosema, “Michezo ni muhimu kwa jamii.”



Zoezi la 7: Utungaji

Tunga majadiliano ya wahusika watatu kuhusu “Kilimo ni uti wa mgongo.” Maneno yasizidi mia mbili (200).

For online use only

Sura ya Kumi na Mbili

Kujibu barua za kirafiki

Utangulizi

Katika sura hii, utajifunza namna ya kujibu barua za kirafiki. Pia, utajifunza vipengele muhimu katika kujibu barua ya kirafiki. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuandika barua za kirafiki kwa usahihi.



Fikiri

Njia utakayoitumia kuwasiliana na rafiki yako ambaye yupo mbali na wewe kumtaarifu kuwa umeingia Darasa la Tano

Ufahamu

Soma habari hii, kisha jibu maswali yanayofuata.

Nia na mdogo wake

Nia ni mwanafunzi wa Shule ya Msingi Ushindi katika Wilaya ya Bora, mkoani Sanya. Baba yake Nia anaitwa Bwana Fukama na mama yake anaitwa Bibi Sokota. Nia ana mdogo wake aitwaye Bute. Nia na mdogo wake wanaishi katika Kijiji cha Kibeta, kilometa tatu kutoka Shule ya Msingi Ushindi. Nia anasoma Darasa la Tano lakini Bute anasoma Darasa la Kwanza. Siku za shule, Nia humuamsha mdogo wake mapema ili kupata kifungua kinywa kabla ya kwenda shuleni.

Siku moja, Nia alichelewa sana kuamka. Alipoamka, alimwamsha mdogo wake kisha wakajiandaa harakaharaka ili waweze kuwahi kwenda shuleni. Baada ya kunywa chai, waliwaaga wazazi wao. Walianza safari yao ya kwenda shuleni. Wakiwa njiani, Nia alitangulia mbele na Bute alimfuata nyuma. Nia alitembea harakaharaka huku akim**himiza** Bute kuongeza mwendo. Kadiri muda ulivyozidi kusogea, Nia aliongeza mwendo bila kugeuka nyuma.

For online use only



Nia na Bute walifika kwenye Daraja la Kitunda. Walipofika hapo, Bute alivutiwa na vipepeo wa rangi mbalimbali. Vipepeo hao waliruka huku na kule wakifurahia maua yaliyokuwa yamezunguka Daraja la Kitunda. Badala ya kuvuka daraja, Bute alisimama na kuwatazama vipepeo hao akitamani kumkamata mmojawapo. Huku Bute akiwa amesimama, Nia aliendelea na safari bila kujua kwamba mdogo wake alikuwa akishangaa vipepeo.

Bute alianza kuwafuata vipepeo. Vipepeo waliruka wawezavyo ili kukwepa kukamatwa. Bute aliendelea kuwakimbiza. Bila kujua, alijikuta katikati ya msitu mnene. Hakuweza ku**tambua** alikotokea. Alisimama na kuanza kumwita dada yake pasipo mafanikio. Alijaribu kutafuta njia ya kurudi darajani bila mafanikio. Baada ya kutembea kwa muda mrefu, alichoka sana. Aliamua kupumzika chini ya mti na kuanza kulia. Baada ya muda, alipitiwa na usingizi; akalala fofofo.

Nia, bila kujua, aliendelea na safari ya kuelekea shuleni. Alipokaribia, aligeuka nyuma kumtazama mdogo wake lakini hakumwona. Alishituka akaanza kurudi nyuma huku akiita kwa sauti, “Bute! Bute! Buteeee...!” Nia aliendelea kuita kwa sauti huku akikimbia kurudi darajani. Njiani alikutana na watoto wawili. Akawauliza, “Mmemwona mwanafunzi wa kiume mwenye begi lenye rangi nyeusi?” Watoto walijibu, “Hapana dada!” Nia aliendelea na safari ya kurudi nyumbani akidhani kwamba angemkuta mdogo wake.

FOT Online

Alipofika nyumbani, aliwakuta wazazi wake wakijiandaa kwenda shambani. Nia alikuwa ame**lowa** jasho mwili mzima. Alikuwa aki**hema** na alionekana amechoka sana. Wazazi wake wali**shituka** na kumkimbilia. Walimuuliza, "Vipi, mbona umerudi mapema?" Nia alijibu, "Bute amepotea." Wazazi wake walipatwa na **hofu** na wasiwasi. Kila mmoja alishika njia yake kumtafuta Bute.

Nia aliamua kuandika tangazo ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa ya kupotea kwa Bute. Aliandika hivi:

TANGAZO MUHIMU
BUTE FUKAMA AMEPOTEA

Bute ni mtoto mwenye umri wa miaka saba. Ni mwanafunzi wa Darasa la Kwanza katika Shule ya Msingi Ushindi, iliyoko Wilaya ya Bora, mkoani Sanya. Bute amepotea tarehe **22/04/2018** saa **1 : 15** asubuhi. Mara ya mwisho alionekana katika Daraja la Kifunda akiwa amevaa sare ya shule, kaptura yenye rangi ya bluu na shati jeupe na alibeba begi la rangi nyeusi mgongoni. Kwa yeyote atakayemuona, apige simu namba **2550123/2550321** au atoe taarifa kwenye kituo chochote cha polisi.

For online use only

Baada ya kuandaa tangazo, alikumbuka kuwa alihitaji kuwa na **nakala** nyingi. Aliandika nakala kumi. Alipokamilisha kazi yake, alifungua mlango na kuelekea nje. Alipiga mbio kuelekea vijiji vya jirani. Alisambaza matangazo yake kwa umakini. Baadhi aliyaweka kwenye kuta za majengo na mengine kwenye miti iliyokuwa karibu na njia.

Baada ya kazi yake kukamilika, alianza safari ya kuelekea shuleni. Alipofika shuleni, aliwaeleza walimu kilichotokea. Walimu walimpa pole na kumtia moyo kwamba mdogo wake atapatikana. Walisisitiza kwamba hatapatikana, saa tisa mchana watatawanyika kwenda kumtafuta. Nia aliingia darasani.

Ilipofika saa nane, Nia alienda ofisini kwa walimu kuuliza kama wamepata taarifa zozote kuhusu mdogo wake. Alipofika ofisini, alishangaa kumwona Bute ameketi ofisini. Alikuta walimu wakizungumza na kijana mmoja aliyetambulishwa kwa jina la Bahati. Bahati alisema, “Nimemkuta mtoto amelala chini ya mti wakati ninakata kuni. Niliondoka naye kuelekea nyumbani. Nikiwa njiani, niliona tangazo lililotaja jina la shule hii. Niliamua kumleta hapa shuleni.” Nia alifurahi sana kumpata mdogo wake. Walimu walifurahi pia. Walim**pongeza** Nia kwa kutumia vyema maarifa aliyoyapata darasani.

Nia na Bute walirudi nyumbani. Wazazi wao walifurahi sana kwa kumwona Bute. Baada ya wiki mbili, Nia alipokea barua kutoka kwa rafiki yake Suma; alimwandikia kumuuliza kama mdogo wake amepatikana. Baada ya kupokea ile barua, Nia alikumbuka kuwa mwalimu wake wa Kiswahili aliwafundisha kuhusu kujibu barua ya kirafiki. Siku iliyofuata jioni, Nia aliingia chumbani kwake, akachukua kalamu na karatasi kwenye begi lake na kuanza kuandika barua ya kumjibu Suma. Aliandika hivi:

Shule ya Msingi Ushindi,
S.L.P. 45,
Bora.

07/05/2018.

Kwako rafiki yangu Suma,

Salamu nyingi sana zikufikie huko uliko. Unaendeleaje na hali yako? Ninatumaini uko salama na unaendelea vyema na shughuli zako za kila siku.

Lengo la barua hii ni kujibu barua uliyoniandikia kuhusu kupotea kwa mdogo wangu. Ninayo furaha kukupa taarifa kwamba mdogo wangu mpendwa Bute alipatikana. Yuko salama na afya yake njema.

Salamu nyingi kwa wazazi wako.

Mimi rafiki yako,

Nia Fukama.

For online use only

Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Nia na mdogo wake waliishi katika kijiji gani?
2. Bute alikuwa mwanafunzi wa darasa la ngapi?
3. Bute alipofika Daraja la Kitunda, alivutiwa na nini?
4. Wazazi wa Nia walipopata taarifa ya kupotea kwa Bute walifanya nini?
5. Nia alikumbuka mwalimu wake wa Kiswahili aliwafundisha kuhusu nini?
6. Nia aliporudi nyumbani kutoa taarifa kwa wazazi wake alifanya nini?
7. Wewe ungekuwa ni Nia ungefanya nini?
8. Vitu gani vilimtambulisha Bute kwenye tangazo?
9. Barua aliyoiandika Nia ilihusu nini?
10. Habari hii inatufundisha nini?

Zoezi la pili: Msamiati

Tunga sentensi mbili kwa kutumia maneno yafuatayo:

1. himiza
2. tambua
3. lowa
4. hema
5. shituka
6. hofu
7. nakala
8. pongeza

Zoezi la 3: Miundo

Kamilisha miundo ifuatayo:

1. ..... akiwa .....

   Mfano: *Mama mkubwa alipata shahada ya kwanza <u>akiwa</u> na umri mdogo.*

2. ..... kwamba .....

   Mfano: *Baba aliniambia <u>kwamba</u> niwahi kurudi nyumbani.*

3. ..... kuwa .....

   Mfano: *Rafiki yangu alisema <u>kuwa</u> niende nyumbani kwao wakati wa likizo.*

4. ..... ili .....

   Mfano: *Mwalimu alitufundisha vizuri <u>ili</u> tuweze kuelewa somo.*

5. ..... ingawa .....

   Mfano: *Sote tulilala usingizi mnono <u>ingawa</u> vyura walitupigia kelele.*

For online use only

Zoezi la 4: Nahau na misemo

unga mkono, kuvuja jasho baridi, kushituka kwa kivuli, moyo kuwa mdogo

Chagua nahau kutoka kwenye kisanduku, kisha uioanishe na maelezo yanayoendana nayo.

1. Mama yake Nia alikuwa na woga mwingi, alishindwa kujikaza baada ya kupata taarifa ya Bute kupotea. _____

2. Nia alipofika nyumbani alitokwa na majimaji mwilini kwa kuhisi hofu au wasiwasi mkubwa. _____

3. Tangu siku alipopotea, Bute aliendelea kuwa na hofu hata kwa vitu vidogovidogo. _____

4. Wanakijiji waliungana na wazazi wa Nia kumtafuta Bute. _____

Zoezi la 5: Mazoezi ya lugha

A. Badili sentensi zifuatazo kuwa katika hali ya uyakinishi.

Mfano: Hapendi kucheza mpira wa miguu.

Anapenda kucheza mpira wa miguu.

Mtoto huyu si mtukutu.

Mtoto huyu ni mtukutu.

Sisi hatukula matunda.

Sisi tulikula matunda.

(i) Sheku si mtoto wa pili kuzaliwa.

(ii) Yeye hakusoma kwa bidii.

(iii) Maji yote hayajamwagika.

(iv) Kaka hafundishi chuo kikuu.

(v) Wao hawataishi maisha ya furaha.

(vi) Ninyi hamtaanza masomo mwaka kesho.

(vii) Babu hatanisomesha.

For online use only

(viii) Sikushindwa kukwambia jambo hili.

(ix) Tausi hapendi kusoma vitabu.

(x) Doto hatakuwa mwanafunzi bora.

B. Andika kinyume cha maneno yafuatayo:

(i) panga _____

(ii) semesha _____

(iii) safisha _____

(iv) washa _____

(v) kubwa _____

(vi) mnene _____

(vii) sukuma _____

(viii) tema _____

(ix) fukia _____

(x) pakia _____

C. Panga vipengele vifuatavyo katika mtiririko sahihi wa uandishi wa barua ya kirafiki.

(i) Utangulizi

(ii) Kiini/madhumuni ya barua

(iii) Salamu

(iv) Hitimisho

(v) Saini/jina la mwandishi

(vi) Tarehe

(vii) Anwani ya mwandishi

D. Tumia maneno yaliyopo kwenye kisanduku kukamilisha vipengele vya barua ya kirafiki.

Johari Hashimu, S.L.P. 3, nilipokea barua uliyoniandikia, J.Hashimu, 9/4/2025, Wasalimie wadogo zangu, nauli

FOR online use only

Shule ya Msingi Mwazye,
(i).....
Kalambo.

(ii).....

Mpendwa baba,

Shikamoo! Mimi ninaendelea vizuri na masomo. Pia, ninajiandaa na mtihani wa nusu muhula wa kwanza ambao tutafanya mwishoni mwa mwezi Mei.

Madhumuni ya barua hii ni kukutaarifu kuwa (iii) .....

pamoja na (iv) ..... Hivyo, nitaanza safari ya kurudi nyumbani baada ya kumaliza mtihani. Asante sana!

(v).....

Mimi mwanao,

(vi) .....
(vii).....

E. Rafiki yako wa Shule ya Msingi Ikorongo, S.L.P. 176, Mugumu - Serengeti, iliyopo mkoani Mara, amekuandikia barua ya kukupongeza kwa kuingia Darasa la Tano. Mjibu barua hiyo kwa kuzingatia vipengele vya barua ya kirafiki.

F. Andika KWELI au SI KWELI kuonesha kukubali au kukanusha wazo lililotolewa.

(i) Unapojibu barua ya kirafiki, unatakiwa kuandika anuani yako juu ya bahasha.

(ii) Unapojibu barua ya kirafiki, unatakiwa kuandika anuani yako tu katika barua.

(iii) Unapojibu barua, lazima ujue mahusiano yako na yule unayemwandikia.

(iv) Unapojibu barua ya kirafiki, unaanza na anuani ya aliyekuandikia barua.

(v) Unapojibu barua ya kirafiki, ni muhimu kuandika kumbukumbu namba.

For online use only

G. Soma barua ifuatayo, kisha andika barua kumjibu aliyeiandika.

Shule ya Msingi Shangarao,
S.L.P. 7022,
Arusha.

20/04/2025.

Mpendwa rafiki yangu Diana,

Habari za masomo? Ni matumaini yangu kuwa u mzima wa afya njema. Mimi na wazazi wangu hatujambo kabisa.

Lengo la barua hii ni kutaka kukujulisha kwamba, michezo ya UMITASHUMTA imeshaanza na kwa sasa tupo ngazi ya wilaya. Mimi nimeshinda mchezo wa ngoma; ni manju wa kuongoza ngoma. Ningependa kujua wewe umeshiriki mchezo gani na kwa sasa mpo ngazi ipi. Kwa upande wangu, ninaendelea na mazoezi ili nishinde ngazi ya mkoa hadi taifa. Walimu na wazazi wangu wananipa moyo kuwa nina kipaji cha kucheza ngoma. Mwalimu wangu wa sanaa na michezo ameniahidi kuendeleza kipaji changu.

Ni matumaini yangu kuwa utajibu barua hii.

Ni mimi rafiki yako,

Salma Maulidi.

Kazi ya kufanya

Andika barua zifuatazo:

(i) Rafiki yako amekuandikia barua kukualika katika sherehe yake ya siku ya kuzaliwa. Mwandikie barua kumjibu kuwa utahudhuria sherehe hiyo.

(ii) Mzazi wako amekuandikia barua kuulizia maendeleo ya masomo yako. Mwandikie barua kumjibu ukimweleza kuhusu maendeleo yako ya masomo.

Zoezi la 6: Utungaji

Tafuta kitabu cha Kiswahili Darasa la Nne, kisha soma barua ya mwanafunzi mwenzako Kabula iliyopo ukurasa wa 62. Andika barua ya kumtakia heri katika ziara yao ya Kiwandani Mtibwa, kisha iweke kwenye bahasha tayari kwa kupelekwa posta.

For online use only

Sura ya Kumi na Tatu

Kuchambua mawazo katika matini

Utangulizi

Katika sura hii, utajifunza kuchambua mawazo mbalimbali yanayojitokeza katika matini, zikiwemo nyimbo na mashairi. Utaimba nyimbo, utaghani mashairi, na utachambua mawazo yaliyomo katika matini hizo. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kubainisha kwa usahihi mawazo yaliyomo katika matini mbalimbali.



Fikiri

Namna unavyoweza kuchambua mawazo katika matini

Ufahamu

Ghani shairi lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.

Naipenda nchi yangu

1. *Naipenda nchi yangu, yenye wingi wa neema,*
   Ni bora maumbileye, popote ukitazama,
   Miinuko na mabonde, tambarare na milima,
   Naisifu nchi yangu, nchi yangu Tanzania.



For Online Use Only

2. *Ina maziwa makubwa, Nyasa pia Tanganyika,*
Na ziwa kubwa kabisa, ni Nyanza lafahamika,
Pia maziwa madogo, ni mengi kuhesabika,
Naisifu nchi yangu, nchi yangu Tanzania.



3. *Yenye mlima mrefu, Afrika unatajika,*
Waitwa Kilimanjaro, duniani wasifika,
*Watu wengi huupanda, **kilele**ni wakafika,*
Naisifu nchi yangu, nchi yangu Tanzania.



For online use only

4. *Mito mikubwa midogo, ni mingi kuhesabika,*
Mingi yao maziwani, baharini humwagika,
*Na **vijito** kiangazi, kifikapo hukauka,*
Naisifu nchi yangu, nchi yangu Tanzania.



5. *Ina mbuga za wanyama, na misitu ya hifadhi,*
*Urithi wa kupendeza, nchi yangu ya u**hodhi**,*
*Kuyaona haya yote, ninataka kwa **ghaidhi**,*
Naisifu nchi yangu, nchi yangu Tanzania.



For Online Use Only

6. *Utajiri ardhini, ni mwingi kupindukia,*
*Lo! Madini **tumbitumbi**, ardhini kuzamia,*
Tanzanaiti dhahabu, almasi rubi pia,
Naisifu nchi yangu, nchi yangu Tanzania.



7. *Nchi ya utamaduni, murua unaokua,*
Wa sasa na wa zamani, haki unazingatia,
***Wigo** ni mpana sana, kwa aina za **sanaa**,*
Naisifu nchi yangu, nchi yangu Tanzania.



For Online Use Only

8. *Ni nchi ya Kiswahili, lugha yetu asilia,*
Lugha yetu ya taifa, na pia ya Jumuia,
Na Umoja wa Afrika, lugha hii hutumia,
Naisifu nchi yangu, nchi yangu Tanzania.



9. *Ni nchi ilonuia, kupiga nyingi hatua,*
Kukuza kilimo chetu, tuwe na hadhi murua,
Sayansi tukazanie, uchumi tutainua,
Naisifu nchi yangu, nchi yangu Tanzania.









For online use only

10. *Wasifu wa nchi yangu, sasa ninamalizia,*
Sifa hizi zimetosha, ni nyingi kwa wasojua,
Kesho nitaziongeza, kisha nitawaghania,
Naisifu nchi yangu, nchi yangu Tanzania.



Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Shairi hili linahusu nini?
2. Mwandishi ana maana gani anaposema “Ni bora maumbileye, popote ukitazama”?
3. Mlima Kilimanjaro una sifa gani barani Afrika?
4. Mshairi anasema utamaduni wa Tanzania unazingatia nini?
5. Taja aina nne za madini ambayo mshairi ameyataja kwenye shairi lake.
6. Taja mbuga tatu za wanyama unazozifahamu.
7. Mshairi anasema nchi yake imenuia kufanya nini?
8. Tofauti na mawazo ya mwandishi, wewe unajivunia nini kuhusu nchi ya Tanzania?
9. Unadhani mwandishi wa shairi alikusudia kutoa ujumbe gani?
10. Umejifunza nini kutokana na shairi hilo?

For online use only

Zoezi la pili: Msamiati

Tunga sentensi mbili kwa kila neno.

1. kilele
2. vijito
3. hodhi
4. ghaidhi
5. tumbitumbi
6. wigo
7. sanaa

Zoezi la 3: Mazoezi ya lugha

A. Andika sentensi zifuatazo katika wakati ujao.

Mfano: Mshairi aliandika shairi la kusisimua.

Mshairi ataandika shairi la kusisimua.

Ninawasisitiza wenzangu kusoma kwa bidii.

Nitawasisitiza wenzangu kusoma kwa bidii.

(i) Niliamka asubuhi na kuisifu nchi yangu.

(ii) Niliandika shairi, kisha nikawaghania wenzangu.

(iii) Wanafunzi wanafanya ziara kwenda kutazama Ziwa Tanganyika.

(iv) Mito hupeleka maji baharini na kwenye maziwa.

(v) Vijito hukauka wakati wa kiangazi.

(vi) Umoja wa Afrika hutumia lugha ya Kiswahili.

(vii) Nchi yetu inakuza kilimo ili kuwa na hadhi murua.

(viii) Tulitangaza utajiri wa nchi yetu ya Tanzania.

B. Oanisha maneno yenye maana sawa kutoka kwenye kisanduku kifuatacho:

Mfano: thamini - *jali*

kibwagizo - *kiitikio*

majira	nyanyua	tumaini	sifu	inua	ahirisha
kiitikio	nuia	tegemea	sitiri	ghani	kamilisha
kibwagizo	imba	jali	tosha	maliza	hifadhi
	kusudia	tukuza	wakati	thamini	

For online use only

C. Andika KWELI kwa sentensi yenye mawazo sahihi au SI KWELI kwa sentensi yenye mawazo ambayo si sahihi.

(i) Akili ni nywele kila mtu ana zake.

(ii) Akili si mali.

(iii) Ziwa Nyanza ni miongoni mwa maziwa makubwa Tanzania.

(iv) Akisema mwendawazimu, msikiaji awe na akili.

(v) Mtu asiyesafiri huusifu upishi wa mama yake tu.

(vi) Lugha ya Kiswahili hutumika katika Umoja wa Afrika.

(vii) Mtu anayetaka kujifunza hupaswa kuogopa kuuliza asilolijua.

(viii) Bidii yako ndiyo mafanikio yako.

(ix) Tanzania ni nchi yenye madini ya tanzanaiti, almasi na dhahabu.

(x) Wanafunzi wanapaswa kuchambua mawazo yaliyomo kwenye hadithi.

D. Badili sentensi zifuatazo kuwa katika kauli taarifa

(i) Bibi alisema, “Nitakusimulia hadithi nzuri.”

(ii) Maki aliuliza, “Msimu huu tutapanda mahindi?”

(iii) “Wanakijiji wametunza misitu,” Mwenyekiti alieleza.

(iv) Babu alisema, “Ni vizuri kuheshimu mila na desturi zetu.”

(v) Mama alisema, “Tanzania ni nchi ya amani.”

(vi) “Mtoto yule anapenda kucheza?” Aliuliza mgeni.

(vii) “Vijana wanapaswa kufanya kazi kwa bidii.” Mjomba alisema.

(viii) Kaka alisema, “Mto umejaa maji.”

(ix) Mshangiliaji aliuliza, “Mpira umekwisha?”

(x) “Watoto walishangilia kwa furaha”, Dada alieleza.

E. Andika sentensi zifuatazo kwa usahihi.

(i) Ninaipenda nchi yangu vyenye wingi wa neema.

(ii) Mimi nalipenda kupanda mlima.

(iii) Watanzania ninapaswa kulinda urithi wa nchi yetu.

(iv) Wageni alikuja kutembelea nchi yetu.

(v) Ningalikuwa na uwezo ningenunua madini ya almasi.

For online use only

(vi) Kizo na Kizinga anapenda kutembelea mbuga za wanyama.

(vii) Zitalinda nchi yangu kwa hali na mali.

(viii) Mimi na sisi nitafanya kazi kwa maendeleo ya taifa letu.

(ix) Mtoto wa Kitanzania wanapaswa kuwa mzalendo.

(x) Sisi wote ni ndugu, ninapaswa kudumisha amani.

F. Andika umoja na wingi wa maneno yaliyomo katika jedwali lifuatalo:

Umoja	Wingi
(i) ramani	_____
(ii) kito	_____
(iii) _____	rubi
(iv) mbuga	_____
(v) kijito	_____
(vi) mwinuko	_____
(vii) bonde	_____
(viii) _____	maumbo
(ix) azimio	_____
(x) kilele	_____

G. Imba wimbo huu, kisha chambua mawazo yaliyojitokeza.

Tazama ramani

1. *Tazama ramani utaona nchi nzuri,*
Yenye mito na mabonde mengi ya nafaka,
Nasema kwa kinywa halafu kwa kufikiri,
Nchi hiyo mashuhuri huitwa Tanzania.

Kibwagizo: *Majira yetu haya,*
Yangekuwaje sasa,
Utumwa wa nchi Nyerere ameukomesha.

For online use only

2. *Chemchemi ya furaha amani nipe tumaini,*
Kila mara kwako niwe nikiburudika,
Nakupenda sana hata nitakusitiri,
Nitalalamika kukuacha Tanzania.

Kibwagizo: *Majira yetu haya,*
Yangekuwaje sasa,
Utumwa wa nchi Karume ameukomesha.

3. *Nchi yenye Azimio lenye tumaini,*
Ndiwe peke yako mwanga wa Watanzania,
Ninakuthamini hadharani na moyoni,
Unilinde nami nikulinde hata kufa.

Kibwagizo: *Majira yetu haya,*
Yangekuwaje sasa,
Utumwa wa nchi TANU imeukomesha.



Kazi ya kufanya

Tafuta shairi kutoka maktaba ya shule au vyanzo mbalimbali vya TEHAMA. Soma shairi hilo na chambua mawazo yaliyojitokeza.



Zoezi la 4: Utungaji

Tunga beti mbili za shairi kuhusu shule yako, kisha chambua mawazo yaliyojitokeza katika beti hizo.

For online use only

Sura ya Kumi na Nne

Kueleza mawazo katika matini

Utangulizi

Katika sura hii, utajifunza kueleza mawazo yanayojitokeza katika matini mbalimbali. Utasoma habari kwa makini na kueleza mawazo yaliyomo kwa maneno yako. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kufafanua mawazo yanayojitokeza katika matini mbalimbali kwa mpangilio mzuri na kwa ufasaha.



Fikiri

Namna utakavyofafanua mawazo yanayojitokeza katika matini mbalimbali

Ufahamu

Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.

Chiku anafanya nini kila siku?

Siku moja, mwalimu wetu wa Kiswahili alileta redio darasani. Aliiwasha na kutuambia sote tusikilize. Lengo lake lilikuwa tusikilize mazungumzo kati ya mtangazaji na mshindi wa **shindano** la uandishi wa insha. Mshindi huyo alikuwa mwanafunzi wa Darasa la Tano aitwaye Chiku. Sote tulikaa kimya na kuanza kusikiliza kwa makini mazungumzo hayo.

Mtangazaji: Chiku, hongera sana kwa kushinda shindano la uandishi wa insha!

Chiku: Asante sana ndugu mtangazaji!

Mtangazaji: Jitambulishe kwa watoto wenzako wanaokusikiliza na uwaeleze **ratiba** yako ya kila siku.

Chiku: Kwa jina ninaitwa Chiku Maneno. Ninasoma Darasa la Tano. Huwa ninaamka saa 12:00 asubuhi kila siku.

Mtangazaji: Hebu tueleze, ukishaamka unafanya shughuli gani?

Chiku: Nikiamka, ninaenda kuwasalimu wazazi wangu. Baada ya hapo, ninasafisha chumba changu. Kisha, ninapiga mswaki na kuoga.

For online use only

Mtangazaji: Ahaa! Ni jambo jema sana Chiku kuwasalimu wazazi kabla ya yote. Ukishaoga unafanya nini?

Chiku: Ninavaa nguo za shule na kupata kifunguakinywa, kisha ninaenda shuleni saa 12:45 asubuhi. Nifikapo shuleni, husafisha eneo langu mpaka muda wa kuingia darasani unapowadia.

Mtangazaji: Kumbe shule yenu inazingatia sana usafi! Vipindi huwa vinaanza na kuisha saa ngapi?

Chiku: Vipindi huanza saa 2:00 asubuhi. Hapo, tunakuwa na vipindi vitatu halafu tunapumzika saa 4:00 mpaka saa 4:30 asubuhi.

Mtangazaji: Baada ya mapumziko, huwa mnafanya nini?

Chiku: Tunaingia tena darasani na kusoma vipindi vitatu.Vipindi hivyo hukamilika saa 6:30 mchana halafu tunapumzika kidogo. Tunacheza nje kwa dakika kumi halafu tunaingia tena darasani kusoma mpaka saa 8:00 mchana. Saa 8:00 mpaka saa 8:30 mchana ni muda wa kufanya **shughuli** za usafi wa mazingira.

Mtangazaji: Kwa hiyo, huwa unarudi nyumbani saa ngapi?

Chiku: Huwa tuna**tawanyika** kurudi nyumbani saa 8:40 mchana. Nikifika nyumbani ninakula na kupumzika. Ifikapo saa 12:00 jioni, huwa ninawafungia kuku na mabata bandani.

Mtangazaji: Asante sana Chiku! Je, siku za wikiendi huwa unafanya nini? Unapiga usingizi tu nyumbani?

Chiku: Hapana! Sipendi kupiga usingizi. Siku za wikiendi siendi shuleni. Huwa ninafanya kazi za nyumbani. Mojawapo ya siku za wikiendi kuanzia saa 2:00 mpaka saa 3:00 asubuhi, huwasaidia wazazi shughuli mbalimbali. Shughuli hizo ni kama vile kutunza na ku**mwagilia** bustani ya mbogamboga. Nikitoka bustanini, ninafua **sare** zangu za shule na kujisomea.

Mtangazaji: Je, kuna ugumu wowote katika kufanya shughuli zote hizo kwa utaratibu?

Chiku: Hapana! Kwangu hakuna ugumu wowote.

Mtangazaji: Vizuri sana! Unawezaje kufanya shughuli zako hizo bila kusahau?

Chiku: Mimi hutumia ratiba niliyoiandaa. Ratiba ni muhimu sana kwa kuwa inaniwezesha kufanya mambo kwa utaratibu bila kusahau.

Mtangazaji: Asante sana Chiku! Ninakushauri uendelee na tabia hiyo. Bila shaka, watoto wanaokusikiliza wamejifunza jambo muhimu sana.

For online use only

Mahojiano kati ya Chiku na mtangazaji yalitukosha mioyo sana. Baada ya mahojiano kuisha, mwalimu wetu akazima redio. Alituuliza maswali kadha wa kadha na kututaka tuandike insha kuhusu shughuli za kila siku. Mwisho, akatu**usia** tuwe na tabia ya kujitengenezea ratiba. Ratiba ni muhimu kwa sababu hutuongoza katika shughuli zetu za nyumbani na shuleni. Sote tuliahidi kuiga mfano wa Chiku.

Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Kwa nini mwalimu alileta redio darasani?
2. Nani alikuwa anahojiwa na mtangazaji?
3. Chiku huamka saa ngapi kila siku?
4. Wanafunzi hufanya nini shuleni kuanzia saa 6:30 mpaka 6:40 mchana?
5. Ratiba ya vipindi katika shule anayosoma Chiku humalizika saa ngapi?
6. Kwa nini ni muhimu kufuata ratiba?
7. Chiku hufanya shughuli gani siku mojawapo ya wikiendi kuanzia saa 2:00 mpaka 3:00 asubuhi?
8. Kama ungepewa nafasi ya kumuuliza Chiku swali moja kuhusu ratiba yake, ungemuuliza nini na kwa nini?
9. Kama ungekuwa Chiku, ungeboresha vipi ratiba yako ya kila siku?
10. Umejifunza nini kutokana na habari ya Chiku?

Zoezi la pili: Msamiati

Tunga sentensi moja kwa kila neno.

1. shindano
2. ratiba
3. shughuli
4. tawanyika
5. mwagilia
6. sare
7. usia

Zoezi la 3: Nahau na misemo

Eleza maana ya nahau na misemo ifuatayo, kisha tunga sentensi moja kwa kila nahau na msemo.

Mfano: pasha moto – *fanya kuwa moto*

Hakupenda chakula cha baridi; hivyo, alikiweka jikoni kukipasha moto.

Mikono mitupu- *bila ya chochote*

Alienda kwa mjomba wake mikono mitupu, lakini alirudi na zawadi nyingi.

For Online Use Only

1. piga usingizi
2. kosha moyo
3. tia pingu
4. piga mwayo
5. nyoosha miguu
6. tega sikio
7. piga foleni
8. tia pamba masikioni
9. dhahiri shahiri
10. fanya vitimbi

Zoezi la 4: Methali

Chagua jibu sahihi linaloeleza maana ya methali zifuatazo kwa kuandika herufi ya jibu hilo katika kisanduku ulichopewa.

1. Hakuna marefu yasiyo na ncha.
   (a) Hakuna jambo lenye mwanzo mrefu.
   (b) Hakuna jambo lisilokuwa na mwisho.
   (c) Hakuna kitu kisicho kirefu.
   (d) Hakuna ncha isiyokuwa na marefu.
   (e) Hakuna jambo lisilokuwa na ncha.

2. Maji ukiyavulia nguo, huna budi kuyaoga.
   (a) Ukianza kufanya jambo, ni lazima ulimalize.
   (b) Maji ni muhimu kwa maisha ya binadamu.
   (c) Nguo zikichafuka, lazima zisafishwe.
   (d) Ukianza kuvua nguo ni lazima uoge.
   (e) Maji ukiyachota lazima uyaoge.

3. Ahadi ni deni.
   (a) Mtu asipopata deni, hawezi kutoa ahadi.
   (b) Ahadi inaweza kusahaulika kabisa.
   (c) Ukimuahidi mtu kitu chochote huna budi kutimiza.
   (d) Mtu asipojua deni hawezi kutoa ahadi.
   (e) Mtu asipoahidi hawezi kujua deni.

For online use only

4. Mkono utoao ndio upokeao.

   (a) Mtu anayesaidia wengine hutoka moyoni.

   (b) Mtu anayesaidia wengine ni mkarimu.

   (c) Mtu anayesaidia wengine kamwe hachoki.

   (d) Mtu anayesaidia wengine naye husaidiwa.

   (e) Mtu anayesaidia wengine hana uhitaji.

5. Ndo ndo ndo hujaza ndoo.

   (a) Kidogokidogo ndoo hujaa maji.

   (b) Kidogokidogo maji hujaa na kuanza kumwagika.

   (c) Kujaza maji katika ndoo ni kuyatunza.

   (d) Kujaza maji katika ndoo taratibu.

   (e) Kidogokidogo mwisho jambo hukamilika.

Zoezi la 5: Mazoezi ya lugha

A. Andika sentensi zifuatazo katika wakati ujao.

Mfano: Tunaandika insha kuhusu ratiba ya siku.

Tutaandika insha kuhusu ratiba ya siku.

Mkiwa alishinda shindano la uandishi wa insha.

Mkiwa atashinda shindano la uandishi wa insha.

(i) Chiku alihojiwa na mtangazaji wa redio.

(ii) Mwalimu amekuja na redio darasani.

(iii) Yeye humwagilia bustani siku ya Jumamosi.

(iv) Wanafunzi hupumzika saa 4:00 asubuhi.

(v) Kila mmoja wetu aliandaa ratiba yake ya wiki nzima.

(vi) Ninawasindikiza wazazi wangu asubuhi.

(vii) Wanafunzi walifanya ziara ya mafunzo katika kiwanda cha nguo.

(viii) Serikali imejenga barabara mpya katika wilaya yetu.

For online use only

(ix) Mdogo wangu anamaliza masomo yake mwaka huu.

(x) Watalii wengi wanatembelea pwani ya Zanzibar.

B. Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuchagua neno sahihi kutoka kwenye mabano.

(i) Kaka na dada _____ gari la baba kila wikiendi.
(husafisha, safisha, amesafisha)

(ii) Unaweza kusafiri kwa basi _____ kwa treni.
(hivyo, au, lakini)

(iii) Watoto wanapenda _____ michezo shuleni.
(cheza, kucheza, hucheza)

(iv) Mwalimu aliwaambia wanafunzi _____ kwa bidii.
(soma, wasome, anasoma)

(v) Chakula _____ mezani na hakijaliwa.
(ipo, kipo, lipo)

(vi) Tulichelewa kufika shuleni _____ mvua ilinyesha asubuhi.
(lakini, hivyo, kwa sababu)

(vii) Wanafunzi _____ shuleni Jumatatu hadi Ijumaa.
(enda, huenda, kwenda)

(viii) Tulifanya mazoezi _____ tukaenda nyumbani kupumzika.
(au, kisha, bali)

(ix) Wanafunzi wale walisoma kwa bidii _____ wamefaulu mtihani.
(hivyo, bali, lakini)

(x) Mwanariadha anakimbia _____ kwa kasi kubwa uwanjani.
(ngao, mbio, medali)

C. Bainisha majina katika sentensi zifuatazo:

Mfano: Ndege anajenga kiota juu ya mti.

Majina: *ndege, kiota na mti*

Urafiki wa Esta na Nduna ni wa muda mrefu.

Majina: *urafiki, Esta, Nduna* na *muda*

(i) Mgeni alituletea zawadi nyingi.

FOR online use only

(ii) Mpishi alitayarisha chakula cha mchana.

(iii) Daktari alimshauri mgonjwa apumzike nyumbani.

(iv) Kijana amekamilisha kusafisha nyumba.

(v) Kilimo ni muhimu kwa maendeleo ya Tanzania.

(vi) Fundi alikarabati daraja lililovunjika Kinondoni.

(vii) Shangazi anaishi Lushoto na familia yake.

(viii) Askari walimkamata mwizi sokoni.

(ix) Uvumilivu huleta mafanikio katika maisha.

(x) Kinyonga hutembea polepole ili kujificha dhidi ya maadui.

D. Panga maneno yafuatayo ili kupata sentensi sahihi.

Mfano:

jana mgeni nyumbani alifika mchana

Mgeni alifika nyumbani jana mchana.

barabarani askari magari aliyasimamisha

Askari aliyasimamisha magari barabarani.

(i) mbwa usiku kwa sauti alibweka

(ii) mkulima shambani mazao anavuna

(iii) wazazi jioni walirejea nyumbani

(iv) mchoraji ramani nzuri alichora

(v) nyumbani wageni asubuhi jana walifika

(vi) mabichi Sungura majani alikula

(vii) maziwa dukani alinunua dada

(viii) mjomba mwavuli aliniletea mkubwa

(ix) anatafuta mwanafunzi mtandaoni maarifa

(x) baharini mvuvi samaki alivua

E. Panga sentensi zifuatazo katika mtiririko sahihi.

(i) Alijua kuwa alishindwa mtihani kwa sababu hakufanya maandalizi ya kutosha.

(ii) Baada ya kujua alijizatiti na kufanya mazoezi kwa bidii ili kufaulu mtihani ujao.

For online use only

(iii) Alielewa kuwa kujitahidi ni muhimu ili kufikia malengo.

(iv) Alijisikia huzuni na alijilaumu kwa kushindwa kufaulu mtihani.

(v) Alipofanya mtihani mwingine, alifaulu kwa alama nzuri.

F. Andika ratiba ya siku ya Jumatano kuhusu shughuli unazozifanya nyumbani na shuleni kuanzia asubuhi unapoamka mpaka usiku unapoenda kulala.

G. Jaza sehemu zilizoachwa wazi katika ratiba ifuatayo kwa kuzingatia maelezo ya Chiku.

Siku	**Muda**	**Shughuli**
Jumatatu	Saa 4:00 asubuhi - saa 4:30 asubuhi	(i) .....
Jumanne	(ii) Saa	Kutawanyika kutoka shuleni
Jumatano	(iii) Saa.....	Kufungia kuku na mabata bandani
Alhamisi	Saa 2:00 asubuhi	(iv) .....
Ijumaa	Saa 6:30 mchana - saa 6:40 mchana	(v) .....
Wikiendi	(vi) Saa	Kufua sare za shule

Kazi ya kufanya

Soma habari unayoipenda kutoka kwenye vitabu au magazeti, kisha fafanua kwa mdomo mbele ya darasa mawazo yaliyomo kwenye habari hiyo. Hakikisha unaeleza kwa mpangilio mzuri mawazo hayo ili kujibu maswali yatakayoulizwa na wanafunzi wenzako au mwalimu.

For online use only

Zoezi la 6: Utungaji

Chunguza picha zifuatazo kuhusu matukio ya Adamu kwa siku za wikiendi. Kisha, tunga habari yenye maneno kati ya themanini (80) na mia moja (100) kuhusu matukio hayo na eleza kwa ufupi mawazo yaliyojitokeza.













For online use only

Sura ya Kumi na Tano

Kufupisha habari

Utangulizi

Katika sura hii, utajifunza kufupisha habari bila kupotosha ujumbe uliokusudiwa. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuwasilisha hoja kwa ufupi kwa njia ya maandishi kulingana na muktadha.



Fikiri

Namna unavyoweza kuandika upya aya ndefu kwa maneno machache bila kupoteza ujumbe uliokusudiwa

Ufahamu

Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.

Yai au kuku

Ilikuwa alasiri yenye upepo mwanana katika Shule ya Msingi Mwangaza. Wanafunzi wa Darasa la Tano walikuwa wakisubiri kwa hamu kipindi cha somo la Kiswahili. Mlango ulifunguliwa; Mwalimu Matola akaingia darasani akiwa na tabasamu pana. “Leo tuna swali moja la kutafakarisha na la kufurahisha,” alisema kwa sauti tulivu yenye msisimko. **“Kati ya yai na kuku, ni kipi kilianza?”** Swali hilo liliwatafakarisha wanafunzi wote darasani na kila mwanafunzi alinyoosha mkono kujaribu kutoa jibu lake. **“Ni kuku!”** mmoja alisema kwa kujiamini. **“Hapana! Ni yai,”** mwingine akasisitiza huku akitikisa kichwa.

Mjadala ulinoga, sauti zikazidi kupanda, kila mmoja akitetea hoja yake kwa ari kubwa. Mwalimu Matola aliwasikiliza na kuwapa muda wa kueleza mawazo yao. Alipoona mjadala unazidi kupamba moto, aliinua mkono wake na kusema kwa upole, “Nyamazeni kidogo.” Darasa likatulia mara moja. “Ninaona swali hili limewachangamsha sana! Ninataka mjue kuwa si ninyi tu mnaojiuliza kuhusu kitendawili hiki. Hata waandishi wa vitabu wamewahi kulijadili kwa kina. Badala ya kubishana, hebu sasa fungueni vitabu vyenu vya Kiswahili, ukurasa wa 128, tusome shairi linalohusu mjadala kati ya yai na kuku.” Wanafunzi walifungua vitabu vyao haraka, wakiwa na shauku kubwa. Macho yao yakatua kwenye maandishi ya shairi hilo, tayari kulisoma na kutafakari utata uliopo kuhusu kilichotangulia kati ya kuku na yai.

use only
For Online

Yai au kuku

1. *Inashangaza dunia, kwa hiki kitendawili,*
   Yupi mwanzo kutokea, kuku yai ndilo swali,
   Sote yai twalijua, suraye na yake hali,
   Nani atutegulie, kitendawili cha ***jadi****?*

2. *Kuku fundi ku****pekua****, ardhi na jalalani,*
   Je, ndiye katangulia, kuja hapa duniani?
   *Huenda li****ibukia****, akiwa* ***tembe*** *yakini,*
   Nani atutegulie, kitendawili cha jadi?

3. *Kuku, Yai wazozana, kila mmoja asema,*
   Ni wa mwanzo kutokeza, Yai asema ni mama,
   Nuru yake yapendeza, tena mleta uzima,
   Nani atutegulie, kitendawili cha jadi?

4. *“Bila mimi hupo Kuku, ni mimi nimekuzaa,*
   *Kuku huwezi ni****piku****, hata kama ’me****komaa****,*
   Tangu zama za masiku, duniani nimekaa,”
   Nani atutegulie, kitendawili cha jadi?

5. *Kuku naye akasema, “E’ Yai acha mikogo,*
   *Umepata’pi uzima? Punguza yako ma****zogo****,*
   Mimi ndiye wako mama, tangu ukiwa mdogo,”
   Nani atutegulie, kitendawili cha jadi?

6. *“Kweli Yai umekwama, kwa fikira za dharau,*
   Akilizo zimehama, umejijaza sahau,
   Nakukumbusha heshima, wazazi usidharau,”
   Nani atutegulie, kitendawili cha jadi?

For online use only

7. *Yai, Kuku kwa maringo, wajidai hadharani,*
*Nani katika **miongo**, aliwahi duniani?*
*Nauliza wenye **bongo**, mliomo darasani,*
Nani atutegulie, kitendawili cha jadi?

8. ***Chapuchapu** lete jibu, nazo sababu nipeni,*
*Tuimalize **sulubu**, nyoyo ziwe na amani,*
Tuwaondolee tabu, Yai, Kuku mzozoni,
Nani atutegulie, kitendawili cha jadi?

9. *Ikiwa ni huyu Kuku, tueleze chanzo chake,*
Ikawaje aje huku, mpekua kwa mateke,
Kama wa mwanzo ni Kuku, tuikiri rai yake,
Nani atutegulie, kitendawili cha jadi?

10. *La, kama Yai kawahi, ni wapi alitokea?*
Mpime nawanasihi, kwa haki kesi amua,
Amua kwa usahihi, bila ya kuwaonea,
Nani atutegulie, kitendawili cha jadi?

Baada ya kusoma shairi hilo lenye mvutano mkali kati ya Kuku na Yai, darasa lote lilitulia. Kila mwanafunzi alizama katika tafakuri, akitafakari kwa kina juu ya swali hilo. Bado lilisalia kuwa kitendawili tata. Hakuna aliyekuwa na jibu la uhakika. Hata hivyo, mjadala huo uliwafurahisha na kuwaamsha fikra. Walifurahia kusikiliza hoja mbalimbali na kushiriki katika kutafakari maswali yasiyo na majibu rahisi. Mwalimu Matola alitabasamu kisha akasema kwa upole, “Si kila swali lina jibu la haraka. Muhimu ni kujifunza kufikiri kwa makini, kuchambua hoja na kuelewa mitazamo tofauti.” Wanafunzi walitazamana wakitabasamu, wakatambua kuwa maarifa ni safari isiyo na mwisho. Kabla ya kipindi kuisha, Mwalimu Matola akaongeza, “Swali hili bado halina jibu bayana. Hata hivyo, msijali, mtakapofika darasa la sita, mtajifunza zaidi na huenda mkapata jibu juu ya kitendawili hiki.” Walipotoka darasani, mazungumzo yao yaliendelea kwa furaha, wakijua kuwa kila mjadala huleta maarifa mapya.

For online use only

Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Habari uliyoisoma inahusu nini?
2. Katika ubeti wa tatu, Kuku na Yai wanabishania nini?
3. Yai anasema nini katika ubeti wa nne?
4. Ubeti wa tano unazungumzia nini?
5. Kuku alifurahi kusikia maneno ya Yai? Kwa nini?
6. Kuku anaposema, “Nakukumbusha heshima, wazazi usidharau” ana maana gani?
7. Katika ubeti wa tisa, mshairi ana maana gani anaposema Kuku ni “mpekua kwa mateke”?
8. Katika ubeti wa kumi, mshairi anawaambia nini wanafunzi?
9. Unadhani “kitendawili” katika shairi kitateguliwa? Toa sababu ya jibu lako.
10. Kama ungepewa nafasi ya kutoa uamuzi, ungefanya uamuzi gani kuhusu Yai na Kuku? Eleza sababu zako.

Zoezi la pili: Msamiati

Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:

1. jadi
2. pekua
3. ibukia
4. tembe
5. piku
6. komaa
7. zogo
8. miongo
9. bongo
10. chapuchapu
11. sulubu

Zoezi la 3: Methali

Kamilisha methali zifuatazo:

Mfano: Usiku mmoja ……..

Usiku mmoja <u>hauozeshi nyama.</u>

Heri jirani karibu ……

Heri jirani karibu <u>kuliko ndugu mbali.</u>

For Online use Only

1. Kuku havunji, ...
2. Teke la kuku, ...
3. Kuku mgeni, ...
4. Mwana wa kuku, ...
5. Damu nzito, ...
6. Mwenye shibe, ...
7. Ukupigao, ...
8. Uvivu, ...
9. Atangae sana na jua, ...
10. Elimu bila adili, ...

Zoezi la 4: Mazoezi ya lugha

A. Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi ya jibu hilo katika kisanduku.

(i) Idadi ya silabi katika mstari mmoja wa shairi huitwa _____

(a) Mshororo
(b) vina
(c) urari
(d) mizani

(ii) Kila mshororo katika shairi hili una mizani ngapi?

(a) Minne
(b) Nane
(c) Kumi na sita
(d) Kumi

(iii) Vina vya katikati na mwishoni katika ubeti wa tano ni _____.

(a) **ma** na **go**
(b) **go** na **e**
(c) **go** na **di**
(d) **go** na **ku**

For online use only

(iv) Kina cha katikati katika ubeti wa kwanza ni kipi?

(a) **a na e**

(b) **a**

(c) **a** na **di**

(d) **li**

(v) Katika shairi, mshororo ni nini?

(a) aya ya shairi

(b) mstari wa mwisho katika ubeti wa shairi

(c) mstari kwenye ubeti

(d) idadi ya mistari yote katika shairi

(vi) Shairi hili lina beti ngapi?

(a) Nne

(b) Kumi

(c) Kumi na sita

(d) Sita

(vii) Kituo katika shairi hili ni kipi?

(a) Nani atutegulie, kitendawili cha jadi?

(b) Amua kwa usahihi, bila ya kuwaonea,

(c) Tuimalize sulubu, nyoyo ziwe na amani,

(d) Nani katika miongo, aliwahi duniani?

(viii) Ni beti zipi katika shairi la “Yai au kuku?” zinafanana vina vyake vya kati?

(a) 6 na 7

(b) 4 na 5

(c) 3 na 4

(d) 5 na 6

FOR online use only

B. Andika kirefu cha maneno haya kulingana na yalivyotumika katika shairi.

(i) suraye _____

(ii) liibukia _____

(iii) umepatapi _____

(iv) akilizo _____

C. Andika kwa kifupi maneno yafuatayo:

Mfano: mfano wake - *mfanowe*

mwisho wake - *mwishowe*

(i) mpwa wake _____

(ii) habari yake _____

(iii) mama yake _____

(iv) Sanduku la Posta _____

(v) ndugu zako _____

(vi) kaka yake _____

(vii) mwana wake _____

(viii) dada yake _____

(ix) Baraza la Kiswahili Tanzania _____

(x) binamu yako _____

D. Andika neno lenye maana sawa na maneno yafuatayo:

Mfano: maringo – *madaha*

pochi – *mkoba*

(i) piku

(ii) dharau

(iii) pendeza

(iv) tangulia

(v) uzima

(vi) shindwa

(vii) idhini

(viii) kauli

For Online use only

E. Chagua jibu sahihi, kisha andika herufi yake katika kisanduku

(i) Nini maana ya kufupisha habari?

(a) Kuongeza maelezo kwenye habari
(b) Kupunguza maneno bila kupoteza ujumbe
(c) Kuandika habari kwa lugha ngumu
(d) Kuongeza aya katika habari
(e) Kupunguza alama za uandishi kwenye habari

(ii) Kwa nini ni muhimu kufupisha habari?

(a) Ili ieleweke kwa urahisi
(b) Ili kuongeza maneno kwenye habari
(c) Ili kufanya habari iwe ndefu zaidi
(d) Ili kutomvutia msomaji wa habari
(e) Ili kufanya habari iwe fupi na kupoteza maana

(iii) Hatua ya kwanza ya kufupisha habari ni ipi?

(a) Kupunguza sentensi kwa haraka
(b) Kuandika maelezo mengi zaidi
(c) Kusoma habari kwa makini
(d) Kuhesabu maneno kwa haraka
(e) Kuangalia alama za uandishi zilizotumika

(iv) Ufupisho wa habari unapaswa kuwa na sifa gani muhimu?

(a) Uwe mfupi na ueleweke
(b) Unapaswa kuwa na maneno magumu
(c) Uwe mrefu na wenye maelezo mengi
(d) Usihusianishe umri na mazingira
(e) Upotoshe maana ya msingi

(v) Ipi siyo njia sahihi ya kufupisha habari?

(a) Kuondoa maelezo yasiyo ya msingi
(b) Kutunga habari mpya fupi
(c) Kutumia maneno machache lakini yenye maana
(d) Kueleza ujumbe wa msingi kwa ufupi
(e) Kueleza ujumbe kwa ufupi wenye maana iliyokusudiwa

For online use only

(vi) Kipengele gani ni muhimu katika ufupisho wa habari?

(a) Kuhifadhi ujumbe wa msingi
(b) Kurefusha sentensi
(c) kutumia maneno magumu
(d) Kichwa cha habari
(e) Kurefusha aya

(vii) Jambo gani linafaa kuzingatiwa unapofupisha habari?

(a) Kuongeza maelezo yasiyo ya lazima
(b) Kupunguza sentensi hadi iwe na neno moja
(c) Kuhakikisha ujumbe wa habari haubadiliki
(d) Ukate sehemu za msingi za habari
(e) Kubadilisha muktadha ili kupata maneno machache

(viii) “Mwalimu wetu alituambia tusome vitabu vyetu kila siku baada ya masomo.” Ufupisho sahihi wa sentensi hii ni upi?

(a) Mwalimu alisema tusome vitabu kila siku.
(b) Mwalimu alituambia tusome vitabu.
(c) Mwalimu alisema tusome kila siku baada ya masomo.
(d) Mwalimu alisema tusome vitabu vyetu baada ya masomo.
(e) Mwalimu alisema kuwa tusome vitabu vyetu.

(ix) “Wanafunzi wa Shule ya Msingi Mlimani walifanya usafi katika mazingira ya shule yao ili kuifanya iwe safi na ya kupendeza.” Ufupisho sahihi wa sentensi hii ni upi?

(a) Wanafunzi wa Mlimani walifanya usafi shuleni.
(b) Wanafunzi walifanya usafi siku nzima.
(c) Shule ilikuwa chafu kwa muda mrefu.
(d) Shule ilitakiwa mazingira yake yapendeze.
(e) Wanafunzi walifanya usafi na kupendezesha.

For Online use only

(x) Lengo kuu la kufupisha habari ni lipi?

(a) Kurefusha maelezo ya habari kwa kuandika maana mpya.
(b) Kupunguza maelezo ili kueleweka kwa urahisi.
(c) Kuandika habari kwa njia tofauti kabisa.
(d) Kupunguza maelezo kwa kuchagua maana za ziada.
(e) Kurefusha maelezo ya habari kupata maana.

F. Ondoa silabi moja katika maneno uliyopewa ili kupata maneno mapya.

Mfano: kilele – *kile, lele*

mawili - *mali*

(i)	mengine	(vi)	ufuta
(ii)	kupata	(vii)	kisima
(iii)	mchanga	(viii)	utepe
(iv)	kipimo	(ix)	machimbo
(v)	viatu	(x)	barafu

Kazi ya kufanya

Soma au sikiliza wimbo wa Tanzania Tanzania na wimbo wa shule yako, kisha fupisha kazi hizo kwa maneno kati ya thelathini hadi hamsini (30 – 50).

Zoezi la 5: Utungaji

A. Fupisha habari ifuatayo kwa maneno kati ya arobaini na hamsini (40 - 50).

Mwalimu wetu anaitwa Mgeni. Anafundisha Somo la Kiswahili. Wakati wa likizo alisafiri kwenda Mtinko - Singida. Sisi pia tulisafiri pamoja na wazazi wetu kwenda sehemu mbalimbali. Tulienda kuwasalimia ndugu na jamaa zetu.

Likizo ilipokwisha, wote tulirudi shuleni kuendelea na masomo. Walimu wa masomo mengine waliingia darasani isipokuwa Mwalimu Mgeni. Hali hiyo ilitushangaza sana kwani Mwalimu Mgeni hakuwa na tabia ya kutoingia darasani. Tulitamani

For online use only

kujua alipo mwalimu wetu wa Kiswahili, lakini hatukujua tumuulize nani. Baada ya wiki mbili Mwalimu Mgeni alikuja shuleni. Looh! Ilikuwa furaha kubwa kwetu. Tulishangilia sana.

Baada ya kutulia, Mwalimu Mgeni alitueleza kuwa, alipokuwa likizo alipata dharura ya kifamilia. Hivyo, alilazimika kukaa huko kwa muda zaidi ili kushughulikia dharura hiyo. Mwalimu Mgeni alitueleza kuwa, kutokana na hali hiyo, ilimlazimu kumwandikia barua Mwalimu Mkuu ili kuomba siku zaidi za kuwa huko. Baada ya maelezo ya Mwalimu Mgeni, wote tulimpa pole kwa kadhia hiyo. Baada ya hapo, Mwalimu Mgeni aliendelea na kufundisha ambapo alitufundisha kuhusu uandishi wa barua ya kiofisi.

B. Fupisha habari ya Yai au kuku kwa maneno kati ya hamsini hadi sitini (50 - 60).

For online use only

Sura ya Kumi na Sita

Kutunga maigizo

Utangulizi

Katika sura hii, utajifunza kutunga maigizo rahisi na mafupi kwa kuzingatia kanuni. Pia, utaeleza wazo kuu na fundisho linalopatikana katika igizo. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kutumia stadi za awali za ubunifu katika sanaa ya uigizaji.



Fikiri

Uzuri wa igizo ulilowahi kuangalia

Ufahamu

Soma igizo lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.

Maskini Tukutu!



For online use only

Sauti ilisikika ikituarifu kuwa **igizo** linaanza. Watu wote walikuwa kimya kabisa. Mara pazia lilifunguliwa. Wahusika wote wa igizo hilo walionekana jukwaani wakiwa wameganda kwa mitindo tofautitofauti. Watazamaji wakapiga kelele za shangwe kwa walichoona.

Kiongozi: Igizo letu linahusu mtoto mtukutu aitwaye Tukutu. Tukutu hawasikilizi wazazi na walimu wake na hata wanafunzi wenzake. Nini kitatokea? Tusimalize utamu. Tujionee wenyewe.

Waigizaji Wote: Tunawakaribisha nyote kujionea mambo mazuri tuliyoandaa. Karibuni sana! (*Wote wanajitambulisha uhusika wao na pazia linafungwa.*)

Watazamaji: (*Wote wanapiga makofi, vigelegele na **mbinja**. Muda huohuo pazia linafunguliwa.*)

Mama: Tukutu! Tukutu! Amka uende shule.

Tukutu: Aaa! Mama! Mambo gani hayo? Mbona unaniharibia usingizi?

Mama: Mwanangu, mbona siku hizi umebadilika? Tabia yako imekuwa ya ajabu!

Tukutu: Mama, nitaenda shuleni baadaye.

Mama: Wewe! Unasemaje? Haya, amka haraka uoge, unywe chai, uende shule. (*Tukutu anakubali kuamka. Anaenda kuoga, anakunywa chai na kuondoka kwenda shuleni.)*

Mwalimu: Tukutu, kwa nini umechelewa?

Tukutu: Mwalimu, nilikuwa ninaumwa tumbo.

Mwalimu: Haya! Ingia darasani haraka; kisha, andika maswali yaliyopo ubaoni. Ni ya somo nililowafundisha jana.

Tukutu: Mwalimu, mimi sina kalamu. Siwezi kuandika kwa sababu sioni ubaoni. (*Tukutu anatoa sababu nyingi.*)

Mwalimu: Haya! Kalamu hii hapa. Sasa ninataka ujibu maswali katika daftari lako. (*Anaondoka. Tukutu anabaki akiwasumbua wenzake darasani*.)

Tukutu: Kisa, ninataka unijibie maswali yote. Usipofanya hivyo, nitakupiga.

For online use only

Kisa: Jibu mwenyewe. Siwezi kukujibia. (*Tukutu anafanya fujo darasani; anawa**nyang'anya** wenzake madaftari ili anakili majibu. Wenzake wanakataa. Yeye anaanza kuwapiga.*)

Masikitiko: (*Akielekea ofisi ya walimu kwa huzuni kutoa taarifa kwa mwalimu.*) Mwalimu, Tukutu anatusumbua darasani. Anatupiga na kutunyang'anya madaftari.

Mwalimu: (*Anaingia darasani.*) Tukutu njoo ofisini haraka. (*Tukutu anamfuata mwalimu.)* (*Mwalimu anamfokea Tukutu.*) Tukutu una nini wewe? Kwa nini unawasumbua wenzako darasani?

Tukutu: (*Akirusha mikono.)* Mwalimu, mimi sitaki kusoma.

Mwalimu: Nenda nyumbani kamwite mzazi wako. (*Tukutu anarudi nyumbani. Njiani anakutana na rafiki yake Kiduku.*)

Kiduku: Aaa! Tukutu unaenda wapi? Twende huku ukatulize akili.

Tukutu: Sasa rafiki yangu Kiduku, unataka twende wapi?

Kiduku: Twende nikupeleke sehemu moja ukafurahie maisha.

Tukutu: (*Anakubali na kumfuata Kiduku*.) Sehemu hiyo ina nini cha kunifurahisha?

Kiduku: Wewe fuata nyuki ule asali; utafurahi tu. (*Wote wanacheka, haa! Haa! Haa! Wanafika uchochoroni sehemu iliyojificha ambayo Kiduku hukutania na vibaka wenzake.*)

Tukutu: Hapa umepajuaje? Mbona panatisha?

Kiduku: (*Anam**kwida** na kutaka kumnyang'anya begi la shule*.) Sasa uko hatarini, kwa usalama wako toa ulicho nacho. (*Tukutu analing'ang'ania begi lake. Kiduku anapatwa na hasira na kumpiga mateke na vichwa. Tukutu anaanguka chini. Kiduku anachukua begi, anatupa madaftari chini na anaondoka nalo. Tukutu anabaki amelala pale chini. Wanafunzi wakiwa wanarudi nyumbani, njiani wanakutana na mbwa mkali; anawafukuza. Wanakimbilia pande tofautitofauti. Mmoja wao, ambaye ni Shauri, anajikuta kwenye kichochoro ambako Tukutu ameachwa*.)

Shauri: (*Anashituka na kuanza kuita kwa sauti*.) Tukutu! Tukutu! Umefanya nini? Amka!

For online use only

Tukutu: (Akiinuka.) Loo! Kiduku amenipiga na kuninyang'anya begi. Ama kweli usilolijua ni kama usiku wa giza!

Shauri: Twende upesi nikupeleke nyumbani. Hapa si mahali salama kabisa. (*Wanaondoka wote kwenda nyumbani, huku Tukutu akichechemea na uso wote ukiwa umevimba.*)

Shauri: Rafiki yangu Tukutu, umekuwa m**kaidi** sana. Humsikilizi mama yako, walimu na hata wanafunzi wenzako. Hii tabia yako italeta madhara katika masomo yako na maisha yako kwa ujumla. Kuanzia sasa, anza kusoma kwa bidii kama mimi. Watu watakupenda.

Tukutu: Asante sana kwa ushauri wako. Nitaomba msamaha kwa mama, walimu, Kisa na wanafunzi wote niliowakosea. Ama kweli akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki wa kweli. (*Pazia linafungwa na watu wanapiga makofi na vigelegele.*)

Zoezi la kwanza: Ufahamu

1. Igizo hili linahusu nini?
2. Tukutu alikuwa na tabia gani?
3. Unafikiri kwa nini pazia hufunguliwa na kufungwa katika onesho la igizo?
4. Eleza kazi ya maneno yaliyomo kwenye mabano katika igizo?
5. Kama wewe ungekutana na Kiduku, ungemwambia nini?
6. Majina ya wahusika gani yanaendana na matendo yao? Kwa nini?
7. Katika igizo hili, ungependa kuwa kama nani? Kwa nini?
8. Taja tofauti kati ya igizo na hadithi?
9. Mwandishi amezingatia mambo gani katika utunzi wa igizo hili?
10. Igizo hili linatufundisha nini?

Zoezi la pili: Msamiati

Tunga sentensi kwa kila neno.

1. igizo
2. mtukutu
3. mbinja
4. nyang'anya
5. kwida
6. kaidi

For online use only

Zoezi la 3: Methali

Andika maana za methali zifuatazo:

1. Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki wa kweli.
2. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.
3. Kawaida ni kama sheria.
4. Mtoto mwerevu hafunzwi adabu.
5. Usiandikie mate, na wino ungalipo.

Zoezi la 4: Mazoezi ya lugha

A. Andika maneno yenye maana sawa na maneno yafuatayo:

(i) kelele _____

(ii) ondoka _____

(iii) mbinja _____

(iv) mtukutu _____

(v) lukuki _____

(vi) nyang'anya _____

(vii) kwida _____

B. Andika wingi wa sentensi zifuatazo:

Mfano: Chura anafurahia maji bwawani.

Vyura wanafurahia maji mabwawani.

Kijana aliitafuna korosho yote bila woga.

Vijana walizitafuna korosho zote bila woga.

(i) Mwanafunzi hodari alifaulu vizuri masomo yake.

(ii) Mimi nilienda kumwona simba katika mbunga ya wanyama ya Manyara.

(iii) Ulimpokea mgeni wako kwa shangwe.

(iv) Sikuamini kama timu yetu ingefungwa magoli mengi.

(v) Wewe unajivunia nini?

(vi) Dada, fungua dirisha njiwa aingie ndani.

FOR online use only

(vii) Wewe umekuwa bingwa katika mieleka.

(viii) Ngoja nimalizie hili ninalofanya sasa.

(ix) Wewe umeeleza wazo lako kwa uwazi.

(x) Unapaswa kuhakikisha choo kinakuwa safi muda wote.

C. Tunga sentensi kumi na tano (15) kutokana na jedwali lifuatalo:

Wiki ijayo			
Kila siku	tulicheza mpira wa miguu		bibi
Jana	tutaenda likizo	kwa	kuingia darasani
Leo	tunaimba wimbo wa taifa	kabla ya	Pugu
Kesho	tutatembelea stesheni ya reli ya kati	ya	uwanjani
Mwaka jana			

D. Badili sentensi zifuatazo kuwa katika kauli taarifa.

Mfano: "Simulia hadithi," Baraka aliniambia.

Baraka aliniambia nisimulie hadithi.

(i) "Fungeni chandarua ili msipatwe na Malaria," Bwana Afya alisema.

(ii) Mwalimu alisema, "Wanafunzi ni lazima mfuate ratiba ya shule."

(iii) Dada alituambia, "Kuleni chakula bora ili muwe na afya njema."

(iv) "Nimechoka," babu alilalamika.

(v) "Je, umemwona Halima?" Kiroboto aliniuliza.

(vi) "Kumbe hamwogopi upupu!" Mwalimu alishangaa.

(vii) "Kila mmoja awepo kwenye mkutano," kiongozi aliagiza.

(viii) "Yamenikuta," Juma alikiri.

For online use only

E. Jaza fumbo lifuatalo kwa kutumia maelekezo ya kwenda chini na kulia



Kwenda chini

1. Kifaa kinachotumika kulalia (7)
2. Kifaa kinachotumika kuandikia (6)
4. Mahali panapohifadhiwa vitabu na ambapo watu hujisomea (7)

Kwenda kulia

2. Kazi ya maandishi iliyochapwa yenye kurasa na kugundishwa pamoja na kuwekewa jalada (6)
3. Silabi zinazolingana kati na mwishoni mwa mstari wa shairi (4)
5. Chumba au mahali wanaposomea wanafunzi (6)
6. Kipande cha mti chembamba upande wa mshikio na bapa upande mwingine kinachotumika hasa kwa kusongea (5)

For online use only

F. Igiza matendo yafuatayo:

(i) kurupuka

(ii) tetemeka

(iii) cheka

(iv) koroga

(v) punga

(vi) nyata

(vii) furahia

(viii) kasirika

(ix) fikiri

(x) kwepa

G. Unda maneno mapya yanayoanza na maneno yafuatayo:

Mfano: mbwa *mbwamwitu*

bibi *bibishamba*

(i) askari _____

(ii) bata _____

(iii) punda _____

(iv) mwendo _____

(v) zima _____

(vi) pima _____

(vii) pembe _____

(viii) mali _____

(ix) kanda _____

(x) mwana _____

For online use only

H. Kamilisha jedwali lifuatalo kwa kubadili sentensi kuwa katika wakati uliopo au ujao.

Wakati uliopo	Wakati ujao
(i) ……	Wanafunzi watatuimbia nyimbo nzuri.
(ii) Ng'ombe wetu wanatoa maziwa mengi.	……
(iii) ……	Utakula chakula kingali moto.
(iv) Mtoto anamlilia mama yake.	……
(v) ……	Siku nzima nitasafiri kuelekea kwa babu.
(vi) Leo tunakula wali na maharage.	……
(vii) ……	Mdogo wangu atang'oa jino la pili.

Kazi ya kufanya

Igiza na wenzako igizo ulilolisoma.

Zoezi la 6: Utungaji

A. Tunga igizo lenye wahusika kati ya 5 – 10; wewe uwe mhusika mkuu.

B. Ongeza beti mbili katika shairi hili:

La tano tumemaliza, na sasa tunaliaga,
Tumelifukuza giza, haliwezi kutukoga,
Maarifa ya mwangaza, akili yanatukaga,
Kengele inacharaza, yatwita twende la sita.

For online use only